**21 SEPTEMBA, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Saba – Tarehe 21 Septemba, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na uchambuzi wa taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, tunaanza Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima.

Mheshimiwa Husna kwa niaba.

Na. 95

**Kurasimisha vijana waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi wa mafunzo**

**MHE. HUSNA J. SHEKIBOKO K.n.y. MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kurasimisha vijana waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PATROBAS P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao mkakati kupitia Mpango wa Taifa wa maendeleo wa miaka mitano wa kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa mafunzo kwa vijana 100,000 ifikapo mwaka 2025/2026. Aidha, katika utekelezaji wake hadi kufikia Juni, 2022 kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi jumla ya vijana wapatao 22,296 (kike 3,349 na kiume 18,947) kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara wamerasimishwa ujuzi ikiwemo Singida zaidi ya watu 1,138.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo fani kumi zinazohusika katika urasimishaji ambazo ni uashi, useremala, ufundi magari (makenika), upishi na uhudumu wa hoteli, baa na migahawa, ufundi bomba, unyooshaji bodi za magari, umeme wa majumbani; ushonaji nguona uchomeleaji vyuma. Aidha, kutokana na manufaa wanayoyapata vijana, katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya vijana 18,445 (wa kiume 13,873 na wa kike 4,572) wamejitokeza na kukuziwa uchuzi na kuchukua fomu kwa ajili ya kurasimishwa ujuzi wao kupitia programu hii ambapo taratibu zinakamilishwa ili waweze kupatiwa fursa hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna.

**MHE. HUSNA J. SHEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa ambao ni mafundi, wamekuwa wakikosa kazi kwenye maeneo tofauti tofauti kwa kigezo cha kukosa cheti, na wale ambao wana vyeti wamekuwa wakichukua hizi kazi na kuwa kama madalali, kazi hizi zinakuwa zinatekelezwa na hawa ambao hawana vyeti.

Je, Serikali haioni sasa umuhimu wa kurasimisha kwa kuwapa vyeti hawa mafundi ujenzi, mafundi seremala, mafundi cherehani ili waweze kuajiriwa katika maeneo mbalimbali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pale Lukozi, Wilaya ya Lushoto kuna vijana ambao wanatengeneza maji ya betri kwa ajili ya magari na pikipiki. Lakini jambo hili limezungumzwa mara kadhaa ndani ya Bunge hili lakini bado vijana wale hawajapatiwa namna ya kurasimishwa na kutambulika kama kibaji kipya katika Taifa letu.

Je, Naibu Waziri yupo tayari sasa kutembelea vijana wale na kuwarasimisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA NA VIJANA (MHE. PATROBAS P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika utoaji wa mafunzo haya ya urasimishaji ujuzi, unaenda sambamba na utoaji wa vyeti pia vya mafunzo ili waweze kutambulika na zaidi ya hapo Serikali ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan, tunaenda hatua mbali zaidi hao vijana wanaomaliza vyuo vikuu na kurasimishiwa ujuzi, mbali na kuwapa vyeti, tunawakutanisha na halmashauri ili waweze kupewa fedha kwa ajili ya kuanza kama *start-up capital* katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwapeleka maeneo ya *practical placement* kwa maana ya sehemu ambazo wanaweza wakajifunza kufanya kazi, lakini pia kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaenda sambamba kwa sehemu kubwa zaidi ya 1,800 wamekwishakupata kazi kwa fedha zilizotolewa mwaka jana wa fedha shilingi bilioni tisa na Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, nakubaliana naye kwamba nitawatembelea vijana hao na hata wengine walioko nchini kama wana ujuzi na maarifa makubwa kama hayo wanayoyafanya, Ofisi ya Waziri Mkuu iko wazi muda wote kuweza kuwahudumia, tuendelee kupata taarifa lakini tunaendelea kuwatambua na kuwahudumia, lakini kuweza kuhakikisha tunawasaidia. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Esther Malleko.

Na. 96

**Ujenzi wa Hosteli Shule za Kata**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza mkakati wa ujenzi wa hosteli kwenye shule za kata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa shule kuwa karibu na jamii na kwa muktadha huo Serikali ilielekeza kujengwa kwa shule za kata nchi nzima ili kuwawezesha wanafunzi kusoma karibu na maeneo wanayoishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo kwa sasa wa ujenzi wa hosteli kwenye shule za kata ambazo kulingana na jiografia ya eneo hususani umbali kutoka shule na makazi ya watu wananchi wenyewe wamekuwa wakijenga hosteli hizo na kuweka utaratibu wa kuziendesha na kuzisimamia kulingana na mahitaji waliyonayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Katika kuboresha ufaulu katika shule zetu za kata; je, Serikali ina mpango gani sasa kuweza kukamilisha maabara?

Lakini swali la pili, ni lini Serikali itamaliza upungufu wa walimu hasa wa sayansi katika shule zetu za Mkoa wa Kilimanjaro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali

mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kwamba lengo la Serikali kwa sasa ni kuhakikisha shule zote zinakuwa na maabara na ndiyo maana katika kila mwaka wa fedha tumetenga fedha kujenga maabara katika shule zetu za sekondari za kata nchini. Kwa hiyo, hilo ni kipaumbele chetu ambacho Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ametuagiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, upungufu wa walimu wa sayansi tunautambua na ndiyo maana katika ajira zote ambazo tumekuwa tukizitoa sasa hivi tunawapa vipaumbele pia zaidi walimu ambao wamesoma masomo ya sayansi na tutaendelea kufanya hivyo ili kuondoa hili tatizo la uhaba wa walimu wa sayansi katika shule zetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba shule zote za kata na za Serikali kwa ujumla zinapata hatimiliki?

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mbunge wa Jimbo la Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha shule zote zinakuwa na hati iliki na ndiyo mpango uliopo sasa na tumehamasisha halmashauri zote kutekeleza jambo hilo. Kwa hiyo lipo katika mpango wa Serikali. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ndugulile, kwa niaba Mheshimiwa Jerry Silaa.

Na. 97

**Kuanza kwa Mradi wa DMDP Awamu ya Pili**

**MHE. JERRY W. SILAA K.n.y. MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Je, ni lini Mradi wa *Dar es Salaam Metrpolitan Development Project* awamu ya pili utaanza katika Jimbo la Kigamboni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na Benki ya Dunia juu ya mkopo wa fedha kwa ajili ya Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam Awamu ya Pili *(DMDP)* ambapo Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es Salaam zitanufaika pamoja na Jimbo la Kigamboni. Aidha, maandalizi ya mradi huo yanategemewa kuanza mwezi Januari, 2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silaa.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia jibu la Mheshimiwa Waziri, na ni kweli kwamba kero ya barabara ni kubwa sana kwenye Mkoa wa Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri ameahidi maandalizi yataanza januari, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni lini hasa ujenzi wa barabara za *DMDP* utaanza katika Jiji la Dar es Salaam?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, pamoja na shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa ujenzi wa barabara lami ya Chanika - Womboza inayoanza kujengwa hivi sasa kero ambayo imeliliwa kwa muda mrefu na diwani wa Kata ya Zigiziwa Mheshimiwa Maige Selemani Maganga.

Naomba kuuliza nini kauli ya Serikali juu ya kutenga fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Dar es Salaam kwa kujenga barabara kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Waziri mwenyewe mhusika, baba lao.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kunipa fursa lakini nipongeze majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninaomba nijibu mawili ya Mheshimiwa Jerry Silaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; ni lini Serikali itakamilisha majadiliano na Benki ya Dunia kwa ajili ya kutengeneza barabara Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa miradi hii ni wahakikishie Mheshimiwa Jerry pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam tunashirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha *negotiations* zinaenda haraka iwezekanavyo ili Serikali iweze kufikia makubaliano na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye nini mwongozo wa Serikali kuhusu mapato ya ndani? Nilishatoa maelekezo kwa halmashauri ambazo zinatenga asilimia 60 ya mapato ya ndani kwa ajili ya maendeleo kutoa asilimia 10 kwa ajili ya kutengeneza barabara za mitaa, ukiwemo Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuwaelekeza wakurugenzi ambao wanahusika na kigezo hiki kuhakikisha asilimia kumi inatengwa na hawatengenezi barabara peke yao wanaungana na *TARURA*, kuwa na mpango mkakati mmoja ili wanachokitengeneza tuweze kukipima na kupata uhalisia wa matumizi wa fedha. Hayo ndiyo maelekezo ya Serikali. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hapo hapo simama, huu mradi wa bonde la Jangwani, fedha zilishatoka, wananchi wamefanyiwa tathmini ya nyumba zao miezi saba iliyopita, mpaka leo kuna sintofahamu, kuna nini huko kwenu? Nasikia mara mnataka mjenge daraja kutoka Magomeni mpaka Mjini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *negotiations* kati ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa niaba ya Serikali na Benki ya Dunia inaendelea. Lakini kwa sababu Serikali hii nishirikishi na Waheshimiwa Wabunge, kesho mimi, Waziri wa Ujenzi, Waziri wa Fedha na Mipango na pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam, tuna kikao saa saba kwa ajili ya kujadili jambo hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, majibu yanatosha hayo.

Mheshimiwa Tumaini Bryceson, kwa niaba Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 98

**Ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya – Busanda**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU K.n.y. MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafanya maboresho ya ujenzi na ukarabati Vituo vya Afya Chikobe na Bukoli ili vitoe huduma stahiki kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Jimbo la Busanda kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita kwa mwaka 2023/2024 itatenga kutoka mapato ya ndani shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Kituo cha Afya cha Bukoli. Aidha katika mwaka huo, Halmashauri ya Wilaya ya Geita itatenga shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati katika Kituo cha Afya Chikobe. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, kwa kuwa hivi sasa halmashauri zimejenga zahanati nyingi na vituo vingi lakini maeneo mengi unakuta anayetibu ni muuguzi badala ya mganga. Ni lini Wizara itafanya tathmini kuona kwamba katika kila zahanati na vituo vya afya kuna idadi ya watumishi wanaotakiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Constantine Kanyasu, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishafanya tathmini na tunafahamu upungufu wa watumishi katika vituo vyetu na kweli baadhi ya zahanati bado zinahudumiwa na wauguzi bila kuwa na madaktari na waganga. Lakini kama ambavyo Serikali imeendelea kuweka mpango ni kuendelea kuajiri watumishi, mwaka huu watumishi wameajiriwa zaidi ya 7,600 lakini tutaendelea kuajiri kwa awamu ili kuhakikisha watumishi wanapelekwa kwenye zahanati zetu ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona, Kituo cha Afya cha Mtanila, pamoja na Kituo cha Afya cha Kata ya

Lupa ni vituo vya afya vya muda mrefu na vimechakaa sana. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kukarabati vituo hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya tathmini ya vituo vya afya, hospitali na zahanati zote chakavu sana nchini kote na tumeweka mpango wa kuanza kukarabati kwa awamu. Kwa mfano kwa mwaka huu tutakarabati hospitali 19 chakavu za wilaya, lakini tutakwenda pia kukarabati vituo vya afya chakavu na zahanati chakavu kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya vituo hivyo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 99

**Wananchi wa Micheweni Kuunganishwa na *TASAF***

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wenye sifa wa Shehia ya Njuguni, Majenzi na Chomboni – Micheweni wataunganishwa na *TASAF*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya *TASAF* iliyoanza rasmi mwezi Januari, 2020 unaendelea katika Halmashauri zote 184 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar kwenye vijiji, mitaa na shehia zote ikiwa ni pamoja na zile ambazo hazikufikiwa wakati wa utekelezaji wa kipindi cha kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika shehia ya Njuguni, Kaya 352 ziliandikishwa, Shehia ya Majenzi Kaya 312 ziliandikishwa na Shehia ya Chamboni Kaya 584 ziliandikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaya ambazo hazikutambuliwa na kuandikishwa kwa sababu mbalimbali katika kipindi hiki cha pili utaratibu umeandaliwa kwenda kwenye vijiji, mitaa na shehia zote kwa maeneo yote ya utekelezaji ili ziweze kuandikishwa na kuingizwa kwenye mpango ikiwa zimekidhi vigezo na sifa stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni nimeona baadhi ya wananchi wakifutwa kwenye mpango wakati bado hali zao ni mbaya sana, na naomba nimtaje mwananchi ambaye ni mfano, anaitwa Ndugu Hamad Faki Hamad maarufu Fofofo kutoka Shehia ya Mjini Wingwi, hali yake ni mbaya sana lakini amefutwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa kauli gani kwa *TASAF* dhidi ya hali kama hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali inatoa kauli gani dhidi ya taarifa ambazo zinasambaa kwa wananchi ambazo zinaleta wasiwasi kwamba wanakwenda kufutwa kwenye mpango wakati hali zao bado ni mbaya. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya taarifa hizi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kumpongeza yeye mwenyewe Mheshimiwa Kombo, Mbunge wa Wingwi, kwa sababu pia ni mjumbe wa Kamati ya USEMI ambayo inasimamia Wizara yetu hii Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na amekuwa akifuatilia sana masuala haya ya *TASAF* hasa jimboni kwake kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikienda kwenye maswali yake anauliza ni vigezo gani ambavyo hata huyu amemtaja Mzee Hamad Faki vimemuacha. Sijui hasa kwenye kesi hiyo kama *individual* na nitakaa naye

Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujua kwa nini Mzee Faki alitoka katika mpango wa *TASAF*, tukitoka hapa nitakutana naye ili tuweze kulijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme jambo moja katika mradi huu awamu hii ya pili imekuwa ina *component* mbili; *component* ya kwanza ni ile ambayo tulikuwa tumeizoea kwenye awamu ya kwanza ya mradi huu wa *TASAF*, ni ule wa *cash* kwenda kwenye kaya hizi, lakini *component* ya pili ni *public works.* Kwamba kaya huenda ina watu watano, na mkuu wa kaya anaweza akawa ni mtu mzima labda ana miaka 70 lakini ndani ya kaya ile kuna watu wenye uwezo wa kufanya kazi. Basi watafanya kazi na kulipwa ujira kutoka kwenye mradi wa *TASAF*, kwenye miradi ile ambayo wameibua wao wenyewe katika maeneo yao husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kwenye swali lake la pili, ya taarifa hizi kwamba wanufaika wanaenda kufutwa. Niseme taarifa hizi si za kweli, walengwa hawa hawaendi kufutwa, na tulifanya uhakiki kabla ya kuingia kwenye awamu ya pili ya mpango huu na kaya zimeongezwa. Serikali hii ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo yake mwenyewe alielekeza tuongeze idadi ya kaya kwenye mpango huu wa *TASAF,* na kaya zimeongezwa na hauendi kufutwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri Mheshimiwa Waziri.

Tunaendelea ma Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Kavejuru Felix.

Na. 100

**Biashara ya Uuzaji/Utunzaji wa Hewa Ukaa**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, Serikali ina mikakati gani kuelimisha wananchi wanaozunguka Hifadhi za Misitu kuhusu biashara ya uuzaji/utunzaji wa hewa ukaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Karibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Maziringira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa Watanzania na Serikali inanufaika na biashara ya hewa ukaa. Serikali Kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja na wadau

inaandaa mwongozo na kanuni za usimamizi wa biashara ya hewa ukaa ambazo zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2022. Mwongozo na kanuni hizo zitaonesha namna ya utaratibu na kusimamia biashara hiyo ikiwemo mgawanyo wa manufaa kwa wadau watakaohusika katika mnyororo wa biashara ya hewa ukaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, baada ya kukamilika kwa mwongozo na kanuni, Serikali imejipanga kuendelea kutoa elimu kuhusu biashara ya hewa ukaa kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi ambao ni sehemu kubwa ya biashara hiyo inayofanyika katika maeneo yao. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, katika kuandaa mwongozo huo *TFS* ambao wamekuwa na migogoro na wananchi wanaozunguka hifadhi hizo za misitu wameshirikije?

Swali la pili; je, Serikali haioni haja ya kushuka kwa wananchi na kutoa elimu ya biashara ya hewa ya ukaa ili kujenga ufahamu zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix, Mbunge wa Buhigwe, najibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba moja miongoni mwa wadau ambao watakuwa ni sehemu kubwa ya mwongozo huo ni *TFS* na nimwambie kwamba tumewashirikisha vya kutosha katika mwongozo huu na siyo wao tu; tumeshirikisha taasisi nyingi za kibinafsi na za Serikali, lakini zaidi tumewashirikisha sana Tawala za Mikoa wakiwemo Halmashauri, Majiji, Wilaya, Mikoa na Vijiji ili lengo na madhumuni na wao wawemo katika sehemu ya mradi huo ili watusaidie katika kuwaeleza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuwafikishia taaluma wananchi, hili jambo ni la mwanzo tumelipa kipaumbele na tayari timu ipo imeelezwa katika mpango huo, kutakuwa na timu maalum ambayo itapita nchi nzima kuzunguka kwa ajili ya kutoa kwanza elimu kwa wananchi wafahamu mradi huo na faida zake, lakini wafahamu fursa zinazopatikana katika mradi huo, lakini wafahamu faida za kimazingira ambazo zitapatikana katika mradi huu. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendela na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

Na. 101

**Ugonjwa wa *TB* kutoonekana katika hatua za awali**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, ni kwa nini ugonjwa wa *TB* hauwezi kuonekana kwa mara moja unapompata mwathirika?

**NAIBU SPIKA:**Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa wa *TB* huchelewa kuonekana kutokana na tabia na mwenendo na vimelea vya *TB* kuzaliana taratibu mwilini na mara nyingi hudhibitiwa na kinga ya mwili wa aliyeambukizwa. Hivyo kila mgonjwa ataanza kuonesha dalili za ugonjwa kutegemea hali ya kinga ya mwili wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa wito kwa wananchi kuwahi mapema katika vituo vya kutolea huduma za afya kupimwa mara tu wanapojisikia dalili zifuatazo; homa za mara kwa mara, kikohozi cha wiki mbili au zaidi, kutoa makohozi yaliyochanganyika na damu, kupungua uzito kwa haraka bila sababu ya msingi na kutokwa jasho jingi hasa usiku. Aidha, ninashauri jamii iwe na utaratibu wa kupima afya mara kwa mara ili kutambua magonjwa mapema na hatimaye kuanza matibabu mapema. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dau.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kutoa maswali yangu mawili ya nyongeza.

Kwa kuchelewa kuonekana *TB* Serikali ina mkakati gani ili kuepukana na masuala ya maambukizi? *(Makofi)*

Je, kuna mpango gani wa kutoa elimu kwa umma juu ya ugonjwa huu kwa kupitia warsha, semina au kongamano? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwantumu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anasema kwa sababu ugonjwa wa *TB* unachelewa kuonekana Serikali ina mpango gani wa kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni utafiti, tayari nchi yetu kwa kushirikiana na vyuo vikuu mbalimbali duniani umefanyika utafiti kwenye Hospitali ya Kibong'oto iliyoko Wilayani Siha ambao ulitizama vinasaba vya *TB* ambavyo huko nyuma *TB* ilichelewa kugundulika sana kwa sababu wakati mwingine ukipima unamuona mtu ana *TB,* lakini ni *TB* mfu, sasa imegundulika kupitia Hospitali yetu ya Kibong'oto *technic* ambayo inatumia *RNA* kwa kutumia watafiti wetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri zungumza kwa kifupi, ukianza kutoa *lecture* hapa tutashindwa kuondoka hapa.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Moja ni kwenye kutambua haraka, sasa hivi kuna vipimo ambavyo vimegundulika madaktari wazalendo wa Kitanzania kwa kushirikiana na Wamarekani wamegundua vinaweza kutambua mapema vimelea. Lakini ya pili, tunapeleka huduma chini sasa kwa bajeti ya mwaka huu kuna vituo 1,859 vinakwenda kuwezeshwa kuweza kupima, kuna *ambulance* na *x-ray digital* ambazo ni *movable* zinakwenda kuzungushwa kwenye nchi nzima ambavyo kila mkoa itakuwa na ya kwake kwa ajili kuzunguka kwenye jamii kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amesema warsha na kutoa semina, sasa hivi Serikali imenunua malori ambayo ni hospitali inayotembea ambayo ina *x-ray* yenye *artificial inteligency* ambayo inatembea kila mkoa na kutoa semina na kwenda kwa kongamano, kila mikutano na kuitisha wananchi, kupima pale pale na tiba kutolewa eneo lile lile. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu sahihi.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Latifa Khamisi Juakali.

Na. 102

**Fidia kwa Wananchi Waliopisha Maeneo ya Jeshi – Zanzibar**

**MHE. LATIFA KHAMISI JUWAKALI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha maeneo ya Jeshi kama Chejuu na Dunga, Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamisi Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum kupitia Kundi la Vijana kutoka Mkoa wa Kusini Unguja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uthamini na upimaji wa maeneo ya Chejuu, na Dunga huko Zanzibar umekamilika, vitabu vya uthamini vipo Kamisheni ya Ardhi Zanzibar. Aidha, kukamilika kwa zoezi hili kunasubiri kukakamilika majadiliano yanayoendelea kati ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mara majadiliano hayo yatakapokamilika, Wizara itawasilisha maombi ya fedha kwa ajili ya fidia kwa kutumia kiasi cha fedha kilichotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Mbunge, aendelee kuwaomba wananchi wa maeneo hayo ya Chejuu, Dunga na maeneo mengine waendelee kuwa na subira wakati tukikamilisha majadiliano hayo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Latifa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nikushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanakwenda kuwatia moyo wananchi.

Kwa kuwa suala hili Wizara mmesema kwamba lipo katika mchakato na wananchi hawa bado sasa hivi wanaendelea kuwa na matumaini makubwa, lakini bado wanakosa kushiriki shughuli zao za kiuchumi ikiwa suala la kilimo, suala la ufugaji kwa sababu tayari walishafanyiwa tathmini.

Je, Serikali mnatoa kauli gani kwa wananchi hawa ili waendelee kuwa na matumaini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Mheshimiwa Waziri wananchi hawa itakapokuwa imetoka hiyo fidia; je, muda huo ambao mtakuwa tayari mmeitoa hiyo fidia inakwenda kuendana na thamani ya fedha katika kipindi hicho yaani *value for money*? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, Mheshimiwa Latifa Khamisi Juakali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika jibu la msingi tayari kuna majibu yanayowapa wananchi matumaini, niwaambie tu Mheshimiwa Mbunge wananchi waendelee kuwa na matumaini kwa sababu azma ya Serikali hii ni kuhakikisha kwamba tunaondosha migogoro yote ambayo inakabili baina ya vyombo vyetu vya ulinzi na wananchi; na ndiyo maana katika jibu la msingi tukasema kuna majadiliano yanaendelea baina ya SMZ na Jeshi la Wizara ya Ulinzi. Lakini pia tukasema kwamba tayari tumeshaomba fedha kwa ajili ya kuwalipa fidia. Kwa hiyo, Mheshimiwa ahakikishe watu wake wanaendelea kuwa na matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine kikubwa ni kwamba tutahakikisha kwamba thamani zitakwenda kwa mujibu wa mali zao, ikiwa vipando, ikiwa nyumba, lakini Serikali haitawadhulumu, itahakikisha kwamba wanapata kile ambacho wanastahiki. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Butondo.

Na. 103

**Barabara ya Kolandoto – Mhunze hadi Mwangongo – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza: -

Je, ni lini barabara ya Kolandoto - Mhunze hadi Mwangongo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kolandoto – Mhunze hadi Mwangongo (kilometa 53) kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Zabuni kwa ajili ya kazi hiyo zitatangazwa mwezi Novemba, 2022. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza.

Swali hili ni kuhusiana na habari ya shilingi bilioni moja ambayo imetengwa. Unaweza kuona ni kiasi kidogo sana cha fedha, nilitaka nipate majibu na wananchi wa Jimbo la Kishapu wapate majibu kwamba kiasi hiki cha fedha tafsiri yake ni nini kwa sababu bilioni moja ni kiasi kidogo sana ili na matumini wawe wananchi wa Kishapu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa ukubwa wa barabara hii, hii fedha ambayo imetengwa haiwezi kuikamilisha, lakini nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni utaratibu kwamba barabara hizi hazijengwi kwa siku moja wala kwa mwaka mmoja na ndiyo maana mpango ambao tunautumia kwa kujenga barabara ni ku-*raise certificate*. Kwa hiyo, wakishaanza kila watakapokuwa wamefika hatua nyingine wanaandika *certificate,* wanalipwa na ndiyo utaratibu ambayo tumekuwa nao katika ujenzi wa barabara zetu baada kazi ana-*raise certificate* na Serikali inalipa hizo fedha. Kwa hiyo, ni barabara kuu tunalijua hilo na ndiyo maana tayari tumeanza kuandaa taratibu za kutangaza hiyo barabara. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Sillo.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mbuyu wa Mjerumani kupitia Magala hadi Mbulu kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mbuyu wa Mjerumani kwenda Mbulu ni barabara ambayo ndiyo tumekamilisha usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi kwa kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ipo kwenye mpango, tulichokuwa tunafanya ni kukamilisha usanifu na tukishakamilisha Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Nakumbushia barabara ya kutoka Kibaoni – Mfinga inapita Mto Wisa inakuja kutokea Mloo, barabara hii ni muhimu sana kwa Mkoa wa Rukwa.

Je, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa kwamba barabara aliyoitaja inaunganisha Mkoa wa Mbeya na Rukwa hadi Katavi, ni barabara ambayo tayari upande mwingine imeshakamilika usanifu lakini bado tunaendelea kukamilisha usanifu wa kina kwa kipande kingine tayari tumeshaanza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ameshakuelewa, Mheshimiwa Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, ni lini Serikali itaendeleza ujenzi wa barabara ya lami iliyoishia katika Kijiji cha Elelai kuelekea Kamwanga inayounganisha Wilaya ya Longido na Wilaya ya Siha inayozunguka Mlima Kilimanjaro?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ni barabara muhimu sana iko kule mpakani. Baadhi ya sehemu tumeshaikamilisha na sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuiunganisha barabara yote kwa lami na iweze kupitika kwa urahisi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim, ajiandae Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. IDDI KASSIM IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayotoka Solwa kuja Moktolio – Bulige - Ngaya mpaka Kahama ni barabara iliyoko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na inatakiwa ijengwe kwa muda mrefu sasa. Sasa swali langu ni lini fedha hizi zitatengwa ili barabara hii ianze ujenzi mara moja? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Kwa kifupi sana Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi Kassim, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara niliyoitaja ipo kwenye mpango na ipo kwenye Ilani, kwa hiyo, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili ijenge kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo, ajiandae Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi; nataka nijue ni lini ujenzi wa barabara wa Mbande - Kisewe - Msongola utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni lini tu, usianze tena sijui mchakato sijui nini. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii itaanza kujengwa kama tulivyoipanga kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante majibu sahihi, Mheshimiwa Anatropia, ajiandae Mheshimiwa Suma.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; barabara ya Bugene – Itela - Nkwenda mpaka Kaisho ambazo ni ahadi ya Mheshimiwa Hayati Rais Magufuli, kilometa 50. Ni lini barabara hii itaanza kujengwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kutimiza hiyo ahadi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ahadi lazima itatekelezwa, Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ninaipongeza sana Serikali kwa juhudi iliyofanya baada ya kusikia ajali nyingi zinatokea pale maeneo ya …

**NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa Suma, swali.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali; je, tumepata barabara ya mchepuo ya kilometa tatu ambapo mvua ikinyesha hali itakuwa mbaya zaidi. Je, Serikali ni lini itatujengea barabara ya lami kwa maeneo hayo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mbeya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo barabara tuliyojenga ni kwa ajili ya dharura ili kuepusha ajali zilizokuwa zinatokea. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Serikali sasa ni kuijenga barabara hiyo ya lami. Kwa hiyo, Serikali inatafuta fedha ili iijenge na liwe ni suluhisho la kudumu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kakoso.

Na. 104

**Mgogoro wa Ardhi katika vijiji vya Vikonge na Nomalusambo dhidi ya *TFS* – Katavi**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Je ni lini, Serikali itamaliza mgogoro wa ardhi kati ya vijiji vya Vikonge na Nomalusambo dhidi ya *TFS?*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa ardhi uliokuwepo kati ya Hifadhi ya Msitu wa *Mpanda North East* na Kijiji cha Vikonge ulitokana na kutotambulika mipaka. Wizara kwa kushirikiana na Serikali za Vijiji, wananchi pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi walienda kutafsiri mipaka hiyo. Hivyo, Serikali inahimiza kuendelea kuheshimu makubaliano yaliyosainiwa kati ya Kijiji cha Vikonge na *TFS* juu ya mpaka na hivyo kumaliza mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kijiji cha Nomalusambo ambacho kina kitongoji kiitwacho Ijenje ambacho kiko ndani ya Hifadhi ya Msitu wa *Mpanda North East,* mwaka 2017 kitongoji hiki kiliondolewa katika eneo la hifadhi kupitia zoezi la uondoaji wavamizi msituni ambapo wananchi wa kitongoji hicho walitii maekelezo na kuondoka ndani ya hifadhi. Hivyo, Serikali inashauri wananchi wa Kijiji cha Nomalusambo waendelee kushirikiana na Serikali katika kuhifadhi Hifadhi ya Msitu wa *Mpanda North East* kwa ajili ya manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Msitu wa *Mpanda North East* ulishapoteza hadhi ya uhifadhi kutokana na shughuli za kibinadamu, pamoja na Serikali yenyewe kuchangia kwa kugawa maeneo kuyafanyia shughuli za maendeleo ukiwemo Mji wa Mpanda pale Mpanda Mjini ni eneo la *TFS*, makazi ya Katumba na vijiji vilivyotajwa.

Je, ni lini Serikali itakuja kutatua huo mgogoro kumaliza mgogoro huo kwa kupitia timu ya Mawaziri wanane ambao Serikali ilielekeza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa *TFS* imekuwa na tabia ya kuwapiga wananchi, kuwaibia mali zao kila wanapozalisha mali, kipindi cha uzalishaji mali hawaendi kuwapiga na kipindi cha uvunaji wanakwenda kuwanyang'anya mali zao. Ni lini tabia hii itakomeshwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba pamoja na majibu ya msingi maeneo haya yaliingizwa kwenye timu ya Mawaziri wa kisekta nane ambao walikwenda kuchakata na pia wameweza kufika katika mikoa 13 kutoa maelekezo ya namna ya kutatua changamoto hizi za migogoro. Hivi ninavyoongea sasa kuna wataalam wako katika maeneo hayo ikiwemo Mpanda Vijijini ambako wataalam wamekwenda kufanya tathmini hiyo. Maeneo haya kama kweli yanakosa sifa ya kuwa hifadhi basi yataingizwa kwenye utatuzi wa migogoro ya Mawaziri nane na kisha yataingizwa kwenye ufutaji wa *GN* ambazo zipo tangu mwaka 1947.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa *TFS* kunyang'anya mazao, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna changamoto ya namna hii ambayo imejitokeza, basi naomba nilichukue, twende kulifanyia kazi na wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za kila siku. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii.

Kwa kuwa na sisi katika Kijiji cha Luhimbalilo, Kata ya Mputa, Wilaya ya Namtumbo kumekuwa na fukuto la mgogoro kati ya *TFS* na kijiji hicho kuhusiana na hifadhi ya Matogolo kuingilia eneo la Kijiji cha Luhimbalilo.

Je, Serikali inaweza kuelekeza sasa kikosi cha wataalam wakaja kufanya mazungumzo na kutafsiri hiyo mipaka ili kuondosha mgogoro huo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mimi nilifikiri unasema mje muambatane pamoja? Mheshimiwa Waziri, ajiandae Mheshimiwa Kunti.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kwamba migogoro yote ambayo inatuletea changamoto katika uhifadhi niwaombe Waheshimiwa Wabunge tuipokee ili tuweze kuleta wataalam waweze kufafanua mipaka na pale ambapo pana uhitaji wa namna ya kuachia maeneo kwenye maeneo

ambayo yamevamiwa zaidi tutakaa chini, tufanye tathmini na kisha tuondokane na hii migogoro ya kila siku ili maeneo ambayo tumeyahifadhi basi yaendelee kuhifadhiwa vizuri kwa maslahi ya Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Waziri mlikuja kwenye Kijiji cha Handa Kata ya Lahoda pamoja na timu ya Mawaziri watano na wewe ukiwemo mlikutana na changamoto kubwa sana, kuhusiana na Hifadhi ya Swagaswaga na wananchi walieleza changamoto wanayoipata kutokana na hifadhi hiyo na mkaunda timu ya wataalam kwa ajili ya Kwenda kutafsiri mipaka.

Je, ni lini Serikali itakwenda kuwaeleza wananchi tafsiri ya mipaka hiyo kwa sababu bado wananchi wale wanapigwa, bado wananchi wale wananyang'anywa mazao yao…

**NAIBU SPIKA:** Basi uliza swali, ulishauliza swali.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanadhalilishwa, nataka kujua ni lini mtakwenda kutoa hayo majibu kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri swali lilishaulizwa ni lini? Basi jibu hilo ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kunti, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wataalam kufika katika maeneo hayo na kufanya tathmini niwaombe wananchi waendelee kusubiri maamuzi ya Serikali, wasiendelee kuvamia maeneo hayo na kujichukulia mamlaka ya kwamba tayari tumeyaachia. Ni mpaka pale Serikali itakapotoa tamko kwamba sasa tunaachia eneo hili, basi wananchi waendelee kufanya shughuli hizo.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge wasubiri kuwa tunachakata tutayaleta majibu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, basi tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mdee.

Na. 105

## Madai ya shilingi trilioni 7.91 ya watoa huduma

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali italipa madai ya shilingi trilioni 7.91 ya watoa huduma kama yalivyoripotiwa kwenye ripoti ya CAG 2021?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la shilingi trilioni 7.91 linajumuisha madeni ya wafanyakazi na watoa huduma kwa mashirika ya umma 71. Ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa na kudhibiti uzalishaji wa madeni mapya, mashirika yote ya umma yameelekezwa kuendelea kulipa kwa haraka iwezekanavyo na kuandaa mkakati wa kukabiliana na madeni na kuwasilisha Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati huo, kila taasisi inatakiwa kuonesha namna itakavyodhibiti uzalishaji wa madeni mapya na kulipa madeni yaliyopo. Lengo ni kuhakikisha kuwa kiwango cha madeni kinafikia asilimia mbili ya jumla ya bajeti ya mashirika ya umma ifikapo mwaka 2025. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina na Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali itatumia mkakati huo katika uchambuzi na uidhinishaji wa mapato na matumizi ya kila mwaka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa madeni haya shilingi trilioni 7.9 kama ulivyosema ni ya wafanyakazi, watoa huduma na wauzaji bidhaa na ni ya muda mrefu, hauoni kwamba Serikali mnakuwa sehemu ya kufifisha shughuli za kiuchumi za Watanzania? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; Wizara yako ya Fedha ndio inayomsimamia Msajili wa Hazina, sasa ni lini mkakati huu utakamilika, nataka *time frame* ili mkakati huu upelekwe kwenye Kamati ya Bunge inayosimamia mashirika ya umma kwa ajili ya ufuatiliaji na utekelezaji? Ni lini? *Time frame*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halima James Mdee, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tumelipa madeni yote hasa Serikali ya Awamu ya Sita, tumelipa madeni yote yaliyopo katika Serikali, lakini ni lini mkakati huu utaanza kutumika ni wakati wowote baada ya kupitia na kuhakiki wataalam wetu basi itatolewa taarifa rasmi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo kwa niaba yake Mheshimiwa Suma.

Na. 106

**Ujenzi wa *Safari City* – Arusha**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO** aliuliza:-

Je, ni lini Shirika la Nyumba la Taifa litaanza ujenzi wa *Safari City* nje kidogo ya Jiji la Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Arumeru kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *Safari City* una jumla ya viwanja 1,713 kwa ajili ya uendelezaji wa nyumba na makazi, majengo ya biashara, maeneo ya viwanda vidogo vidogo, huduma za jamii kama shule, hospitali, maeneo ya kuabudia, sehemu za michezo, sehemu za mapumziko na maeneo ya usalama wa mji kama kituo cha polisi na zimamoto pamoja na maeneo ya wazi. Kwa kipindi cha kuanzia Juni, 2022 hadi sasa jumla ya viwanja 970 vyenye thamani ya shilingi bilioni 19.64 vimeuzwa ambapo Shirika la Nyumba la Taifa limekusanya shilingi bilioni 12.33 sawa na asilimia 62.78 ya mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa mradi wa *Safari City* tayari umeanza ambapo mamlaka zinazohusika zinaendelea na uwekaji wa miundombinu

muhimu ya barabara, maji na umeme. Pia Shirika la Nyumba la Taifa tayari limejenga nyumba 10 za gharama nafuu za mfano kuwawezesha wanunuzi wa viwanja takribani 23 kuanza ujenzi ambapo baadhi yao tayari wamehamia katika makazi yao.

Aidha, baadhi ya taasisi za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha *(AUWSA)* na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Ufundi Stadi *(NACTVE)* zinaendelea na ujenzi katika eneo la mradi. Vilevile Taasisi nyingine ni pamoja na *LATRA*, *OSHA* na *EWURA* zimekamilisha ununuzi wa viwanja na zinatarajia kuanza uendelezaji katika viwanja vyao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mkoani Mbeya Wilayani Rungwe maarufu kama Tukuyu hakuna Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi yapata miaka minne sasa ambapo Halmashauri ya Busekelo inategemea hapo na tatizo hilo Mbarali kuna tatizo hakuna pia Mwenyekiti na Chunya, ukizingatia wananchi wa Chunya wanatoka mbali kabisa Kambi Katoto wanakwenda Mbeya Mjini ambapo ni karibu na Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Sasa je, Serikali ni lini itatupelekea Wenyeviti Baraza la Ardhi kwenye Wilaya hizo? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Wizara inaendelea na utaratibu, ni maeneo mengi hayana Mabaraza haya, kwa hiyo Wizara inaendelea kufanya matayarisho kwa ajili ya kuajiri Wenyeviti wa Mabaraza na moja ya watakaoajiriwa tuta-*consider* hilo eneo la Tukuyu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo kama Njombe ambayo ni Miji inayokua inauhitaji mkubwa sana wa makazi kwa sasa na maofisi. Ni lini, Shirika la Nyumba litakwenda kuanza mpango wa kujenga nyumba katika maeneo hayo ya Njombe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Deo, Mbunge wa Njombe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi *National Housing* inafanya mabadiliko makubwa sana ambayo yanakwenda kuanzisha ujenzi katika maeneo mengi sana ya nchi na hasa pembezoni mwa miji ambayo kwa kweli ilikuwa imesahaulika. Nikuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwenye eneo lako hilo muweze kuandaa maeneo ambayo shirika litakapofika lipate ushirikiano wa kupata maeneo ya kujenga nyumba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Shirika la Nyumba lina nyumba nyingi ambazo ni chakavu na ukarabati wake umekuwa ni changamoto kubwa sana hususani kwenye Mkoa wa Tabora hasa Manispaa ya Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kukarabati nyumba hizi na kama wameshindwa basi waziuze? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Tabora, Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi ukarabati unaendelea nchi nzima na kwa sababu hawawezi kufanya vitu vyote kwa pamoja, ndio maana unaona kama Tabora wamechelewa kidogo. Hatuna mpango wa kuuza nyumba zile kwa sababu zinaendelea kuwasaidia watumishi mbalimbali ambao wanazitumia kwa ajili ya kupunguza ile uwezekano wa kukosa nyumba katika maeneo ambayo wanakwenda.

Kwa hiyo, nipende tu kusema kwamba ukarabati unaendelea nchi nzima na muda mfupi ujao mtafikiwa Tabora, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 107

**Kupeleka Wapimaji wa Ardhi Mji wa Tukuyu**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Wapimaji wa Ardhi katika Mji wa Tukuyu Wilayani Rungwe ili kupunguza migogoro ya ardhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina watalaam wa sekta ya ardhi ambao ni Maafisa Ardhi, Mpima Ardhi na Afisa Ramani ambao wanaendelea na utaratibu wa shughuli za ardhi katika Halmashauri hiyo ikiwemo kushughulikia mgogoro wa ardhi. Aidha, Mkoa wa Mbeya una timu ya wapima ardhi ambayo kukiwa na uhitaji wa kupima eneo katika Halmashauri za Mkoa wa Mbeya timu hiyo hushiriki katika kazi za kupima katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Mbeya itapeleka timu ya wataalam wa ardhi katika Wilaya ya Rungwe tarehe 26 Septemba, 2022 ili kushughulikia kero na mgogoro wa ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kimsingi ninaishukuru Serikali baada ya kupiga kelele kwa muda mrefu imetuletea Mpima mmoja katika Wilaya ya Rungwe.

Swali langu la kwanza; ni kwa nini msiongeze Mpima mwingine kwa sababu Wilaya ya Rungwe ina vitongoji 502 hivyo uhitaji wa Wapima ni mkubwa sana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili tuna shughuli inayoendelea katika Wilaya ya Rungwe ya upimaji wa vijiji 11 katika upimaji huo tunashukuru Serikali mmeleta shilingi milioni 500 na inafanya *revolving fund* kwa wananchi kulipa shilingi 30,000 ili wapimiwe.

Ni kwa nini Serikali msiongeze fedha ili wananchi hawa watoe angalau shilingi 15,000 kuwapunguzia makali katika upimaji wa viwanja hasa kwenye vijiji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nipende kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na lile swali dogo la kwanza ambalo linaomba nyongeza ya watumishi katika sekta ya wapima kwa sababu wanaye mmoja. Wizara inalichukua na bado inaendelea kulifanyia kazi na upo uwezekano wa kuongeza maofisa hao kulingana na jinsi tutakavyokuwa tumejijengea uwezo wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili kuhusu suala la kuongeza fedha ni kweli kabisa kwamba jambo hili ni muhimu na tumelipokea kwanza kwa uzito wa kutosha ili baadae tukalifanyie kazi na kuona uwezekano wa kupata vyanzo vya fedha kwa ajili ya kuongeza nguvu ingawa hatutarajii wapunguziwe thamani ile wanayolipa sasa kwa sababu nayo vilevile inasaidia kuongeza uharakishwaji wa zoezi hili. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Fatma Toufiq.

Na. 108

**Wataalamu wa zao la zabibu Dodoma**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wataalam wa zao la zabibu Dodoma?

**NABU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania *(TARI)* imepata kibali cha kuajiri watumishi wapya 100 na wengine 68 kuhamia *TARI* kutoka Wizarani wakiwemo Maafisa Kilimo ambao watapelekwa katika vituo vya utafiti ikiwemo Kituo cha Uendelezaji wa Zao la Zabibu *TARI* Makutupora. Mkakati uliopo ni kuwajengea uwezo wa kutosha

wataalamu waliopo kwa kuwapatia mafunzo mahsusi ya kilimo cha zabibu na kujifunza teknolojia mpya za kilimo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la zabibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Toufiq.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nishukuru sana kwa majibu ya Serikali, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali haioni imefikia wakati wa kutenga bajeti maalum ili kuweza kuwapeleka baadhi ya wataalam wa kilimo katika zile nchi ambazo zimekuwa zikizalisha zabibu kwa wingi ikiwemo Afrika ya Kusini, China na Spain? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo wataalam wetu na hivi sasa tumekamilisha mazungumzo na wenzetu wa Afrika ya Kusini, Ufaransa na Israel kwa ajili ya kuwapeleka wataalam wetu kwenda kujifunza maeneo mbalimbali, ikiwepo ubunifu na uzalishaji wa mbegu bora na udhibiti wa magonjwa wa wadudu pamoja na mbinu bora za kilimo za shambani yaani *agronomy.*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mheshimiwa Kihenzile.

Na. 109

**Idadi ya wawekezaji katika kipindi cha miaka kumi**

**MHE. DAVID M. KIHENZILE** aliuliza:-

Je, kwa miaka kumi ni wawekezaji wangapi wa nje walionesha nia ya kuwekeza na kufanikiwa na upi mkakati kwa ambao hawajafanikiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kusini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* jumla ya miradi 4,543 ilisajiliwa katika kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2021 ambapo mitaji yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 53.1 ilitarajiwa kuwekezwa na kutoa ajira 654,260. Kati ya miradi hiyo, miradi 3,304 ilitekelezwa sawa na asilimia 72.7 ya miradi yote iliyosajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuweka mikakati mbalimbali ya kufanikisha uwekezaji ikiwemo kuimarisha matumizi ya TEHAMA, dirisha moja la kuhudumia wawekezaji, kuboresha na kujenga miundombinu wezeshi, vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi na kutenga maeneo kwa ajili ya wawekezaji. Nakushukuru.

**NAIBUU SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina swali la nyongeza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Mwita Mwikwabwe kwa niaba yake Mheshimiwa Jafari Chege.

Na. 110

**Wananchi wa Tarime na Rorya kupata bidhaa kutoka Kenya**

**MHE. JAFARI W. CHEGE K.n.y. MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawawezesha wananchi wa Jimbo la Tarime Vijijini, Tarime Mjini na Rorya kupata bidhaa kutoka nchi jirani ya Kenya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na inatekeleza makubaliano ya hatua ya pili ya ushirikiano ya Soko la Pamoja ambapo wafanyabiashara kutoka nchi wanachama wameruhusiwa kusafirisha bidhaa kutoka nchi moja kwenda

nchi nyingine kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa katika nchi husika. Hivyo, kutokana na mazingira hayo, Serikali haijaweka zuio lolote la bidhaa kutoka nchi jirani ya Kenya kuingia Tanzania. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, Wilaya ya Rory ana Tarime moja ya faida ambayo tunaipata kuwepo mpakani kati ya Tanzania na Kenya ni pamoja na unafuu wa bei ya bidhaa ambazo zinazalishwa maeneo ya mpakani.

Swali la msingi hapa lilikuwa linauliza Wizara haioni kuna umuhimu sasa wa kuwasaidia wale wachuuzi wadogo ambao unakuta bidhaa chache, kwa mfano mifuko miwili ya *cement,* mifuko mitano ya sukari ambayo wakikamatwa wakati mwingine hupewa kesi za uhujumu uchumi au hunyang'anywa pikipiki zao au kutaifishwa bidhaa zao zile chache. Mheshimiwa Waziri haoni kuna umuhimu wa kuwasaidia hawa wafanyabiashara wadogo ili kutengeneza mazingira rafiki angalau waweze kufanya biashara hizi bila usumbufu wanaopata?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Wilaya ya Rorya tayari tuna eneo ambalo tumelitenga kwa ajili ya kuweka viwanda kwa mahitaji na muktadha wa bidhaa hizo hizo ambazo wananchi wetu wanavuka kwenda kuzifata Kenya.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha angalau inazungumza na wawekezaji wa bidhaa hizi hizi wanazozalisha Kenya kujenga kiwanda, kuja kuwekeza maeneo ya Rorya ili tuwasaidie hawa wananchi wanaovuka maeneo ya mpaka kwenda nchini Kenya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja ya mikakati ambayo tunayo Serikali ni kuona namna gani tunawasaidia wachuuzi au wafanyabiashara wadogo wadogo, wajasiriamali katika mikoa ya mipakani ambao wanafanya biashara kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maelekezo ambayo tulishawaelekeza maafisa wetu wa taasisi zote zinazohudumia wafanyabiashara mipakani ikiwemo *TRA, TBS* na nyingine kuhakikisha kwanza wanatoa elimu kwa wachuuzi hawa wajasiriamali namna ya kufanya biashara kati ya nchi moja na nyingine. Lakini zaidi waendelee kuwasaidia

kwa maana ya kuwapa muda fulani kama angalizo wakati wanaendelea kujifunza namna ya kufanya biashara kati ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la pili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya mikakati yenu ni kuona tunawavutia wawekezaji katika kujenga viwanda maeneo ya mipakani ikiwemo katika eneo la Rorya. Kwa hiyo, hilo tutalifanya na tutachukua kwa uzito mkubwa nimwakikishie Mbunge tutalifanya hilo tutashirikiana naye, nitawasiliana naye baada ya kikao hiki. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Matiko.

Waheshimiwa Wabunge naomba utulivu ndani ya Bunge.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; ni kweli kumekuwa na kero kubwa sana kwa hawa wafanyabiashara wadogo wanaokutwa wanafata bidhaa upande wa pili Kenya. Ni kwa nini sasa Serikali isielekeze *task force* iache huu utaratibu wa kufukuzana na hawa wafanyabiashara wadogo ambapo wakati mwingine inapelekea vifo kwa kuwagonga ili kuwepo na utaratibu wa kiofisi kama mtu amekwepa kodi basi anafatiliwa kuliko wanavyofanya sasa hivi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan imeshasema na tumeshaelekeza kwamba tuwahudumie wafanyabiashara na hasa tukiwa na lengo la kujenga sekta binafsi yenye nguvu kuhakikisha kwamba wanafanya biashara zao vizuri bila kero. Kwa hiyo, nilichukue hili ili tuone kama kweli shughuli hizo zinafanyika, kero hizo au *task force* hizo ziweze kukomeshwa mara moja kuhakikisha wanawasaidia badala ya kuwa-*harass* wafanyabiashara.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Ndaisaba kwa niaba Mheshimiwa Oliver.

Na. 111

**Kuunganisha Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MHE. NDAISABA G. RUHORO** aliuliza: -

Je, ni lini mifuko ya kuwezesha wananchi kiuchumi itaunganishwa ili kuleta tija na manufaa kwa Watanzania hasa waishio vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, Mbunge wa Jimbo la Ngara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara inaratibu utekelezaji wa mifuko na programu 62 za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha tathmini ya mifuko na programu za uwezeshaji ishirini. Napenda kutumia fursa hii kukujulisha kuwa, Serikali inafanyia uchambuzi wa kina taarifa ya tathmini hiyo na kuja na hatua za kuchukua ili kuboresha utoaji wa huduma wa mifuko husika. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ilitueleza kwamba kuna viwanda vya kuanzia 3,500,000 na katika Mkoa wetu wa Kagera kina mama wamekuwa wakikopeshwa mikopo isiyo na tija.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwakopesha hivyo viwanda badala ya pesa ili kutengeneza ajira nyingi mkoani kwetu Kagera? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Oliver Semuguruka, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Kagera kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa sababu amekuwa akifatilia sana kuhusiana na wafanyabiashara wakina mama wajasiriamali katika Mkoa wa Kagera. Nimshukuru sana kwa kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Oliver. Lakini kuhusiana na mitaji hii ni kweli wajasiriamali wadogo hasa akina mama tunataka kupitia Shirika letu la Viwanda Vidogo kuwakopesha viwanda au

teknolojia rahisi za kufanyia biashara zao badala ya kuwapa fedha ambazo wakati mwingine zinaweza kutumika katika malengo yasiyokusudiwa.

Kwa hiyo, moja ya mikakati ni hiyo kuwapa viwanda ili iwasaidie kuzalisha bidhaa ndogondogo pia waweze kukidhi mahitaji ambayo wameomba katika mikopo hii. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA;** Mheshimiwa Condester.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Je, ni upi mpango wa Serikali kupitia Wizara hii ya Uwekezaji kuangalia yale makundi ya asilimia 10 ambayo hayana vigezo vya kukopeshwa. Kwa mfano wanaume ambao wamepita umri wa vijana kwa ajili ya kuwawezesha, lakini pia kwenye asilimia 10 zipo baadhi ya halmashauri hazina uwezo kukidhi makundi yote asilimia 10. Ipi kauli ya Wizara hii kuwawezesha makundi hayo ambayo yanabaguliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufatilia kuhusiana na asilimia zinazotengwa kwa ajili ya kuwakopesha akina mama…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri subiri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu kwa kweli hata hapa mezani hatusikii majibu ya Waziri, sijui huko kwenu mnasikiaje. Mheshimiwa Waziri endelea.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Condester Sichalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mbunge kwa kufatilia kuhusiana na asilimia 10 za fedha zinazotengwa kwenye halmashauri zetu ili kuwasaidia akina mama, vijana na wenyeulemavu katika kufanya biashara zao ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mikakati ya Serikali sasa ni kuona makundi haya kwanza yanapata elimu ya ujasiriamali kupitia wataalamu

wetu wa Maafisa Biashara katika halmashauri pia kwa kushirikiana na Shirika letu la Maendeleo ya Viwanda Vidogo *(SIDO)* ili waweze kutimiza malengo ambayo wamekusidia katika mikopo hiyo. Lakini zaidi tutaangalia namna ya kuwezesha zile halmashauri ambazo kidogo zina mapato machache ili nao waweze kutosheleza mahitaji katika kuwakopesha vijana na akina mama ambao wanahitaji mikopo kwa ajili ya kufanya biashara zao katika halmashauri zetu na majimbo yetu. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Chaya.

Na. 112

**Hitaji la Chuo cha *VETA* - Wilayani Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Manyoni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Jimbo Manyoni Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inayo azma ya kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni mia moja kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 62 kwa Wilaya ambazo zilikuwa hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi. Aidha, Wilaya ya Manyoni ni miongoni mwa Wilaya hizo 62 ambazo zipo kwenye mpango wa kujengewa Vyuo vya Ufundi Stadi kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa ambapo Serikali inaendelea na hatua hizi, nashauri wananchi wa Wilaya ya Manyoni wakiwemo wa Jimbo la Manyoni Mashariki waendelee kutumia Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Singida, na Chuo cha Wilaya ya Ikungi, Pamoja na Vyuo vya Singida vya *FDC* na vyuo vingine vya ufundi stadi vilivyopo hapa nchini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii kuishukuru sana Serikali kwa ajili ya kuingiza Wilaya ya Manyoni katika

mpango wa kujenga Chuo cha *VETA* mwaka huu, lakini ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa tuna vijana wengi wanamaliza kidato cha nne hawaendelei kidato cha tano na vijana wengi wanamaliza kidato cha tano na sita hawaendelei vyuoni; je, nini mpango wa Serikali kuifanya elimu ya ufundi kuwa *basic education* yaani elimu ya msingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa sasa hivi tuna uhitaji mkubwa sana wa elimu ya ufundi hasa hasa kwa ajili ya uzalishaji viwandani; nini mpango wa Serikali na Wizara kutoa mikopo kwa vijana ambao wanaenda kusoma elimu ya ufundi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Serikali inakusudia kama nilivyosema kujenga vyuo vya ufundi katika Wilaya zote hapa nchini na sasa hivi zimebaki wilaya hizo 62. Kwa hiyo, ujenzi utaendelea na kuhakikisha kwamba vyote vinafanya kazi kwa ajili ya wanafunzi kuweza kusoma humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa sababu sasa hivi tunapitia mitaala na kazi mojawapo kubwa ya kupitia mitaala ni kuongeza elimu ya ujuzi, ujuzi ikiwa ni pamoja na ufundi, tunaamini tutakapokamilisha kazi hii rasimu zitakamilika mwisho wa mwaka huu maamuzi mwakani, tunaamini kwamba tutakuja na mkakati ambao utaongeza mafunzo ya ufundi na ujuzi katika shule zetu kuanzia darasa la kwanza kwenda mpaka elimu ya kidato cha sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili kuhusu mikopo. Kwa sasa hivi kwa kweli Serikali haitoi mikopo kwa ajili ya kwenda kwenye vyuo vya *VETA,* lakini tumefanya mazungumzo na Benki ya NMB kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaweza tukatoa mikopo kwa wale ambao wana miamala inayopitia kwenye benki hiyo kwa ajili ya kusaidia wanafunzi kusoma kwenye vyuo vyote ikiwa ni pamoja na vyuo vya ufundi.

Kwa hiyo, tunaamini kwamba itasaidia kupunguza adha ya wanafunzi kutopata mkopo lakini tutaendelea kutafuta mikakati mizuri zaidi kuhakikisha kwamba tunatoa fursa ya mikopo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kapinga.

**MHE. BENEYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Wilaya ya Mbinga hatuna Chuo cha *VETA* na tulipata ahadi ya Serikali kwamba awamu hii tutaingia kwenye mpango wa kujengewa Chuo cha *VETA,* tayari tuna eneo. Ni lini sasa chou hiki kinaenda kuanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi ni lini.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema Wilaya zote ambazo hazina Vyuo vya *VETA* tunaanza kujenga *VETA* mwaka huu tumekubaliana kwenye hizo bilioni 100 ambazo tumezipata kutoka Hazina tutaanza ujenzi mwaka huu na mwakani tutapata bilioni 100 nyingine na kumalizia ujenzi. Kwa hiyo, tutafanya hivyo pamoja na Wilaya ya Mbinga na ujenzi utaanza siku za karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu kwa Wabunge wote ni kwamba kuhakikisha tunapata maeneo mapema, tunapata hati miliki ili tuweze kujenga kwa sababu hatuwezi kwenda kujenga chou mahali ambapo hatumiliki ardhi chini ya utaratibu wa *VETA*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Maimuna Pathan.

Na. 113

**Wavuvi wanaotumia *ring net***

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itabadili utaratibu kuwataka wavuvi wanaotumia *ring net* kutoruhusiwa kuvua mchana na kuvua chini ya mita 50?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya wavu wa *ring net* wakati wa usiku yanawezesha kuvua samaki wanaolengwa yaani dagaa pekee na kupunguza uwezekano wa kukamata samaki wasiolengwa yaani *by-catch*. Aidha, matumizi ya wavu wa *ring net* kwenye kina cha mita 50 wakati wa maji kupwa kwa upande wa baharini na katika umbali wa mita 1,000 kutoka ufukweni kwenye visiwa na rasi kwa upande wa Ziwa Tanganyika yanawezesha kuwa na uvuvi endelevu kwa kutovua samaki wachanga na kutosababisha uharibifu wa maeneo ya mazalia, makulia na malisho ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wavuvi pamoja na wadau wa uvuvi kudhibiti matumizi ya zana haramu katika shughuli za uvuvi ikiwemo matumizi ya *ring net* kwenye kina cha maji chini ya mita 50 na wakati wa mchana ili kuwa na uvuvi endelevu. Hivyo, kupitia Bunge lako tukufu; Serikali inatoa wito kwa jamii za wavuvi kuendelea kuzingatia sheria za nchi katika kulinda rasilimali za uvuvi kwa manufaa ya sasa na ya kizazi kijacho.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, huoni kwamba kuvua samaki usiku wakiwa wamelala unaweza ukavua samaki hata wale ambao hawajalengwa? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini Serikali itabadilisha au itafanya marekebisho ya kanuni ya mwaka 2020, kipengele cha 66(b)(b), 66(f)(f), 66(g)(g) na kipengele 128(1) ambacho kina faini ambayo haitekelezeki kwa wavuvi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba nitoe ufafanuzi katika suala hili la kuvua samaki usiku. Kuvua samaki usiku kuna uwezekano wa samaki wale wadogo kuwa karibu zaidi ya kina 50 kuliko wale samaki wakubwa, lakini pia uvuvi wa kutumia *ring net* unasababisha kuchukua mazalia ya samaki pamoja na mayai ambayo yanaweza yakaondoa uvuvi

endelevu katika mazalia ya samaki na hivyo kufanya maeneo haya yasiwe endelevu kiuchumi na kiuvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la lini Serikali itabadili kanuni; mchakato wa kanuni hizi unaendelea, hivyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Bunge, muda ukifika zitakuja kwenye kamati husika na kanuni hizi zitafanyiwa marekebisho, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asya.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imefikia wapi katika kuwasaidia wavuvi ili waweze kupata vifaa vya kisasa na waweze kuvua uvuvi wenye tija?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na zana bora za uvuvi, na kwa mwaka huu wa fedha tayari wavuvi wameshapata taarifa na wameshaanza kufanya maombi na zana hizi watakazopewa zitakuwa hazina riba, watapewa mikopo ambayo haina riba ili kufanya uvuvi uwe ni uvuvi endelevu na wa kisasa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na uvuvi wa mita 50 yanaenda kinyume kabisa na uhalisia katika maeneo yote ya ukanda wa pwani. Wavuvi wetu wa Mtwara, Lindi, Pwani, Kilwa, Tanga ni wavuvi wa kawaida ambao hawana uwezo wa kuvua kina cha mita 50 ambayo ni bahari kuu. Katika mabadiliko ya kanuni yanayokuja, Serikali iko tayari kuondoa kikwazo hiki cha uvuvi wa mita 50?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tulipokee wazo lake na tutalifikisha kwa wataalamu, watalichakata na majibu yatatoka katika Bunge lako tukufu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aida.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni hizi ambazo zinaandaliwa, Ziwa Tanganyika tuna-*share* zaidi ya nchi moja, lakini nchi nyingine kwenye ziwa hilo hilo wanavua mchana. Hamuoni kama zuwio hilo linawapa umasikini wavuvi wa nchi yetu na mbadilishe ili waendelee kunufaika na Taifa letu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Waheshimiwa Wabunge watambue kwamba rasilimali za uvuvi ni rasilimali za muhimu sana ambazo zinahitaji kuwa na uvuvi endelevu. Kwanza Serikali inafanya kuyalinda maeneo haya, kuyasimamia vizuri, lakini pia kuyahifadhi ili kuwepo na uvuvi endelevu. Hivyo tunavyoelekeza namna ya kutumia uvuvi wa kisasa na ni uvuvi endelevu kwa kuyafanya mazalia ya samaki yaendelee kuwa endelevu wananchi wanapaswa kufuata taratibu na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii ina lengo la kuhakikisha kwamba, tunalinda maeneo haya ili tuwe na uvuvi endelevu, tunapoyamaliza haya mazalia ya samaki tutahakikisha uvuvi usiwepo kabisa hapa nchini. Kwa hiyo, tunaendelea kuwaomba wananchi waendelee kufuata sheria zilizopo ili kufanya uvuvi uwe uvuvi endelevu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha. Sasa ni wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Wageni walioko Jukwaa la Spika; wageni wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Yasushi Misawa, Balozi wa Japan nchini Tanzania na mwakilishi wa Japan katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

*Welcome to the Parliament Your Excellence. Welcome to the Parliament, thank you very much. (Makofi)*

Yupo pia Ndugu Benedict Faustine Kikove, Mshauri Mwandamizi wa Siasa, Mawasiliano na Utamaduni Ubalozi wa Japan. *(Makofi)*

Ndugu Abdallah Said Kirungi, Afisa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mc Pilipili, karibu. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge, wasimame kwa pamoja, karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 75 wa Shule ya Msingi Iwondo kutoka Mpwapwa, Mkoani Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa kuna jambo hapa bado halijakaa vizuri huko Serikalini na hasa suala la mfumo wa ukusanyaji mapato. Limepigiwa kelele na Mheshimiwa Rais, limepigiwa kelele na Mheshimiwa Spika, sisi wote tunalipigia makelele, lakini bado inaelekea mnavutana na kuendelea kuvutana ni kuendelea kukosa mapato. Bandari yetu ya Dar es Salaam inakusanya bilioni 95 tu kwa mwezi, kuna bandari nchi jirani inakusanya *almost* bilioni 300 kwa mwezi. Kwa hiyo, hii inatokana na mifumo hii kutokuunganishwa, mapato mengi yanapotea, hilo moja. *(Makofi)*

La pili, Tanzania hatuna *GDP* kwenye *internet, sovereignty* ya *internet gateway* iko nje ya nchi, kwa maana hiyo, pesa zinakwenda nje ya nchi tunapowasiliana kutumia *internet* sisi. Tunao *service providers,* lakini na wao vilevile wanalipa hizi pesa nje ya nchi.

Sasa mimi nikuombe Mheshimiwa Nape, wewe ni mtaalamu na wewe ndio mwokozi wa nchi hii, tunakutegemea wewe ufanye haya mabadiliko nchini mwetu, tupate pesa nyingi kwenye *internet. (Makofi)*

Sasa hivi mapato mengi ya simu sio kwenye *voice call* ni kwenye *data, that is where the money is.* Kwa hiyo, nikuombe wewe na Wizara yako mshirikiane na Wizara ya Fedha muweke mkakati maalum wa kuhakikisha *gateway* ya *internet* ibaki nchini na mapato haya yabaki nchini tusilipe nje ya nchi na *internet* inaweza ikawa-*decentralized* maeneo mengi nchini hata vijana hawa wakawa *service providers.*

Najua sio jambo dogo, litapigwa vita kwa sababu ni suala la pesa. Hapa tunazungumzia *national interests,* kumsaidia Rais apate mapato, kuwasaidia vijana wapate ajira ya kuwa *service providers* na wao kwenye *internet. (Makofi)*

Lingine jana Serikali imetangaza kupunguza gharama hizi za miamala, lakini wananchi wengi wanailalamikia kodi ya Serikali, hawatizami mapato

yanayokatwa na benki, hawatizami mapato yanayokatwa na kampuni za simu. Lazima hii iwe *regulated,* benki unatuma pesa wanachukua pesa nyingi zaidi ya Serikali kwa asilimia kubwa sana, lakini Serikali imejenga madarasa na vituo vya afya ndio inayolaumiwa. Kwa hiyo, kuna ki-*syndicate* ambacho kinatengenezwa kuipiga dongo Serikali wakati pesa wanachukua watu wengine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili nalo mlitizame ni namna gani mta-*regulate* mapato ya benki kupunguza gharama za *service charges* zao pamoja na gharama za simu. *(Makofi)*

Mimi niwaombe wananchi, pamoja na sisi Wabunge, unapotuma pesa, tizama *breakdown* ya pesa inavyoandikwa utaona *levy* ya Serikali iko chini sana na mapato wanayochukua kampuni za simu na *financial organisations* yako juu zaidi ya mapato inayoyapata Serikali.

Lingine la mwisho, Serikali imeanza kuwa na majibu marefu Bungeni. Tumeanza kuona kuanzia wiki hii majibu yanakuwa marefu sio kama mlivyoanza. Kwa hiyo, tuwaombe na tulishapewa Mwongozo wa Mheshimiwa Spika maswali mwisho saa 4:30 asubuhi, lakini lazima maswali yote yaishe. Na tunajaribu ku-*manage* hiyo *time,* lakini majibu ya Serikali yakiwa marefu sana Kiti kinapata taabu ku-*manage* hizi *time*. Ahsante.

Katibu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa jambo lililotokea mapema na hususan Kanuni ya 53(1) juu ya maswali kujibiwa kikamilifu.

Nimeuliza swali langu namba 105 kwa Wizara ya Fedha, ambapo Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anajibu hapa, maswali ambayo Serikali imeyapata zaidi ya miezi miwili, mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niliuliza maswali mawili ya nyongeza, swali la msingi lilikuwa linahusu ni lini Serikali italipa madai ya shilingi trilioni 7.9 yanayodaiwa na watoa huduma na wafanyakazi na wauzaji wa bidhaa? Likajibiwa kama alivyojibu swali la msingi, nikauliza maswali madogo mawili ya nyongeza; la kwanza nikasema kwa kuzingatia madai hayo ni ya muda mrefu sana, Serikali haidhani kwamba inashiriki kufifisha shughuli za uchumi za wananchi? Sikujibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikauliza swali la pili kwa sababu Naibu Waziri alisema kwamba wamempa Msajili wa Hazina dhamana ya kufanya uchunguzi na kutoa maelekezo, nikauliza; kwa kuwa Wizara ya Fedha ndio inamsimamia Msajili wa Hazina ni lini hiyo kazi aliyopewa Msajili wa Hazina itakamilika ili Kamati ya Bunge inayosimamia mashirika haya iweze kuipitia kwa ukamilifu ili madeni haya yalipwe? Majibu niliyopewa na Waziri; ni wakati wowote baada ya kupita na kuhakiki wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kunakuwa hakuna *seriousness* ya kujibu maswali ya msingi. Sasa Mawaziri hawa wamepewa dhamana ya kumsaidia Rais, sasa ifike kipindi watekeleze wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba Mwongozo wako ili Mawaziri hawa ama wayajibu sasa hivi ama kama hawajajiandaa wakajibu maswali haya mawili kiukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo tu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Halima kwa kuomba Mwongozo.

Majibu ya kiti, Kanuni ya 53(4) kinasema kwa uhakika kabisa, iwapo Spika ataridhika kuwa swali halikujibiwa kiufasaha ataagiza swali hilo lirudiwe tena kwenye Bunge lijalo. Kiti kitaomba *Hansard* ikipatie majibu na Kiti kikiridhika kuwa swali halikujibiwa sahihi basi swali hilo litarudiwa kwenye Bunge lijalo, laa kama limejibiwa kwa usahihi basi itakuwa ndio imekwisha. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Hoja za Kamati.

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti.

Ahsante Mwenyekiti kuja bila kuitwa, unaokoa muda. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza; kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, naomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika binafsi kwa kuona umuhimu wa kuiweka Taarifa hii kwenye Orodha ya Shughuli za leo za Bunge akitumia madaraka yake chini ya kifungu cha 11(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inakusudia kubainisha matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni na kuwekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Tano wa Bunge. Aidha, taarifa hii inalijulisha Bunge yaliyobainika katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Kwa msingi huo, natanguliza maelezo kuhusu mipaka na masharti ya uchambuzi na njia na mbinu zilizotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipaka na masharti ya uchambuzi; naomba kulibainishia Bunge mipaka ya maudhui ya taarifa hii inayojikita kwenye uchambuzi wa sheria ndogo na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Kwa ujumla, taarifa hii imeishia kwenye sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge na utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo yaliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia na mbinu zilizotumika; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge kuhusu kubainisha njia na mbinu zilizotumika, naomba kulijulisha Bunge kuhusu njia zilizotumiwa na Kamati hadi kupata Taarifa hii. Njia hizo ni kusoma matini *(text)* ya sheria ndogo na matini ya sheria mama kwa lengo la kuchunguza dhamira ya sheria. Njia nyingine ni kutafakari madhumuni ya sheria ndogo inayohusika ikilinganiishwa na nia ya Bunge kukasimu utungwaji wa sheria ndogo pamoja na kuzingatia masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria. Vilevile kufungamanisha maudhui, dhamira ya sheria ndogo na lengo kuu la sheria mama ni njia iliyotumika ili kuipima kwa vigezo vya uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili; uchambuzi wa sheria ndogo na tarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Sehemu ya pili inabainisha uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge. Vilevile sehemu hii inafafanua uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge. Maelezo yake yanahusu msingi wa uchambuzi, vigezo vilivyotumika na hatua za uchambuzi. Kwa muhtasari, nitaeleza mambo makuu mawili katika sehemu ya uchambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge; naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu chimbuko la sheria ndogo zilizochambuliwa, vigezo vilivyotumika na hatua za uchambuzi wa sheria ndogo kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la sheria ndogo zilizochambuliwa; chimbuko la sheria ndogo zilizochambuliwa na kubainika kuwa na hoja ni sheria kumi na moja zilizotungwa na Bunge kwa wakati tofauti. Miongoni mwake ni hizi zifuatazo:-

(i) Sheria ya Udhibiti wa Nishati na Maji Sura ya 141, iliyolenga kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Masuala ya Nishati na Huduma za Maji pamoja na mambo mengine kuhusiana na hayo.

(ii) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, iliyotungwa kuweka masharti ya uanzishaji wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini kwa lengo la kusimamia sekta ya usafiri ardhini na mambo mengine kuhusiana na hayo.

(iii) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, iliyotungwa kwa lengo la kuweka masharti yanayohusu Serikali za Mitaa na mambo mengine kuhusu uendeshaji wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara.

(iv) Sheria ya Umeme Sura ya 131, iliyotungwa kwa lengo la kuwezesha usimamizi wa uzalishaji, usafirishaji, ubadilishaji, utawanyaji, ugawaji na matumizi ya nishati ya umeme na mambo mengine kuhusiana na hayo.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Bunge wakati wa kutunga sheria nilizozitaja ilizingatiwa wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo zinazoripotiwa katika taarifa hii. Naliomba Bunge lako tukufu litakapofanya uamuzi wa hoja hii likumbuke dhamira hiyo.

(b) Vigezo vilivyotumika katika uchambuzi lengo la kubainisha vigezo vilivyotumika katika uchambuzi wa sheria ndogo ni kuwezesha uhakika wa matokeo ya uchambuzi ambao umetokana na masharti ya kifungu cha 11(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge masharti hayo yamegusa vigezo vikuu vifuatavyo:-

(i) Iwapo sheria ndogo zimekidhi masharti ya Katiba;

(ii) Iwapo sheria ndogo zinaendana na masharti ya sheria mama; na

(iii) Iwapo sheria ndogo zimekidhi masharti ya sheria nyingine za nchi

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuzingatia vigezo hivyo Kamati ilidadisi mambo matano yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa masharti ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Kutokinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika;

(iii) Uzingatiaji wa misingi ya uandishi wa sheria;

(iv) Usahihi wa ufasaha na uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika; na

(v) Uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini ulivyotiliwa maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yametumika kupima sheria ndogo kwa vigezo nilivyovitaja kutokana na masharti ya Kanuni za Bunge.

Hatua za uchambuzi; wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo Kamati ilizingatia hatua zifuatazo:-

(i) Kufanya uchambuzi wa awali ili kubaini sheria zinazohitaji kufanyiwa uchambuzi wa kina na mambo yatakayopaswa kuzingatiwa wakati wa uchambuzi huo.

(ii) Kupokea maoni ya wadau ili kupata uhalisia wa mazingira ya utekelezaji wa sheria ndogo.

(iii) Kujumuisha maoni ya wadau na uchambuzi wa awali ili kupata matokeo ya awali ya uchambuzi;

(iv) Kujadiliana na mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika ili kupata maelezo kuhusu hoja zilizobainika kufika hatua zilizotangulia;

(v) Kupata uamuzi wa kamati unaotokana na mtazamo wa kamati baada ya majadiliano; na

(vi) Kuandaa hoja ya Kamati itakayoingia Bungeni baada ya uchambuzi wa sheria ndogo kwa lengo la kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nilizozitaja ziliiwezesha Kamati kubaini iwapo sheria ndogo zilizotungwa na mamlaka mbalimbali zimetokana na madaraka ya Bunge na kwamba madaraka hayo hayakutumika vibaya au tofauti kwa msingi huo taarifa hii italiwezesha Bunge kuamua inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge; naomba kueleza kwa muhtasari kuhusu msingi wa uchambuzi vigezo vilivyotumika na hatua ya uchambuzi wa hatua za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Msingi wa uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge unatokana na nia ya Bunge kuhakikisha madaraka yake ya kutunga sheria yanatumika inavyostahili. Ili kutimiza azma hiyo Kamati hii imepewa majukumu yanayolisaidia Bunge kwa muktadha huo taarifa ninayowasilisha inafafanua utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vilivyotumika; uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge uliongozwa na vigezo vifuatavyo:-

(i) Iwapo marekebisho yaliyoazimiwa yamezingatiwa katika rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo inayohusika;

(ii) Iwapo rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo imepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki;

(iii) Iwapo rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo iliyohakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefikia hatua ya kusubiria kutangazwa; na

(iv) Iwapo rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo inayohusika ambayo imehakikiwa na imetangazwa kwenye gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya yalizingatiwa katika tathmini ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge.

(c) Hatua ya uchambuzi; mchakato wa Kamati kuchambua taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge ilipitia hatua zifuatazo:-

(i) Kuainisha maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo kwa kuzingatia mamlaka zinazohusika;

(ii) Kufanya mapitio ya jumla ya taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zilizowasilishwa na mamlaka zinazohusika;

(iii) Kukutana na mamlaka zilizopaswa kutekeleza maazimio ili kupata ufafanuzi wa zaidi kuhusu yatokanayo na Maazimio ya Bunge; na

(iv) Kujadiliana na kupata mtazamo wa pamoja kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwa lengo la kuandaa hoja inayoingia Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua hizo ni wazi kuwa matokeo ya uchambuzi yanatosheleza majadiliano na uamuzi wa Bunge leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ni matokeo ya uchambuzi maoni na mependekezo; sehemu hii inaonesha matokeo ya uchambuzi maoni na mapendekezo ufafanuzi kuhusu matokeo hayo umebainishwa kwa kirefu katika taarifa iliyoko mezani. Aidha, maoni na mapendekezo ni miongoni mwa mambo makuu katika sehemu hii kwa ujumla sehemu hii inagusa mambo yafuatayo:-

(i) Matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo yaliyofafanuliwa katika Taarifa ya Kamati iliyowekwa mezani leo;

(ii) Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo;

(iii) Maoni yanayotokana na matokeo ya uchambuzi; na

(iv) Mapendekezo katika mfumo wa hoja uliowekewa masharti katika Kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufafanua kwa muhtasari kuhusu mambo haya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo; uchambuzi wa sheria ndogo kumi na nne umebainisha dosari thelathini na tatu. Naomba kufafanua dosari hizo kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi; maudhui ya sheria ndogo saba zilizochambuliwa yanakinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni *The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products Price Setting) Rules, 2022* - kanuni ya 8(3); sheria ndogo hii inaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa mtu atayetiwa hatiani kwa kosa la kutoitika wito wa *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu hiyo inakinzana na adhabu iliyowekwa na kifungu cha 18(5) cha sheria mama. Kifungu hicho kimeweka faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na tano au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa kosa la kutoitikia wito wa *EWURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza kimeweka sharti kwa sheria ndogo kutokinzana na masharti ya sheria mama. Katika mifano niliyoitoa sheria ndogo zimekiuka masharti ya sheria mama jambo linalosababisha sheria ndogo hizo kuwa batili kwa kiwango cha kukinzana kwake na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria; dosari ya sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria imebainika katika sheria ndogo nane. Mfano wa sheria ndogo hizo ni *The Tanzania Shipping Agencies (Performance Benchmarks) Regulations, 2022* - knuni ya 14(2) ya kanuni hizo inampa Waziri mamlaka ya kuteua watu watakaofanya tathmini ya utendaji wa *TASAC* bila kuonesha watakapotoka wateuliwa hao kwa maana ya kada, tasnia, aina au kategoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu wa kawaida unaonesha kwamba wanaoteuliwa katika nafasi mbalimbali hupatikana kutoka aina ya watu au wataalamu au kada au tasnia fulani. Aidha, kwa desturi ya uandishi wa sheria ndogo, inatarajiwa kwamba kanuni inayotungwa chini ya masharti ya sheria mama ya Bunge, inatoa ufafanuzi wa kutosha. kwa Kanuni hizo kutokufafanua watakapopatikana wateuliwa hao wa kufanya tathmini ya utendaji wa *TASAC,* haziendani na misingi ya uandishi wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuweka masharti yasiyoendana na uhalisia; sheria ndogo tano zimebainika kuwa na masharti yasiyoendana na uhalisia. Miongoni mwa sheria hizo ni Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, 2022 - kifungu cha 14(3) cha sheria ndogo hizo kinachukulia kosa la abiria kutupa takataka nje ya chombo cha usafiri, kimetendwa na mmiliki au dereva au kondakta wa chombo hicho. Kifungu hicho kinachofafanua kuwa mtendaji wa kosa hilo atalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi 50,000 chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uhalisia adhabu hulenga kumuadhibu mtenda kosa na kuwaogofya wengine wasitende kosa. Kwa namna ilivyoelezwa adhabu katika kifungu cha 14(3), mtenda kosa halisi ni msafiri aliyetupa taka nje ya chombo cha usafiri, lakini anayeadhibiwa ni mmiliki wa chombo au dereva au kondakta wa chombo kinachohusika. Hali hiyo, inaonesha lengo la adhabu halimgusi mlengwa wala haliwaogopeshi watu wengine kutenda kosa hilo kwa kuwa watakaoadhibiwa sio watendaji wa kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile sharti la adhabu lililowekwa katika kifungu cha 14(3) linasababisha usumbufu kwa wasiotenda kosa linalohusika. Kwa namna hiyo, sheria ndogo hiyo imeweka adhabu kwa masharti yasiyozingatia uhalisia katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya uandishi wa majedwali; sheria ndogo tatu zimebainika kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali kwa kukosa ukamilifu. Mfano wa sheria ndogo yenye dosari hizo ni *The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022* - Jedwali la Nne la Kanuni hizo limekosa ukamilifu ulioelekezwa na kanuni ya 19(3). Kanuni hiyo, inaweka masharti kwa mwenye leseni ya kuunganisha umeme kwamba baada ya kukamilisha ukaguzi wa miundombinu ya umeme atapaswa kumpatia mteja wake cheti ambacho mfano wake unaoneshwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari iliyobainika katika jedwali ni kukosekana kwa muonekano wa cheti kinachohusika. Kilichowekwa kwenye Jedwali ni angalizo juu ya kuambatisha maelezo yanayoonesha upungufu uliobainika wakati wa ukaguzi. Angalizo hilo si mfano wa cheti kilichokusudiwa na kanuni ya 19(3). Hali hiyo inasababisha kutokutimia kwa ufafanuzi uliolengwa kutolewa na jedwali hilo.

(b) Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo; matokeo ya uchambuzi yanabainisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2021. Ufafanuzi wa matokeo hayo umebainishwa katika kipengele cha 2.3 cha Sehemu ya Pili ya Taarifa iliyowekwa Mezani mapema leo hii. Kwa kifupi hatua hizo zipo katika makundi manne yafuatayo:-

(i) Utekelezaji uliofikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali;

(ii) Utekelezaji uliofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali;

(iii) Utekelezaji uliofikia hatua ya Rasimu ya Sheria Ndogo kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Uhakiki na Kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali; na

(iv) Utekelezaji ulio katika hatua ya awali za maandalizi ya rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, uainishaji wa hatua hizo umefafanuliwa zaidi katika jedwali la uchambuzi wa sheria na taarifa za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati; kutokana na uchambuzi wa sheria ndogo na Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge, Kamati imepata mtazamo unaojenga msingi wa mapendekezo. Kwa upande wa sheria ndogo dosari zilizobainika zisipofanyiwa marekebisho zitaathiri dhamira ya Bunge. Aidha, mamlaka zilizokasimiwa na Bunge jukumu la kutunga sheria ndogo zilizochambuliwa na kubainika kuwa na dosari zinapaswa kurekebisha dosari hizo kama ilivyoazimiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo na hoja; baada ya maelezo niliyoyatoa, sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie, matokeo ya uchambuzi na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Hoja hii inahusu maeneo muhimu ya utekelezaji wa sheria ndogo ambao kwa sehemu kubwa inagusa moja kwa moja maisha ya wananchi walio wengi. Kwa msingi huo naomba kutoa hoja katika maeneo matano kama ifuatavyo:-

Kwanza; kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo na sheria nyingine za nchi; kwa kuwa imebainika zipo sheria ndogo zilizobainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa sheria mama inayokusudiwa; na kwa kuwa sheria ndogo zinazokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, haziendani na masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria, hali inayosababisha kuwa batili kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya Kwanza, kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizotengeneza sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zirekebishe sheria hizo mara moja.

Pili; kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zimebainika kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kinyume na desturi ya uandishi wa sheria ndogo; na kwa kuwa kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi kunasababisha sheria ndogo kutoeleweka kwa urahisi na kutotabirika, hali inayoweza kuathiri utekelezaji wa sheria mama; kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya

kutengeneza sheria ndogo hizo zifanye marekebisho na kuzingatia misingi ya uandishi.

Tatu; kuweka masharti yasiyoenda na uhalisia; kwa kuwa zipo baadhi ya sheria ndogo zilizoweka masharti yasiyoendana na uhalisia; na kwa kuwa, masharti hayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa sheria na tija inayokusudiwa; kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizopewa madaraka ya kutengeneza sheria hizo zifanye marekebisho na kuzingatia uhalisia.

Nne, dosari katika uandishi wa majedwali; kwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali, ilihali kifungu cha 25(2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinatambua majedwali kuwa sehemu ya sheria, na kwa kuwa, dosari hizo zinaathiri ukamilifu na kutatiza utekelezaji sheria inayohusika; kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutengeneza sheria ndogo hizo zifanye marekebisho kuwezesha ufasaha na uandishi wa sheria inayohusika wa majedwali.

Tano; utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo; kwa kuwa Bunge linapotoa maazimio kuhusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo, linakusudia kuondoa madhara ya utekelezaji wa sheria hizo ndogo; na kwa kuwa, kutokutekelezwa kwa maazimio hayo ni kuendelea kuruhusu dosari hizo kuendelea kuwa sehemu ya sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge, kwa hiyo basi;

(a) Mamlaka ambazo hadi kufikia mwezi Machi, 2022 hazikuwa zimekamilisha hatua ya marekebisho ya sheria ndogo zilizoazimiwa na Bunge zihakikishe zimekamilisha mchakato huo ifikapo tarehe 1 Novemba, 2022; na

(b) Mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge na kubainika kuwa na dosari kama inavyoonekana katika jedwali ambalo ni sehemu ya taarifa hii zikamilishe mchakato huo wa marekebisho ya sheria ndogo ifikapo tarehe 1 Disemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika binafsi na Bunge hili tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge hili tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba nimshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu kwa kuendelea na uratibu wa kuwasilisha mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (sheria ndogo) kwa wakati. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na watendaji wa

Wizara kwa kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa sana iliyofanyika kwa weledi mkubwa wa uchambuzi. Juhudi na weledi wao umefanikisha taarifa hii. Kwa heshima hiyo naomba majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Majadiliano ya Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati. Vilevile nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Katibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndugu Mkuta Masoli akisaidiwa na Bi. Imelda Ntimba, Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA SITA NA MKUTANO WA SABA, PAMOJA NA UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KWENYE MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE WA BUNGE – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, naomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuona umuhimu wa kuiweka Taarifa hii kwenye orodha ya shughuli za leo za Bunge ukitumia madaraka yako chini ya Kifungu cha 11(3) cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Bila shaka umezingatia umuhimu wa kulipatia Bunge fursa adhimu inayoliwezesha kufuatilia na kudhibiti matumizi ya madaraka yake ya kutunga Sheria

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inakusudia kubainisha matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni na kuwekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Tano wa Bunge. Aidha, taarifa hii inalijulisha Bunge yaliyobainika katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la ufuatiliaji huo ni kulionesha Bunge lako tukufu jinsi madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa sheria za Bunge yalivyotekelezwa. Vilevile, Taarifa hii inalenga kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu sheria ndogo zilizowalishwa wakati wa Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

### 1.2 Mipaka na Masharti ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matarajio ya Bunge kutokana na maelezo niliyoyatoa, Taarifa hii imewekwa katika muundo unaoonesha sheria ndogo zilizochambuliwa, vigezo vya uchambuzi, matokeo ya uchambuzi na mapendekezo. Upangaji wa maudhui hayo umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa za Kamati zinazoingia Bungeni.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kurahisisha ufuatiliaji wa mtiririko wa taarifa hii, naomba kubainisha kuwa Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

a) Sehemu ya Kwanza inayohusu utangulizi ikionesha mipaka na msahrti ya uchambuzi, njia na mbinu zilizotumika na mambo mengine yanayoendana na sheria ndogo;

b) Sehemu ya Pili inayohusu uchambuzi ambayo inabainisha sheria ndogo zilizochambuliwa na chimbuko la sheria ndogo hizo, vigezo vya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo, msingi wa uchambuzi wa taarifa hizo, vigezo na hatua za uchambuzi;

c) Sehemu ya Tatu inabainisha matokeo ya uchambuzi, maoni ya Kamati na Mapendekezo ambayo yamewekwa kwa muundo wa hoja uliowekewa masharti katika Kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Bunge.

Aidha, Taarifa hii inafunga na sehemu ya nne ambayo inatoa shukurani na kuhitimisha.

**Mheshimiwa Spika**, mawanda ya taarifa hii yanazingatia lengo la kujenga msingi wa mjadala wa Bunge utakaowezesha uamuzi wenye manufaa kwa wananchi. Aidha, Taarifa hii inasomwa kwa pamoja na Majedwali mawili yaliyoambatishwa, ambayo ni sehemu ya Taarifa hii. Naomba taarifa yote pamoja na Majedwali yake iingie kwenye kumbukumbu za majadiliano ya Bunge (*Hansard*). Majedwali hayo ni, Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge ambalo ni **Kiambatisho Na. 1**, linaloonesha dosari katika jumla ya sheria ndogo kumi na nne na Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge pamoja na Kanuni za Uvuvi, 2009 ambalo ni **Kiambatisho Na. 2.** Jedwali hilo linaonesha Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika sheria ndogo ishirini na tatu (23).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na maelezo hayo**,** nilikumbushe Bunge hili kuwa ili taarifa hii ifikie lengo lililokusudiwa, kuna umuhimu wa kurejea maelezo kuhusu madaraka ya kutunga Sheria nchini, Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo na Kamati inavyosaidia udhibiti wa sheria ndogo. Baada ya ufafanuzi huo ambao ni msingi mkuu wa majadiliano ya Bunge lako tukufu, Taarifa hii inabainisha matokeo ya uchambuzi lengo likiwa ni kuonesha msingi wa maoni ya Kamati na kubainisha hoja na mapendekezo juu ya uamuzi unaotarajiwa kutoka katika Bunge lako tukufu.

### 1.3 Njia na Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** ili kuzingatia ipasavyo masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge yanayoitaka Taarifa hii kubainisha njia na mbinu zilizotumika katika utekelezaji wa jukumu la kuchambua sheria ndogo, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitumia njia na mbinu kuu zifuatazo:-

a) Kusoma matini (*text*) ya sheria ndogo na matini ya sheria mama;

b) Kuchunguza dhamira ya sheria mama ili kuipata nia ya Bunge kwa lengo la kujirishisha na namna nia hiyo ilivyozingatiwa katika sheria ndogo inayohusika;

c) Kutafakari dhamira ya sheria ndogo inayohusika ikilinganiishwa na nia ya Bunge kukasimu utungwaji wa sheria ndogo;

d) Kuzingatia masharti ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayotoa maana na muongozo wa uandishi, matumizi na tafsiri ya sheria zote zikiwemo sheria ndogo. Aidha, sheria hiyo inaelekeza mchakato wa sheria ndogo kuwekwa mezani Bungeni ili hatimaye upatikane uamuzi wa Bunge; na

e) Kufungamanisha maudhui, dhamira ya sheria ndogo na lengo kuu la sheria mama ili kuipima kwa vigezo vya uchambuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia mbinu hizo za uchambuzi wa sheria ndogo, Kamati iliweza kubaini dosari za aina tano kama ifuatavyo:-

a) kuwa kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutengeneza sheria ndogo au sheria nyingine ya nchi;

b) kutozingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria (*drafting principles*);

c) kutoendana na uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini; na

d) makosa ya uandishi katika Majedwali kwa mfano kutorejea Kanuni sahihi, kurejea Kanuni ambazo hazipo, kutorejea kabisa Kanuni na Maudhui ya Jedwali tofautiana na Vifungu vinavyoyaanzisha.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilikutana na kujadiliana mamlaka zilizotunga sheria ndogo zilizochambuliwa na Kamati kwa lengo la kupata ufafanuzi wa hoja zilizoibuliwa na Kamati. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa majadiliano na ushirikiano kutoka kwa mamlaka hizo yaliwezesha Kamati kufanya uchambuzi inavyostahili.

### 1.4 Mambo Mengine Yanayoendana na Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba sheria ndogo hutokana na sheria zilizotungwa na Bunge wakati likitekeleza madaraka yake ya kutunga sheria. Aidha, Bunge huwa na utaratibu wa udhibiti wa sheria ndogo kwa kuwa ni zao la sheria zilizotungwa na Bunge. Kwa minajili hiyo ni vema Kamati ikatoa ufafanuzi mfupi kuhusu dhana ya madaraka ya kutunga sheria na udhibiti wa kibunge wa sheria ndogo. Lengo ni kuonesha msingi wa uchambuzi wa sheria ndogo unaohitaji kuzingatiwa katika Taarifa hii.

#### *1.4.1 Madaraka ya Kutunga Sheria*

**Mheshimiwa Spika**, madaraka ya kutunga sheria zote nchini yamewekwa chini ya mamlaka ya Bunge. Ibara ya 4 na 64 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (Kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara), imelipa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya Muungano na yasiyo ya Muungano yahusuyo Tanzania bara. Aidha, Ibara ya 97 ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Bunge katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mamlaka hayo ya Bunge, Ibara ya 97 (5) ya Katiba inaliruhusu Bunge kukasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali. Utaratibu huo ni wa kawaida katika utungaji wa sheria. Miongoni mwa sababu za utaratibu huo ni umuhimu wa kuzingatia utaalamu mahsusi unaopatikana katika mamlaka mbalimbali za kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na msingi huo, utaratibu huu ni halali na unafaa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini unatumika kwa madhumuni maalumu, kuweka mipaka, ukomo au upeo kwa namna yenye udhibiti. Msimamo huu si wa Bunge la Tanzania pekee bali unakubalika na kutumika pia katika mabunge mengine duniani. Kwa kawaida Mabunge yanahitaji kuhakikisha kuwa madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika vizuri bila kuwa kero au kusababisha kero kwa wananchi. Kuwezesha hilo, Mabunge duniani hutumia utaratibu unaozingatia mambo yafuatayo:-

a) Madaraka ya kutengeneza sheria ndogo hukasimiwa kwa mamlaka yenye kuaminika na kukubalika kitaifa;

b) Wigo na mipaka ya sheria ndogo inayoweza kutungwa katika utekelezaji wa Sheria Mama (*Principal legislation*) huwekwa bayana;

c) Utekelezaji wa madaraka ya kutunga Sheria huelekezwa kuwahusisha wadau;

d) Mchakato wa utenganezaji wa sheria ndogo na matumizi yake hutakiwa kuwezesha sheria ndogo inayohusika ijulikane kwa umma; na

e) Kujulikana kwa mfumo, utaratibu na mamlaka inayowezesha marekebisho au zuio la kutumika kwa sheria ndogo iwapo kama itahitajika hivyo.

### *1.4.2 Udhibiti wa Kibunge wa Sheria Ndogo*

**Mheshimiwa Spika,** udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo (*Parliamentary Control Over Subsidiary Legislation*) ni utaratibu unaotumika katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola. Utaratibu huu unalenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha kikamilifu iwapo utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine umefanyika ilivyokusudiwa na Bunge lenyewe. Udhibiti huo, hufanyika kwa kulinganisha sheria ndogo na masharti ya sheria kuu (Sheria Mama) pamoja na misingi mingine iliyowekwa na Sheria zilizotungwa na Bunge. Tanzania ambayo pia hutumia utaratibu wa udhibiti wa sheria ndogo kwa kuweka kwanza kifungu kwenye sheria mama kinachobainisha madaraka yanayokasimiwa katika sheria ndogo. Kifungu

hicho kinaweza kuainisha sheria ndogo inayoweza kutengenezwa na mamlaka inayopewa madaraka ya kutengeneza sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, mchakato huo wa utungaji na udhibiti wa sheria ndogo nchini Tanzania umefafanuliwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, (*The Interpretation of Laws Act, Cap.* 1). Kifungu cha 37 (1) na 37 (2) cha Sheria hii kinataka sheria ndogo itangazwe kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika. Aidha, kifungu cha 38 (1) cha Sheria hiyo kimeweka sharti kwa sheria ndogo zinazotangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwasilishwa (kuwekwa mezani) Bungeni ndani ya siku sita za vikao vya Bunge vinavyofuata baada ya tarehe ya kuchapisha toleo la Gazeti lililotangaza sheria ndogo hizo. Masharti hayo yamewekewa utaratibu katika mchakato wa Kibunge kwa kufafanuliwa na Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 43 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka utaratibu wa sheria ndogo zilizotangazwa katika Gazeti la Serikali kuwasilishwa Bungeni. Baada ya sheria ndogo kuwekwa mezani, Kanuni ya 43 (8) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inataka sheria ndogo hizo zijadiliwe na Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo. Katika Utaratibu huo, Kifungu cha 11 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kinaelekeza kuwa, Kamati inapokamilisha kazi ya uchambuzi Mwenyekiti wa Kamati anapaswa kumjulisha Spika kwa maandishi.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo ya Kanuni za Bunge yamezingatiwa ipasavyo na kukuwezesha kutumia mamlaka uliyopewa chini Kifungu cha 11 (3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kuagiza Taarifa hii iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Leo. Katika hatua hii, niliombe Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili kwa kina Taarifa ninayoiwasilisha na hatimaye litoe uamuzi kwa maazimio yanayotokana na Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge, Mkutano wa Saba wa Bunge pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge. Majadiliano hayo yazingatie kuwa Kifungu cha 38 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kimebainisha uwezo wa Bunge kufanya marekebisho katika sheria ndogo au kuibadilisha sheria ndogo inayohusika.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ni nyenzo muhimu na ya msingi itakayoliwezesha Bunge lako tukufu kutekeleza wajibu wake wa kudhibiti sheria ndogo nchini. Ili kufanikisha wajibu huo wa Bunge, Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo inaweza kutumia njia ya kuchambua sheria zilizowekwa Mezani au kuchambua sheria ndogo zinazoendelea kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii pia inatoa matokeo ya Uchambuzi wa sheria ndogo zilizowekwa mezani wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge, Mkutano

wa Saba wa Bunge na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge katika sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Nne wa Bunge. Utaratibu huu wa kutumika kwa sheria ndogo kabla ya kuchambuliwa na kujadiliwa na Bunge unaruhususiwa katika mfumo wa udhibiti wa sheria ndogo usio wa moja kwa moja (*Indirect control*) ambao Tanzania unaoufuata na kuutumia.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sehemu inayofuata ya Taarifa hii italiwezesha Bunge kujadili inavyopaswa na hatimaye kufanya uamuzi ulio na tija na wenye manufaa kwa wananchi na maisha yao kwa ujumla. Nitumie fursa hii kuliomba Bunge lako tukufu liendelee na msisitizo wake wa kuona sheria ndogo haziwi chanzo cha kero katika shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na wananchi na wala haziweki vikwazo katika ustawi na maendeleo yao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli hizo kwa uhai na maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla, Bunge lina kila sababu ya kuwa na jicho kali katika sheria ndogo zinazotungwa na mamlaka mbalimbali. Lengo ni kuondoa uwezekano kero zinazoweza kusababishwa na sheria ndogo zinazohusika na hatimaye kuchochea maendeleo ya nchi, ustawi wa watu na taifa kwa ujumla.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA SITA NA MKUTANO WA SABA WA BUNGE PAMOJA NA TARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA TATU NA MKUTANO WA NNE WA BUNGE

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla wa Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inabainisha uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge. Katika ufafanuzi sehemu hii inabainisha chimbuko la sheria ndogo zilizochambuliwa, vigezo vilivyotumika katika uchambuzi na hatua za uchambuzi.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, sehemu hii inafafanua uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge. Maelezo yake yanahusu msingi wa uchambuzi, vigezo vilivyotumika na hatua za uchambuzi wa Taarifa hizo.

## 2.2 Uchambuzi wa Sheria Ndogo Zilizowasilishwa katika Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge

**Mheshimiwa Spika,** ili kuweka mtiririko rahisi wa shughuli ya uchambuzi wa Sheria Ndogo, naomba kutoa maelezo mafupi kwa mambo matatu muhimu. Mambo hayo ni chimbuko la sheria ndogo zilizochambuliwa, vigezo vya uchambuzi wa sheria ndogo hizo na hatua zilizotumika wakati wa uchambuzi. Maelezo hayo ni kama ifuatavyo:-

### *2.2.1 Chimbuko la Sheria Ndogo Zilizochambuliwa*

**Mheshimiwa Spika**, chimbuko la sheria ndogo zilizochambuliwa na kubainika kuwa na hoja ni sheria kumi na moja zilizotungwa na Bunge kwa wakati tofauti. Sheria hizo ni:-

a) Sheria ya Udhibiti wa Nishati na Maji Sura ya 141, iliyolenga kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Masuala ya Nishati na Huduma za Maji pamoja na mambo mengine kuhusiana na hayo;

b) Sheria ya Madini Sura ya 123, iliyotungwa kwa lengo la kuweka masharti ya kisheria kuhusu ugunduzi, uchimbaji, uchakataji wa madini, malipo ya mirabaha, ada na tozo nyingine pamoja na mambo mengine kuhusiana na hayo;

c) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 iliyotungwa kuweka masharti ya uanzishaji wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini ili kusimamia sekta ya usafiri ardhini pamoja na mambo mengine kuhusiana na hayo;

d) Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438, iliyotungwa kwa ajili ya kurahisisha usimamizi wa kodi na utekelezaji wa sheria za kodi unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na mambo mengine yanayoendana na hayo;

e) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288, iliyotungwa kwa ajili ya kuweka masharti ya kuanzisha Mamlaka za Miji pamoja na mambo mengine kuhusiana na hayo;

f) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, iliyotungwa kwa lengo la kuweka masharti yanayohusu Serikali za Mitaa na mambo mengine kuhusu uendeshaji wa Serikali za Mitaa Tanzania Bara;

g) Sheria ya Umeme Sura ya 131, iliyotungwa kwa lengo la kuwezesha usimamizi wa uzalishaji, usafirishaji, ubadilishaji, utawanyaji, ugawaji na matumizi ya nishati ya umeme na mambo mengine kuhusiana na hayo;

h) Sheria ya Uwakala ya Meli Tanzania Sura ya 415 iliyotungwa ili kuweka masharti ya uanzishwaji wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania na usimamizi wa mabaharia, bandari, huduma za meli, usalama na mambo mengine kuhusiana na hayo;

i) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura ya 290, iliyotungwa ili kuweka masharti ya vyanzo vya mapato na usimamizi wa fedha za Mamlaka za Mitaa na mambo mengine kuhusiana na mifumo ya fedha katika Mamlaka hizo;

j) Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218, iliyotungwa kwa lengo la kuweka masharti yanayolinda hakimiliki na hakishiriki katika kazi za uandishi, sanaa na ubunifu pamoja na mambo mengine kuhusu hakimiliki na hakishiriki; na

k) Sheria ya Petroli Sura ya 392 inayosimamia shughuli zinazohusu mambo ya Petroli za mkondo wa juu, mkondo wa kati na mkondo wa chini, uanzishaji wa PURA na mambo mengine yanayohusu masuala ya Petroli.

**Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Bunge wakati wa kutunga sheria nilizozitaja ilizingatiwa wakati wa uchambuzi wa sheria ndogo zinazoripotiwa katika Taarifa hii. Naliomba Bunge lako tukufu litakapofanya uamuzi wa hoja hii likumbuke dhamira yake.

### *2.2.2 Vigezo Vilivyotumika katika Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inabainisha vigezo vilivyotumika katika uchambuzi wa sheria ndogo zinazoripotiwa. Lengo ni kuliwezesha Bunge kujiridhisha na uhakika wa matokeo ya uchambuzi kwa kulinganisha na nia yake ya kufuatilia utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria.

**Mheshimiwa Spika,** vigezo vilivyotumika wakati wa uchambuzi vimetokana na masharti ya kifungu cha 11(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Masharti hayo yamegusa vigezo vikuu vitatu ambavyo ni:-

a) Iwapo sheria ndogo zimekidhi masharti ya Katiba;

b) Iwapo sheria ndogo zinaendana na masharti ya sheria mama; na

c) Iwapo sheria ndogo zimekidhi masharti ya sheria nyingine za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuzingatia vigezo hivyo, Kamati ilidadisi mambo matano yafuatayo:-

a) Uzingatiaji wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

b) Kutokinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika;

c) Uzingatiaji wa misingi ya uandishi wa sheria;

d) Usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya sheria ndogo inayohusika. Mfano, kurejea kanuni kwa sahihi, kutorejea Kanuni ambazo hazipo, kurejea Kanuni inayohusika pamoja na maudhui ya Jedwali kuendana na vifungu vinavyoyaanzisha Jedwali; na

e) Uhalisia wa mambo ikiwemo urahisi wa utekelezaji wake, hali ya uchumi wa walengwa na viwango vya adhabu na faini ulivyotiliwa maanani.

**Mheshimiwa Spika,** mambo hayo matano yameisaidia Kamati kubaini dosari za kutozingatia masharti ya Katiba, kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Kwa msingi huo, mapendekezo kuhusu dosari zilizobainika yanahitaji kuzingatiwa wakati wa kufanya uamuzi.

### *2.2.3 Hatua za Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika,** hatua za uchambuzi wa jambo lolote zina mchango mkubwa katika matokeo ya kazi hiyo. Kwa kuthamini mchango huo, naomba kulijulisha Bunge hatua za uchambuzi wa sheria ndogo kama ifuatavyo:-

a) Kufanya uchambuzi wa awali ili kubaini sheria zinazohitaji kufanyiwa uchambuzi wa kina na mambo yatakayopaswa kuzingatiwa wakati wa uchambuzi huo;

b) Kupokea maoni ya wadau ili kupata uhalisia wa mazingira ya utekelezaji sheria ndogo;

c) Kujumuisha maoni ya wadau na uchambuzi wa awali ili kupata matokeo ya awali ya uchambuzi;

d) Kujadiliana na Mamlaka iliyotunga sheria ndogo inayohusika ili kupata maelezo kuhusu hoja zilizobainika katika hatua zilizotangulia;

e) Kupata uamuzi wa Kamati unaotokana na mtazamo wa Kamati baada ya majadiliano; na

f) Kuandaa hoja ya Kamati itakayoingia Bungeni baada ya uchambuzi wa sheria ndogo kwa lengo la kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi.

**Mheshimiwa Spika,** hatua za uchambuzi wa sheria ndogo nilizozitaja, ziliiwezesha Kamati kubaini iwapo sheria ndogo zilizotungwa na mamlaka

mbalimbali zimetokana na madaraka ya Bunge na kwamba madaraka hayo hayakutumika tofauti. Kwa msingi huo, Taarifa hii italiwezesha Bunge kuamua inavyostahili.

## 2.3 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Kuhusu Sheria Ndogo Zilizowasilishwa Katika Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge unahusu sheria ndogo ishirini na tatu (23) zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge. Sheria ndogo hizo zilikuwa na hoja sitini na saba (67) ambazo zilitolewa maazimio na Bunge.

### *2.3.1 Msingi wa Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge unatokana na nia ya Bunge kuhakikisha madaraka yake ya kutunga Sheria yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Kwa mudhumuni hayo, Bunge halipaswi kuishia ubainishaji wa dosari na maazimio kuhusu dosari hizo, bali pia kujiridhisha na marekebisho ya dosari zilizobainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Utaratibu wa Bunge kufanya kazi kwa kutumia Kamati za Bunge, ndio unaoiweka Kamati ya Sheria Ndogo katika nafasi ya kuliwezesha Bunge kufuatilia sheria ndogo na urekebishaji wa dosari zote zilizobainika. Kwa msingi huo, uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Tatu tarehe 9 Aprili, 2021 na Mkutano wa Nne tarehe 7 Septemba, 2021ulifanyika. Uchambuzi huo ulilenga kubaini hatua zilizofikiwa katika kufanya marekebisho kwa lengo la kundoa dosari zilizobainika.

### *2.3.2 Vigezo Vilivyotumika*

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, ulizingatia hatua iliyoripotiwa kuwa imefikiwa. Uzingatiaji huo, ulifanyika kwa kuongozwa na udadisi wa mambo yafuatayo:-

a) Iwapo marekebisho yaliyoazimiwa yamezingatiwa katika Rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo inayohusika;

b) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo imepelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki;

c) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo iliyohakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefikia hatua ya kusubiri kutangazwa; na

d) Iwapo Rasimu ya marekebisho ya sheria ndogo inayohusika ambayo imehakikiwa imetangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, vigezo hivyo, viliisaidia Kamati kutathmini hali ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Matokeo ya tathmini hiyo yanaliwezesha Bunge kuamua hatua inayofuata.

#### *2.3.3 Hatua za Uchambuzi*

**Mheshimiwa Spika,** Hatua za uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji ni jambo linalosaidia katika ubora, uhalisia na uhakika wa matokeo ya uchambuzi. Kwasbabu hiyo, naomba kulijulisha Bunge hili hatua zilizotumika ambazo ni:-

a) Kuainisha Maazimio ya Bunge kuhusu sharia ndogo kwa kuzingatia mamlaka zinazohusika;

b) Kufanya mapitio ya jumla ya Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zilizowasilishwa na mamlaka zinazohusika lengo ni kubaini iwapo dosari zote zilizoazimiwa zimezingatiwa na hatua iliyofikiwa katika marekebisho;

c) Kukutana na mamlaka zilizopaswa kutekeleza maazimio. Lengo kupata ufafanuzi zaidi na tahmini ya kina kuhusu yatokanayo na maazimio ya Bunge; na

d) Kujadiliana na kufikia uamuzi unaotokana na mtazamo wa Kamati kuhusu utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Lengo ni kuandaa hoja kwa ajili ya kuwezesha uamuzi wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hatua hizo Taarifa hii imebeba matokeo ambayo ni msingi wa mapendekezo ya maazimio ya Bunge katika hoja hii ya Kamati.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI, MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Ufafanuzi wa Jumla wa Sehemu ya Tatu

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya tatu ya Taarifa hii inonesha matokeo ya uchambuzi, maoni na mapendekezo. Ufafanuzi wake unahusu matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo na uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Aidha, maoni kutokana na matokeo hayo yanabainishwa kwa kuzingatia  Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, dhamira ya Bunge kutunga sheria mama au sheria nyingine  za nchi pamoja na mazingira halisi  ya utekelezaji  wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge, maoni ya Kamati yamezingatia madhara ya dosari zilizokuwa zimebainishwa na nafasi ya Bunge katika mfumo wa sheria za nchi. Aidha wajibu wa Bunge kuangalia utekelezaji wa madaraka ya kutunga sheria ndogo umekuwa msingi wa maoni yanayobainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** maoni ya Kamati katika sehemu hii yanaonesha mawazo ya Kamati kuhusu yatokanayo na uchambuzi. Mawazo hayo yanaweka msingi wa mapendekezo ya Kamati kwa Bunge lako tukufu. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia vizuri Taarifa hii na kuamua juu ya mapendekezo ya Kamati, naomba kutaja vipengele vitano vya sehemu ya tatu ya Taarifa hii kama ifuatavyo:-

a) Kipengele cha kwanza kinatoa ufafanuzi wa jumla kama nilivyoanza kueleza;

b) Kipengele cha pili kinabainisha matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo;

c) Kipengele cha tatu kinabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji;

d) Kipengele cha nne kinabainisha maoni kutokana na uchambuzi; na

e) Kipengele cha tano kinaonesha mapendekezo katika mfumo wa hoja uliowekewa masharti katika Kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mtiririko huo, bila shaka Bunge litaijadili Taarifa hii na hatimaye kuamua. Uamuzi wa Bunge kutokana na Taarifa hii utakuwa umezingatia madaraka ya Bunge kutunga sheria na wajibu wake wa kufuatilia utekelezaji wa madaraka yake yaliyokasimiwa kwa mamlaka za kiutendaji.

### 3.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa sheria ndogo kumi na nne uliiwezesha Kamati kubaini dosari thelatini na tatu. Matokeo hayo yanatokana na uzingatiaji wa vigezo vinne nilivyovijata awali. Kwa msingi huo, Kamati inabainisha dosari katika mchanganuo ufuatao:-

a) Dosari ya kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutungwa kwa sheria ndogo inayohusika na sheria nyingine za nchi imebainika katika sheria ndogo saba;

b) Dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria imebainika katika sheria ndogo nane;

c) Dosari ya kuweka masharti yasiyo na uhalisia imebainika katika sheria ndogo sita; na

d) Dosari ya uandishi wa majedwali imebainika katika sheria ndogo tatu.

**Mheshimiwa Spika,** mchanganuo huo unazijumuisha baadhi ya sheria ndogo katika aina zaidi ya moja ya dosari. Jambo hilo linasababisha idadi ya sheria ndogo kutofautiana kitakwimu na jumla ya sheria ndogo katika mchanganuo huo. Kwa ufafanuzi zaidi wa takwimu na dosari, Taarifa hii imeambatisha Jedwali la Uchambuzi ili kuwezesha rejea wakati wa mjadala na uamuzi. Kwa madhumuni ya uwasilishaji, naomba kufafanua kwa muhtasari dosari zilizobainishwa kama ifuatavyo:-

***3.2.1 Kukinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine na Nchi***

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa, maudhui ya sheria ndogo saba zilizochambuliwa yanakinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Mfano wa sheria ndogo hizo ni ***The Electricity (Electrical Installation Services) Rules, 2022 (TS. Na.113/4, Machi 2022)*** *ambazo zimetungwa* chini Sheria ya ***The Electricity Act*** **(Sura 131)**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri ya kawaida, leseni ni idhini maalumu kutoka kwenye mamlaka inayohusika ili kufanya shughuli au kazi mahususi, hivyo shughuli au kazi yoyote nje ya idhini hiyo au bila ya idhini hiyo inahesabika kufanyika bila leseni.

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 4** imeweka wajibu wa kuomba na kupata leseni kwa ajili ya kufanya shughuli ya kuunganisha umeme. Kwa msingi huo, kufanya shughuli ya kuunganisha umeme pasipokuwa na leseni kosa linalostahili adhabu kwa mujibu wa kanuni hizi. Hata hivyo, Kanuni zimeweka adhabu mbili tofauti kwa makosa ya kuunganisha umeme pasipo na leseni. Adhabu ya kwanza imetajwa katika **Kanuni ya 4(2)** ni faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo cha muda usiozidi miaka mitano au vyote. Adhabu ya pili imewekwa na **Kanuni ya 21(1)** ambayo ni faini ya shilingi laki mbili kwa mwenye leseni anayefanya kazi ya kuunganisha umeme iliyo nje ya wigo wa leseni yake.

**Mheshimiwa Spika**, adhabu zilizowekwa na **Kanuni ya 4(2)** na **21(1)** zinakinzana na adhabu iliyowekwa na **Kifungu cha 8(5)** cha sheria mama. Kifungu hicho kinatamka adhabu ya shilingi zisizozidi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa kosa la kuunganisha umeme bila leseni.

**Mheshimiwa Spika,** mfano mwingine wa sheria ndogo yenye dosari ya kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi ni Kanuni za ***The Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Petroleum Products***

***Price Setting) Rules (TS. Na. 57/28, Januari 2022).*** Kanuni hizo zimetungwa chini Sheria ya ***The Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act (Sura. 414).*** **Kanuni ya 8 (3)** ya sheria ndogo hii inaweka adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja kwa mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa la kutoitika wito uliotolewa na EWURA.

**Mheshimiwa Spika,** adhabu inayowekwa na **Kanuni ya 8(3)** inakinzana na adhabu iliyowekwa na **Kifungu cha 18(5)** cha sheria mama. Kifungu hicho kimeweka faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na tano au adhabu zote pamoja kwa kosa la kutoitikia wito uliotolewa na EWURA.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1 kimeweka sharti kwa sheria ndogo kutokinzana na masharti ya sheria mama. Katika mifano niliyoitoa sheria ndogo zimekiuka masharti ya sheria mama jambo linalosababisha sheria ndogo hizo kuwa batili kwa kiwango cha kukinzana kwake na sheria mama.

### *3.2.2 Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria*

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya sheria ndogo kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria imejitokeza katika sheria ndogo nane. Mfano wa sheria ndogo hizo ni ***The Tanzania Shipping Agencies (Performance Benchmarks) Regulations, 2022*** **(TS. Na. 116/4 Machi, 2022)** zilizotungwa chini ya **Sheria ya *The Tanzania Shipping Agencies Act*, Sura ya 415. Kanuni ya 14(2)** inampa Waziri mamlaka ya kuteua watu watakaofanya tathmini ya utendaji wa TASAC bila kuonesha watakapotoka wateuliwa hao (kada, tasnia, aina au kategoria).

**Mheshimiwa Spika**, uzoefu wa kawaida unaonesha kwamba, wanaoteuliwa katika nafasi mbalimbali hupatikana kutoka aina ya watu au wataalamu au kada au tasnia fulani. Aidha, kwa desturi ya uandishi wa sheria ndogo, inatarajiwa kwamba, kanuni inayotungwa chini ya msaharti ya Sheria ya Bunge, itatoa ufafanuzi wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa Kanuni hizo kutokufafanua watakapotoka wateuliwa wa kufanya tathmini ya utendaji wa TASAC, haziendani na misingi ya uandishi wa sheria ndogo. Hali hiyo inafifisha azma ya sheria ndogo kuwezesha utekelezaji wa masharti ya Sheria mama iliyokasimu madaraka ya kufafanua masharti ya Sheria ya Bunge.

### *3.2.3 Kuweka Masharti Yasiyoendana na Uhalisia*

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya sheria ndogo kuweka masharti yasioendana na uhalisia imebainika katika sheria ndogo tano. Miongoni mwa sheria hizo ni **Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya**

**Itigi, 2022 (TS. Na. 128/4 Machi, 2022).** Sheria ndogo hizo zilizotungwa chini ya **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287. Kifungu cha 14(3)** cha sheria ndogo hizo kinachukulia kosa la abiria kutupa takataka nje ya chombo cha usafiri, limetendwa na mmiliki au dereva au kondakta wa chombo hicho. Kifungu hicho kinafafanua kuwa, mtendaji wa kosa hilo atalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uhalisia adhabu hulenga kumuadhibu mtenda kosa na kuwaogofya wengine wasitende kosa. Kwa namna ilivyoelezwa adhabu katika kifungu cha 14(3), mtenda kosa halisi ni msafiri aliyetupa taka nje ya chombo cha usafiri, lakini anayeadhibiwa ni mmiliki au dereva au kondakta wa chombo kinachohusika. Hali hiyo, inaonesha lengo la adhabu halimgusi mlengwa wala haliogofi watu wengine kutenda kosa kwa kuwa watakaoadhibiwa sio watendaji wa kosa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile sharti la adhabu lililowekwa katika kifungu cha 14(3) linasababisha usumbufu kwa wasiotenda kosa linalohusika. Kwa namna hiyo, sheria ndogo hiyo imeweka adhabu kwa masharti yasiyozingatia uhalisia katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi.

**Mheshimiwa Spika,** mfano mwingine wa sheria ndogo iliyobainika kuwa na vifungu visivyo na uhalisia ni ***The Tax Administration (Tax Ombudsman Service Complaint Procedure) Regulations*, 2022 (TS. Na. 106/25 Februari, 2022).** Sheria ndogo hizo zimetungwa chini ya ***The Tax Administration Act, Sura 438***.

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 6** inakataza mtu aliyeajiriwa kama mchunguzi maalumu wa masuala ya kikodi (*ombudsman*) kuwa katika shughuli nyingine ambayo ina masharti ya malipo ya mshahara. Masharti hayo hayaoneshi mantiki ya zuio hilo au mgogano unaoweza kusababishwa na mchunguzi maalumu kuwa katika ajira nyingine inayomuingizia kipato.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali hiyo, masharti hayo yana muonekano wa kumzuia muhusika kuwa katika ajira binafsi ambazo hazihusiani majukumu ambayo yanasimamiwa chini ya Kanuni hizi. Muonekano huo unatokana na kutokufafanuliwa kwa kazi zinazokatazwa kwa mchunguzi maalumu. Hali hiyo ni tofauti na uhalisia uliolengwa na Bunge katika **Kifungu cha 28G** cha sheria mama.

### *3.2.4 Dosari ya Uandishi wa Majedwali*

**Mheshimiwa Spika,** sheria ndogo tatu zimebainka kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali. Dosari hizo, zinatokana na majedwali kukosa ukamilifu wa ufafanuzi uliotarajiwa au dosari ya rejea ya kifungu kinachoyaanzisha majedwali hayo. Mfano wa sheria ndogo yenye dosari hizo ni ***The Electricity***

***(Electrical Installation Services) Rules, 2022* (TS. Na.113/4 Machi, 2022).** Sheria ndogo hiyo ilitungwa chini ya **Sheria ya *The Electricity Act* Sura ya 131.**

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Nne la Kanuni hizo limekosa ukamilifu ulioelekezwa na kanuni ya 19(3). Kanuni hiyo, inaweka masharti kwa mwenye leseni ya kuunganisha umeme kwamba, baada ya kukamilisha ukaguzi wa miundombinu ya umeme atapaswa kumpatia mteja wake cheti ambacho mfano wake unaoneshwa kwenye Jedwali la Nne la Kanuni.

**Mheshimiwa Spika,** dosari iliyobainika katika Jedwali ni kukosekana kwa muonekano wa cheti kinachohusika. Kilichowekwa kwenye Jedwali ni angalizo juu ya kuambatisha maelezo yanayoonesha upungufu uliobainika wakati wa ukaguzi. Angalizo hilo limewekwa kwa maneno yafuatayo:-
**Nanukuu** * *attach details of discrepancies observed** **Mwisho wa Kunukuu**.
Maneno hayo si mfano wa cheti uliokusudiwa na Kanuni ya 19(3).

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa pili wa sheria ndogo hizo ni Kanuni za ***The Copyright and Neighbouring Rights (Licensing and Rights to Benefit from Re-Sale), Regulations 2022* (TS. Na. 137/18 Machi, 2022).** Kanuni hizo zimetungwa chini ya **Sheria ya *The Copyright and Neighbouring Rights Act*, Sura 218.** **Jedwali la Nne** la Kanuni hizi linaonesha kuwa limetokana na Kanuni ya 29 linahusu "***distribution rules for public performance and broadcasting***". Imebainika kuwa, maudhui ya Kanuni ya 29 inayorejewa kuanzisha **Jedwali la Nne** hayahusiani **Jedwali** hilo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida uandishi wa Majedwali katika sheria unalenga kutoa ufafanuzi wa ziada wa maudhui yaliyo katika vifungu. Kwa msingi huo, kutokuandika majedwali kwa ufasaha kunasababisha mkanganyiko katika sheria. Mkanganyiko huo unaweza kuathiri malengo yaliyokusudiwa.

### 3.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanabainisha hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yalitolewa mnamo tarehe 10 Novemba, 2021. Hatua hizo zilizoripotiwa kwa kipindi cha utekelezaji hadi tarehe 31 Machi, 2022. Kipindi hicho ni takribani miezi minne tangu kupitishwa kwa maazimio ya Bunge, muda ambao ulitosha kwa kila mamlaka inayohusika kurekebisha dosari zilizobainika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na urefu wa kipindi cha utekelezaji wa maazimio ya Bunge nilioutaja, si dosari zote katika sheria ndogo ishirini na tatu zilizoazimiwa na Bunge zimeweza kurekebishwa ndani ya kipindi hicho. Kwa madhumuni ya kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake,

naomba kuainisha utekelezaji wa maazimio yanayohusika katika makundi yafuatayo:-

a) Utekelezaji wa Maazimio uliofikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Sheria Ndogo moja imefikia hatua hiyo.

b) Utekelezaji wa Maazimio uliofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo iliyohakikiwa na kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali. Sheria ndogo tatu zimefikia hatua hiyo;

c) Utekelezaji wa Maazimio uliofikia hatua ya Rasimu ya Sheria Ndogo kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Uhakiki na Kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Sheria Ndogo hizo ni nne; na

d) Utekelezaji wa Maazimio ulio katika hatua za awali za Maandalizi ya Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Sheria ndogo hizo ni kumi na tano.

**Mheshimiwa Spika**, uainishaji wa hatua hizo umefafanuliwa zaidi katika Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ambalo ni sehemu ya Taarifa hii. Aidha, ubainishaji wa Wizara zinazohusika utaliwezesha Bunge kuona hatua iliyofikiwa na kupata maelezo yanayohitajika. Kwa msingi huo naomba pia kuzitaja Wizara nane zinazohusika na Sheria Ndogo zilizoguswa na Maazimio ya Bunge ya tarehe 10 Novemba, 2021. Wizara hizo ni:-

a) Ofisi ya Rais TAMISEMI;
b) Wizara ya Afya;
c) Wizara ya Nishati;
d) Wizara ya Mifugo na Uvuvi;
e) Wizara ya Maliasili na Utalii;
f) Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
g) Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; na
h) Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hizo ndizo zenye dhamana ya Sheria mama zilizoruhusu utungwaji wa sheria ndogo zinazohusika na maazimio ya Bunge yaliyofuatiliwa. Sababu ya kuzitaja ni kuwezesha Bunge kupata taarifa ya utekelezaji kwa muktadha halisi wa wahusika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya uwasilishaji naomba kufafanua hatua nne zilizobainika kufikiwa kama ifuatavyo:-

### *3.3.1 Utekelezaji wa Maazimio Uliofikia Hatua ya Marekebisho Kutangazwa Katika Gazeti la Serikali.*

**Mheshimiwa Spika,** sheria ndogo moja imefanyiwa marekebisho ya dosari zilizobainika na kufikia hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Sheria

ndogo hiyo ni ***The Tanzania Medicines and Medical Devices (Good Storage and Distribution Practices) Regulations, 2021.***

**Mheshimiwa Spika,** mamlaka inayohusika na sheria ndogo hiyo, imechukua hatua madhubiti kutekeleza maazimio ya Bunge, pia kuondoa dosari ambazo zingeliweza kusababisha madhara iwapo ingeliendelea kutumika ikiwa na dosari hizo.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa dosari hizo ni **Kanuni ya 10**. Kanuni hiyo, iliweka sharti la mpokeaji wa bidhaa tiba kujiridhisha na tarehe za mwisho wa kutumika kwa bidhaa pasipo ulazima wa kujiridhisha na tarehe ya kutengenezwa kwake. Dosari hiyo ingeliweza kusababisha madhara yanayo hatarisha afya na maisha ya watumiaji wa bidhaa tiba.

***3.3.2 Utekelezaji wa Maazimio Uliofikia Hatua ya Marekebisho Kusubiri Namba ya Tangazo la Serikali***

**Mheshimiwa Spika,** sheria ndogo tatu zilizokuwa na dosari zimekamilisha hatua ya kuhakikiwa na zinasubiri namba ya Tangazo la Serikali. Sheria ndogo hizo ni:-

a) Kanuni za Uvuvi;

b) *The Civil Aviation (Training Centre) and Management and Operations, Rules 2021*; na

c) *The Electronic and Postal Communications (Tele-Traffic) Regulations 2021*.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua iliyokuwa imefikiwa na Wizara zinazohusika kutengeneza sheria ndogo zinazohusika na sheria ndogo hizo, inafanikisha dhamira ya Bunge kuondoa dosari. Hatua hiyo, ni muelekeo mzuri wa kuondoa changamoto inayoweza kusababishwa na sheria ndogo katika hali halisi ya utekelezaji.

***3.3.3 Utekelezaji wa Maazimio Uliofikia Hatua ya Rasimu Kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Ajili ya Uhakiki***

**Mheshimiwa Spika,** sheria ndogo nne zimebainika kuwasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya hatua ya kufanyiwa uhakiki. Sheria ndogo hizo ni:-

a) *The Environmental Management (Registration and Practice of Environmental Experts) Regulations, 2021;*

b) *The Environmental Management (Fees and Charges) Regulations, 2021;*

c) *The Environmental Management (Control and Management of Electrical and Electronic Equipment Waste) Regulations, 2021;* na

d) *The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2021*.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hiyo inaonesha dhamira njema ya kufanyia kazi maazimio ya Bunge. Pamoja na hivyo mchakato huo umechukua muda mrefu. Hali hiyo inaashiria kwamba, sheria ndogo hizo zenye dosari ziliendelea kutumiak na kuwa na athari mbalimbali.

***3.3.4 Utekelezaji wa Maazimio katika Hatua za Awali za Maandalizi ya Rasimu ya Marekebisho***

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umebainisha sheria ndogo kumi na tano zimeanza kufanyiwa marekebisho kwa hatua ya maandalizi ya Rasimu ya Marekebisho. Sheria ndogo hizo ni:-

a) *The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Registration and Movement of Animal Feed Resources and Products), 2021;*

b) *The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Import and Export of Animal Feed Resources) Regulations, 2021;*

c) *The Grazing – Land and Animal Feed Resources (Packaging, Branding, Labeling and Sealing) Regulations, 2021;*

d) *The Tanzania Meteorological Authority (Weather and Climate Forecasting Activities) Regulations, 2021;*

e) *The Tanzania Meteorological Authority (Meteorological Stations) Regulations, 2021;*

f) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli, 2021;

g) Sheria Ndogo ya Udhibiti wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 2021;

h) Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, 2021;

i) Sheria Ndogo ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, 2021;

j) Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, 2021;

k) *The Tanzania Communications Regulatory Authority (Bundle Tariffs, Promotions and Special Offers) Rules,2021;*

l) *The Wildlife Conservation (Resident Hunting) Regulations 2021;*

m) *The Wildlife Conservation (Wildlife and Forest Conservation Service) Regulations, 2021;*

n) *The Forest (Production, Transport and Selling of briquettes) Regulations, 2021;* na

o) *The Petroleum (Condensate Operations) Rules, 2021*.

**Mheshimiwa Spika**, hatua ya mamlaka zinazohusika na sheria ndogo hizo kuanza utekelezaji ilionesha matumaini kuwa, dosari zilizopo zingerekebishwa. Hata hivyo, hadi kipindi ambacho Kamati ilikuwa ikipokea taarifa za utekelezaji wa maazimio, ilikuwa imechukua takriban miezi minne kwa mamlaka zinazohusika kuwa kwenye hatua ya rasimu ya marekebisho tangu kutolewa kwa maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hiyo imechukua muda mrefu bila kuzingatia azma ya Bunge. Hali hiyo imesababisha wanaoguswa na sheria ndogo hizo, kuendelea kuathirika tofauti na dhamira ya Bunge yenye mamlaka ya asili ya kutunga sheria.

### 3.4 Maoni Kutokana na Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi yamebainisha mambo niliyoyataja awali kuhusu sheria ndogo zilizochambuliwa na Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Mambo hayo yaliyobainika, yameiwezesha Kamati kuwa na mtazamo unaojenga msingi wa maoni kama ifuatavyo:-

#### *3.4.1 Maoni Kutokana na Uchambuzi wa Sheria Ndogo*

**Mheshimiwa Spika**, dosari ya sheria ndogo kukinzana na sheria mama na sheria nyingine za nchi, kutozingatia misingi ya uandishi, kuweka masharti yasiyo na uhalisia na dosari ya uandishi wa majedwali zinaathiri tija ya sheria mama kuruhusu utungwaji wa sheria ndogo. Sheria ndogo hizo, zilitungwa ili kutoa ufafanuzi wa sheria mama kwa kuzingatia mazingira halisi ya

utekelezaji. Aidha, uandishi wa sheria hizo ulitazamiwa kurahisisha usomaji wa sheria mama kwa pamoja na ufafanuzi wa sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, dosari hizo zinazuia utekelezaji wa sheria mama kutokana na kutofafanuliwa ipasavyo au kutoendana na dhamira ya sheria mama na sheria nyingine za nchi. Kwa msingi huo Kamati ina maoni kwamba, Bunge lisipoamua kuhusu dosari hizo dhamira yake kutunga sheria na kuruhusu mamlaka zinazohusika kufafanua haitatimia.

### *3.4.2 Maoni Kutokana na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio*

**Mheshimiwa Spika**, maazimio ya Bunge yaliyotolewa tarehe 10 Novemba, 2021yalitokana na madaraka yake ya kutunga sheria. Katika desturi ya uendeshaji wa nchi kwa kutumia sheria, Bunge lilikasimu madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka zinazohusika na sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari. Kwa sababu hiyo, Bunge liliona haja ya marekebisho ya sheria ndogo hizo na kuazimia zirekebishwe.

**Mheshimiwa Spika,** mamlaka zinazohusika hazikuwa na hiari ya kurekebisha dosari zilizobainika, isipokuwa kufanya marekebisho kama ilivyoazimiwa. Zaidi ya hayo, dosari zilizobainika zilikuwa ni mazalia ya kero kwa wananchi na mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni kwamba, mamlaka zinazochelewa kufanya marekebisho yaliyoelekezwa na Bunge zinasababisha kuendelea kwa kero kwa wananchi, mkanganyiko katika utekelezaji wa sheria na kuathiri azma ya Bunge kutunga sheria mama. Hivyo basi, Bunge lisisitiza marekebisho hayo madaraka yake hayatakuwa yametumika ipasavyo.

## 3.5 Mapendekezo na Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo niliyoyatoa, sasa naliomba Bunge lako tukufu lizingatie ufafanuzi nilioutoa, matokeo ya uchambuzi na maoni ya Kamati ili lijadili na kutoa uamuzi wa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Hoja hii inahusu eneo muhimu la utekelezaji wa sheria ndogo ambalo kwa sehemu kubwa linagusa moja kwa moja maisha ya wananchi walio wengi. Kwa msingi huo naomba kutoa hoja katika maeneo matano kama ifuatavyo:-

### *3.5.1 Kukinzana na Masharti ya Sheria Inayotoa Mamlaka ya Kutungwa kwa Sheria Ndogo na Sheria Nyingine za Nchi*

**KWA KUWA,** imebainika zipo sheria ndogo zilizobainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria mama inayohusika,

**NA KWA KUWA,** sheria ndogo zinazokinzana na sheria mama au sheria nyingine za nchi, haziendani na masharti ya sheria ya tafsiri ya sheria, hali inayoisababisha kuwa batili kwa mujibu wa Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria Sura ya 1,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotengeneza sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zirekebishe sheria ndogo hizo.

### *3.5.2 Kutozingatia Misingi ya Uandishi wa Sheria*

**KWA KUWA,** baadhi ya sheria ndogo zimebainika kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria kinyume na desturi ya uandishi wa sheria ndogo,

**NA KWA KUWA,** kutozingatiwa kwa misingi ya uandishi kunasababisha sheria kutoeleweka kwa urahisi na kutotabirika, hali inayoweza kuathiri utekelezaji wa sheria mama,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutengeneza sheria ndogo hizo zifanye marekebisho na kuzingatia misingi ya uandishi.

### *3.5.3 Kuweka Masharti Yasiyoenda na Uhalisia*

**KWA KUWA,** zipo baadhi ya sheria ndogo zilizoweka masharti yasiyoendana na uhalisia,

**NA KWA KUWA**, masharti hayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa sheria na tija iliyokusudiwa,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizopewa madaraka ya kutengeneza sheria hizo zifanye marekebisho na kuzingatia uhalisia.

### *3.5.4 Dosari ya Uandishi wa Majedwali*

**KWA KUWA**, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya uandishi wa majedwali, ilihali Kifungu cha 25 (2) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinatambua majedwali kuwa sehemu ya Sheria,

**NA KWA KUWA,** dosari hizo zinaathiri ukamilifu na kutatiza utekelezaji sheria inayohusika,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizokabidhiwa madaraka ya kutengeneza sheria ndogo hizo zifanye marekebisho kuwezesha ufasaha wa uandishi wa majedwali.

### *3.5.5 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Kuhusu Sheria Ndogo*

**KWA KUWA**, Bunge linapotoa maazimio kuhusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo, linakusudia kuondoa madhara ya utekelezaji wa sheria zenye dosari,

**NA KWA KUWA**, kutokutekelezwa kwa maazimio hayo ni kuendelea kuruhusu dosari hizo ziendelee kuwa sehemu ya sheria za nchi, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge,

**KWA HIYO BASI,**

a) Mamlaka ambazo hadi kufikia mwezi Machi, 2022 hazikuwa zimekamilisha hatua ya marekebisho ya sheria ndogo zilizoazimiwa na Bunge, zihakikishe zimekamilisha mchakato huo ifikapo mwezi tarehe 1 Novemba, 2022; na

b) Mamlaka zinazohusika na Sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni wakati wa Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba wa Bunge na kubainika kuwa na dosari kama inavyoonekana katika Jedwali ambalo ni sehemu ya taarifa hii, zikamilishe mchakato wa marekebisho ya sheria ndogo ifikapo tarehe 1 Disemba, 2022.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Bunge lako tukufu kwa kuweka utaratibu wa taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika Bunge lako tukufu. Ni matumaini yangu kwamba, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii katika maendeleo ya nchi yetu utaonekana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa sheria ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. George Boniface Simbachawene, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa kuendelea kuweka uratibu mzuri wa kuwasilisha Mezani Magazeti ya Serikali pamoja na viambatisho vyake (sheria ndogo) kwa wakati. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wa Wizara kwa kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati na pia kwa kuanza hatua za utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ili kuondoa dosari mbalimbali zilizojitokeza katika sheria ndogo. Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

***4.1.1 Mawaziri***

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb) – **Waziri wa Mifugo na Uvuvi;**
2. Mhe. Innocent Lugha Bashungwa (Mb) – **Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI)**;
3. Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb) - **Waziri wa Afya**;
4. Mhe. January Yusuf Makamba (Mb) - **Waziri wa Nishati**;
5. Mhe. Dkt. Pindi Hazara Chana (Mb) – **Waziri wa Maliasili na Utalii**;
6. Mhe. Nape Moses Nnauye (Mb) – **Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**;
7. Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) - **Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi**;
8. Mhe. Suleiman Said Jafo (Mb) – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**;
9. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) – **Waziri wa Fedha na Mipango**; na
10. Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb) – **Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo**.

***4.1.2 Naibu Mawaziri***

1. Mhe. Hamad Hassan Chande, (Mb) – **Fedha na Mipango**;
2. Mhe. Abdallah Ulega, (Mb) – **Naibu Waziri - Mifugo na Uvuvi**;
3. Mhe. Patrobas Katambi, (Mb) **– Naibu Waziri - Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira;**
4. Mhe. Stephen Byabato, (Mb) – **Naibu Waziri, Wizara ya Nishati;**
5. Mhe. Pauline Philipo Gekul (Mb)– **Naibu Waziri, Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo**;
6. Mhe. Mhe. David Ernest Silinde (Mb) -**Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI;**
7. Mhe. Fred Atupele Mwakibete (Mb) – **Naibu Waziri Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi;**
8. Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb) – **Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira**;
9. Mhe. Eng. Kundo Andrea Mathew (Mb) – **Naibu Waziri, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;**
10. Mhe. Mary Francis Masanja (Mb) – **Naibu Waziri, Wizara ya Maliasili na Utalii.**

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo na hatimaye kufanikisha kazi hii. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge (*Hansard*):-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Kilumbe Shabani Ng'enda (Mb) | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan (Mb) | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Idrissa Juma Abdul-Hafar (Mb) | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Mhe. Simai Hassan Sadiki (Mb) | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Sylvia Francis Sigula (Mb) | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Emmanuel Mageni Kasalali (Mb) | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Ndaisaba George Ruhoro (Mb) | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Edwin Enosy Swalle (Mb) | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Judith Salvio Kapinga (Mb) | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Santiel Erick Kirumba (Mb) | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Jacob Tarimo Priscus (Mb) | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Regina Ndege Qwaray (Mb) | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Esther Edwin Malleko (Mb) | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Amour Khamis Mbarouk (Mb) | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Esther Lukago Midimu (Mb) | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Minza Simon Mjika (Mb) | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Khamis Ali Vuai (Mb) | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Nicholaus George Ngassa, (Mb) | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile (Mb) | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani (Mb) | Mjumbe |
| 22. | Mhe.Eng.Dkt.Leonard Madaraka Chamuriho (Mb) | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Ally Yahya Mhata (Mb) | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Francis Isack Mtinga (Mb) | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Aloyce Andrew Kwezi (Mb) | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, aidha napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Ndg. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* Katibu wa Bunge kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, *ndc* akisaidiwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Gerald Magili, kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Kamati.

Mwisho lakini si kwa umuhimu, niwashukuru Katibu wa Kamati ya Sheria Ndogo Ndg. Mkuta Masoli na akisaidiwa na Bi. Imelda Ntimba Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**4.2 Kutoa Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Jasson S. Rweikiza, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**
21 Septemba, 2022

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja imetolewa lamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa Waheshimiwa tunaanza uchangiaji, tunaanza na Mheshimiwa Edwin Swalle ajiandae Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mheshimiwa Amour Hamis Mbarouk.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuweza kuchangia taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo. Kwanza nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kututeua kuwa kwenye Kamati hii ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati hii ya Sheria Ndogo kwa kufanya kazi nzuri ya kusoma hotuba ya Kamati hii ya sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kusema kwamba wajibu wa kutunga sheria za nchi hii ni mamlaka ya Bunge lako tukufu, na wajibu huu wa kutunga sheria tumepewa kama Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 4 na Ibara ya 64 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wajibu huu sisi kama Bunge tunao wajibu wa kuulinda kwa wivu mkubwa pale ambapo Bunge linakasimu haya madaraka kwa mamlaka zingine kutunga kanuni mbalimbali za kuendesha taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kama ambavyo taarifa imesomwa hapa, Bunge lako kwa mujibu wa Ibara ya 97 inayo Mamlaka ya kukasimu madaraka ya utunzi wa sheria ndogo kwa mamlaka zingine za Serikali, na miongoni mwa hizo mamlaka ni pamoja na Wizara mbalimbali na taasisi mbalimbali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kumekuwa na shida kidogo siku za karibu, Bunge likitunga sheria mama ndani ya Bunge na kutoa mamlaka au kukasimu madaraka kwa mamlaka zingine kutunga kanuni, mamlaka hizi nyingine zimekuwa zikitunga kanuni ambazo wakati fulani zinakinzana na dhamira ya Bunge lako tukufu. Kwa sababu mamlaka ya utunzi wa sheria ni ya Bunge zinapokwenda kutungwa kanuni zingine na hizo mamlaka zikileta mkanganyiko kwa wananchi lawama zinakuwa ni kwa Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa kuanza tu naomba nitoe wito na rai sana mamlaka za Serikali zinazokasimiwa mamlaka na Bunge kutunga kanuni mbalimbali za uendeshaji wa shughuli zihakikishe zinatunga kanuni ambazo zinasaidia wananchi wetu kufanya kazi vizuri kwenye maeneo yao.

Kwa sababu kumekuwa na kero nyingi kwenye kanuni na sio sheria za Bunge. Kwa mfano Bunge lako tukufu hapa ndani lilitunga sheria ya Bunge ambayo ni sheria ya watu wa *EWURA* ikitoa mamlaka kwa Wizara kutunga kanuni kuratibu uendeshaji bora wa vyombo vya usafirishaji wa abiria. Lakini kwenye utunzi wa kanuni kwenye mamlaka husika imekwenda kutungwa kanuni ambayo inaitwa *The Land Transport Licensing Private Hire Regulations, 2020.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kanuni hii, kwenye kanuni ndogo ya 15(d) kanuni imeweka utaratibu kwamba wanaomiliki leseni za vyombo vya moto vya usafirishaji wa abiria kwa mfano wakiwemo watu wa bodaboda, watu *taxi* na kadhalika na watu wa bajaji, kila mmoja afunge mita kwenye chombo chake cha moto, ifungwe mita kwa ajili ya kukokotoa nauli za abiria. Kamati yako inajiuliza unafunga mita kwenye bodaboda kukokotoa nauli gani ya abiria. Kwa hiyo, sisi kama Bunge tunadhani waliokwenda kutunga hizi kanuni wanaweza kwenda kuleta kero kwa wananchi, na ikienda kuwepo kero inakuwa ni lawama kwa Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa hiyo kwakuwa Bunge lako lina mamlaka ya kufuatilia utunzi wa kanuni hizo, na kama zimetungwa kinyume na utaratibu au haziwezi kuwa na ufanisi mzuri Bunge lako linayo mamlaka ya kuitisha kanuni hiyo na kuirekebisha na ndio maana taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo inaliomba Bunge leo hii, kwenye moja ya maazimio yake ni kwamba tunataka mamlaka husika ikarekebishe na kufuta makosa haya ambayo yamekwenda kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, Bunge hili linapotoa maazimio kwa mamlaka ambazo zinatunga sheria ndogo mwaka jana mwezi Novemba Bunge liliazimia hapa ndani kwamba baadhi ya makosa ambayo yalionekana kwenye kanuni au sheria ndogo yakarekebishwe, lakini kama ambavyo taarifa imesomwa hapa leo, tangu mwaka jana mwezi Novemba hadi leo mwezi Septemba hizi kanuni hazijarekebishwa, tafsiri yake ni nini.  Azimio la Bunge halijafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Naomba kutao rai kwa niaba ya kamati ya Sheria Ndogo, maagizo ya Bunge Kwenda kurekebisha kanuni sio hisani, ni maelekezo ya Bunge na ni lazima yatekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lipo jambo lingine ambalo pia limesemwa kwenye taarifa ya Kamati kwamba Bunge limetunga sheria mama kuweka adhabu kwa watu mbalimbali ambao watakiuka taratibu kwenye sheria ya *The Energy and Water Utilities Regulatory Act* Namba 414; kwenye kifungu cha 8 cha sheria hii kimetoa adhabu ambayo ni kiasi cha shilingi 300,000 au kifungo cha miezi 15 na kikaitaka mamlaka husika wa watu wa maji wanapokwenda kutunga kanuni zao za kuratibu vizuri zoezi hili la shughuli za maji wamekwenda kutuma kanuni ambayo imeongeza adhabu

baada ya Bunge ambalo limeweka adhabu ndogo ya shilingi 300,000 wao wameweka shilingi 3,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge limesema adhabu isizidi miezi 15 kwa maana ya kifungo, wao wamekwenda kuweka miezi 15. Tunaomba kutoa rai tena kwamba tunaomba mamlaka zinazokasimiwa utunzi wa kanuni na sheria ndogo wazingatie maelekezo ya Bunge kwa ustawi wa nchi na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba kuunga mkono hoja taarifa ya Kamati kwamba tunaliomba Bunge likubali na kutoa maazimio kwamba kwa kuwa hizi dosari ni kubwa na zipo kwenye taarifa ya Kamati, tunaomba ifikapo mwezi Novemba, 2022 marekebisho haya yakafanyiwe kazi. Na mwisho kama ambavyo taarifa imesema marekebisho ya mwisho yafanyike mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Bunge mfano mwaka jana hapa kupitia serikali na mapenzi mema ya Mheshimiwa Rais tumepunguza hata faini kwa watu wa boda boda kutoka shilingi 30,000 hadi shilingi 10,000 ili bodaboda wetu wafanye kazi vizuri, wafanye kazi kama Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inapofika mahali kunakuwa kuna kanuni ambazo badala ya kusaidia kazi nzuri ya bodaboda zinakwenda kuanzisha utaratibu wa kufunga mita, naomba Bunge hili lisikubali na lazima haya mambo yafike mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho naliomba sana Bunge lako tukufu, sisi kama Wabunge na wawakilishi wa wananchi tuendelee kufuatilia kanuni zote ambazo zimekuwa ni kero kwa wananchi wetu, na sisi kama Kamati yako ya Sheria Ndogo kwa niaba ya Bunge hili tukufu tutaendelea kufanya kazi hii, ili kusudi wananchi wetu waendelee kufanya kazi nzuri za uzalishaji kwa ajili ya maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa upekee sana naomba mamlaka zote ambao wanatunga sheria ndogo wasitunge sheria za udhibiti tutunge sheria za kuwezesha wananchi kufanya majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji katika ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii kuwapongeza sana Mawaziri wote pamoja na Wizara zao na Serikali kwa ujumla kwa kuwa na nia safi kabisa ya kutunga sheria kulingana na mazingira na mabadiliko ya nchi na dunia kwa ujumla yanayoendelea kutokea kila siku. Ni ukweli usiopingika Tanzania ni kama sehemu moja wapo ya dunia ni wazi hatuwezi kuishi bila kufuata sheria na kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hata kama Bunge hili tutaazimia kwamba tuondoe sheria zote za nchi hii, bado tutaendelea kuishi katika zile *scope* za sheria za kimaumbile, kwa sababu binadamu toka azaliwe anaongozwa na sheria. Kwa maana hiyo hii inaonesha wazi umuhimu wa sheria katika maisha ya binadamu ni sawasawa na umuhimu wa maji hatuna namna ya kuweza kuziepuka sheria na kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi kabisa la kuzingatia katika utunzi mzima wa sheria tuelewe ya kwamba sheria siku zote ndizo ambazo zinakuja kuonesha ule uhalisia wa maisha ya wananchi yaliyowazunguka, kwa hiyo, sheria zinatakiwa na sheria ndizo zitakazokuwa zinaongoza maisha na matendo halisi ya nchi na raia wanaoishi katika sehemu hiyo, lakini suala la kujiuliza; je, ni kwa namna gani sheria hizi zinaakisi na zinafikia malengo halisi ya utunzi wa sheria zilizokuwa bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli sisi kama Kamati tumeweza kupitia sheria nyingi na kusema kweli niipongeze Serikali kwa kazi wanazoendelea kuzifanya, lakini changamoto haziwezi zikakosekana, utaona kwamba mantiki walizokuwa nazo Wizara na Mawaziri wetu katika utunzi wa hizi kanuni na sheria ni nzuri na unaweza kuikuta kanuni ile kwa asilimia 100 inawezekana inakidhi matakwa na mahitaji ya jamii husika, lakini ikakosa ubora kutokana na kipengele kimoja tu au vipengele viwili ikaitoa maanani sheria yote ikaonekana haina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika utaratibu huu ni vizuri zaidi kwa watunzi wa kanuni na sheria kuzingatia mazingira na matakwa halisi ya sheria na jamii nini inachohitaji kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano ningependa sana nilizungumzie ule usawa na uhalisia wa sheria na kanuni tulizoweza kuzipitia na mazingira halisi ya Watanzania tunayoishi. Nichukulie mfano ukiangalia mfano Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Itigi kipengele namba 14(3) kinaeleza wazi kwamba abiria yeyote atakayetupa taka nje ya basi la abiria basi itachukuliwa kosa hilo limefanywa na dereva, kondakta au

mmiliki wa basi hilo, ukiangalia mantiki ya kutunga hiyo sheria unajua wazi kwamba lengo ni kuweka usafi wa mazingira katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la usafi wa mazingira katika nchi ni suala la Kikatiba ni wajibu wa kila mtu, ukiangalia Ibara 27(1) ni wajibu wa kila Mtanzania kuweka mazingira safi na salama. Tunajua dhamira ilikuwa ni nzuri lakini nani wa kuadhibiwa? Hakuna utaratibu duniani kosa lifanywe na mtu 'A' baadaye aende akaadhibiwe na mtu 'B' hiyo sheria itakosa maana, hivi kweli kosa kafanya abiria itakuwaje aende akaadhibiwe kondakta au mmiliki wa basi? Kwa nini? Tutoke na tukimbilie kumtafuta mmiliki wa basi, wakati mmiliki wa basi, dereva au kondakta katekeleza majukumu yake kuhakikisha usafi unadumu na unatekelezeka katika gari yake pengine kaweka *dustbin* na vifaa vingine vitakavyoweza kusababisha usafi usitoke nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini abiria mwenyewe tu akaamua kufungua kioo akatupa taka nje, leo hii unaenda kumkamata nani dereva, uwajibikaji katika sheria na usawa uko wapi? Sasa ukiangalia katika mazingira kama hayo haitokuwa hiyo sheria ina uhalisia katika utekelezaji, kwa sababu ni mwiko katika sheria kuadhibiwa mtu kwa kosa ambalo hakustahiki kuadhibiwa nalo hakuna kitu kama hicho duniani na haya itakuwa tuseme kwamba Tanzania tunatunga sheria za kwamba aliyefanya kosa mtu mwingine baadaye anakwenda kuadhibiwa mtu mwingine maana yake lile lengo la sheria halitofikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu lengo la sheria ni kumfanya yule ambaye amefanya kosa kupata adhabu ili kutoa funzo kwa wengine wasirejee makosa kama yale, sasa leo kosa kafanya baba umeenda nyumbani baba umemkosa unamkamata mama na watoto haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ikiwa katika nchi hii tukitunga sheria za namna hiyo, tusema kwamba tunatunga sheria kwamba anayefanya kosa siye anayehusika moja kwa moja katika adhabu tunazidiana kwa niaba hivi kweli nchi inaweza kutawalika, sio kweli kabisa kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kusema kweli katika hali kama hii tuangalie ile mantiki ni nini na kipi kinachotakiwa kufanywa ili sheria zetu ziweze kusadifu mazingira halisi na kugusa wale walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliishie hapo nchi yetu kwa asilimia kubwa raia wake ni wakulima na wafugaji. Wakulima wanaishi sana katika sehemu za kijiji, vijiji vingi ndivyo ambavyo unaweza ukawakuta wakulima; ukienda katika Ibara ya 4(1) ya sheria ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Itigi utaona wameweka baadhi ya masharti ambayo yanawataka wakulima wanapotaka kulima lazima wafuate kalenda ya Halmashauri, sio wazo baya

lakini unajiuliza *how come* inaweza kutekeleza hii sheria kwamba sisi sote tulime kwa kufuata kalenda ya Halmashauri, ipo wapi hiyo kalenda ya Halmashauri. Namna gani una uwezo wa kuifuata wapi ipo, je, ni namna gani mwananchi anauwezo wa kuielewa imeandikwa, imebandikwa sehemu, imetangwazwa yaani unapatwa na maswali mengi ambayo yanauwezo wa kukosa majibu katika *application* yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuiandika ni rahisi, tamu kumeza, lakini ngumu kutafuna yaani kuitamka tu hivi kuiandika inawezekana kuwa rahisi, lakini namna gani katika utekelezaji wake ndipo shida inapokuja. Unaposema kwamba tufuate kalenda ya Halmashauri, tukienda katika *aspect* za utekelezaji kilimo unaweza ukakuta katika mazingira tuliyokuwa nayo mtu analima vile anavyojisikia, hakuna mtu anayelazimishwa kwamba bwana wewe uende ukalime analima kwa wakati wake na anavuna kwa wakati wake. Sasa ukisema kwamba tufuate hiyo kalenda, hiyo kalenda unapata maswali inaanzaje katika mazingira kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu analima yeye mwenyewe anavyojisika, anavuna yeye mwenyewe anavyojisikia, lakini hakuna sheria hata moja inayoenda kumlazimisha mtu kwamba lazima alime kwa eneo la ukubwa wa kiasi fulani, kwa maana hiyo itakuwaje tuki-*impose* kifungu cha sheria kinachotaka wakati wa kulima lazima ufuate kalenda ya Halmashauri, haiwezekani, itakuwa hilo ni jambo gumu. Unajiuliza hivi Halmashauri wana kalenda ya mvua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake unaweza ukajiuliza mvua wanakalenda nayo wanajua ni *exactly* wakati gani mvua ina uwezo wa kunyesha. Hivi katika mazingira ya kawaida tunayoishi wale raia wa kawaida vijiji huku hivi taarifa hata hawana leo hii mnamtungia sheria za namna hiyo tunajua mantiki ni nini, lakini tuangalie ule uhalisia wa hiki kitu ambacho tunachotaka kwenda kukisimamia, pengine tukikosa kukiwekea mazingira mazuri basi hata utekelezaji wake utabakia katika maandishi tu lakini uhalisia utakuwa haupo kwa sababu kuna mazingira mengine mtu analima pengine kutokana na kipindi hiki nalima mazao haya na ardhi yangu nalima hiki hana kalenda huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwingine anaweza akasema kwa kipindi hiki nina uwezo wa kufanya jambo moja, mbili, tatu au ana uwezo wa kuanzisha kilimo cha umwagiliaji, hili kalenda ya Halmashauri ina nafasi gani katika suala hilo, lakini ukiachilia hapo katika wakulima vile vile kuna suala la wafugaji Ibara 3 ya hiyo kanuni na hiyo vilevile haikuacha imewekea masharti ambayo ni magumu kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano hiyo kanuni inamtaka mfugaji yeyote atayekuwa anafuga wanyama katika Halmashauri ya Itigi ni lazima idadi ya mifugo itaamuliwa na Halmashauri, Halmashauri ndio

itakayokupangia wewe, wao ndio mabwana wakubwa itakupangia idadi ya mifugo utakayotakiwa kufuga. Kiukweli kabisa ukisoma hiyo sheria unajua mantiki ni nini tunajua kabisa ni matumizi bora ya ardhi pengine, lakini ukienda katika *application* vipi inaweza kutekelezeka, vipi inaweza ukaenda kum-*control* mfugaji amenunua eneo lake huko kijijini anafuga kuku wake, wewe utampitiaje mfugaji mmoja mmoja wa kuku halafu um-*control.* Hivi kweli inaweza kutekelezeka mtu anafuga kuku wake, njiwa, kwa sababu hiyo sheria ukija kutafsiri hilo neno wanyama, wanyama inajumuisha mjumuiko mpana zaidi maana yake ngo'mbe, kuku, bata, njiwa hata kunguru na mende pia vilevile ni Wanyama. Kwa sababu sheria imejumuisha, je, ana uwezo wa kufuga na nani? Ni binadamu na mende siku hizi wanafugwa na binadamu. I*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namna gani ukiangalia unaweza kuchukua kama ni vitu vidogo vidogo lakini ukiangalie yule anayeiandika anaenda kuisimamia ni tofauti, sasa yule anayekwenda kuisimamia inawezekana akaja na mtazamo tofauti na yale malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa masuala kama hayo ni vizuri yakawa *under control,* ni vizuri kwakuwa hizi sheria nyingi za Halmashari zinazotungwa takribani zote zinakuwa zinafanana sasa ili kuepuka matatizo kama haya ni vizuri watunzi wetu wa sheria wakawa wanaangalia ile mifumo inayoongoza katika utungaji bora wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, ajiandae Mheshimiwa Tumaini Bryceson, ajiandae Mheshimiwa Kunti.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi ya kuchangia katika wasilisho hili la sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakushukuru kwa kutuchagua pia katika jambo hili au katika Kamati hii ya Sheria Ndogo, tunakushukuru sana wewe na Mheshimiwa Spika kwa sababu Kamati ya Sheria Ndogo kimsingi ndiyo Kamati inayoendeleza Miji, Halmashauri, Vijiji, kuna sheria nyingi hapa ambazo sisi zitatufanya tuelewe kila kitu kinachokwenda ndani ya nchi hii, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, mama msikivu, muadilifu, mwenye hekima, mwenye huruma kubwa sana kwa wananchi wake na hii ni kwa sababu anatoka kwenye Chama cha Mapinduzi, chama ambacho kinatekeleza Ilani yake kwa uangalifu na uadilifu sana. Mama

huyu ukilalamika tu tozo yeye anaondoa, sijui halmashauri hii haina shule anakuletea, hakuna hospitali mahali analeta, huyo ndiyo Mama Samia kutoka Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka Mama Samia anafikia kwenye maamuzi hayo au kwenye sifa hizo ni kwa sababu Tanzania ni nchi tunayoisifu na inayosifika duniani kwamba ni nchi yenye utawala bora. Na nchi hii yenye utawala bora ni utawala wa sheria, na sheria hizi ndiyo tupo kwenye sheria ndogo, sheria zinazoongoza huko vijijini na kwenye halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba sana wale ambao wamekasimiwa madaraka na Bunge kutunga sheria hizi tunazoziita sheria ndogo basi wawe makini sana kwa sababu hizi sheria tunaziita ndogo, lakini ndiyo zinazowafanya watu wawe jela, ndizo zinazowafanya watu watozwe faini. Kwa hiyo, si sheria ndogo kama tunavyosaini ni sheria hasa za nchi. Kwa hiyo, tunawaomba sana wawe makini sana na hii ni kwa sababu Waarabu wana msemo wao wanasema *dawamulhali minalmuhali* (mtu hadumu kwa kwa hali moja Maisha) na sheria hizi zinaenda kusimamiwa na watu mahakamani, leo hakimu anaweza kuwa na hasira akatumia sheria ndogo hii hii akamuonea mtu. Kwa hiyo, ili tumdhibiti hasira zake, furaha yake, huzuni yake lazima tuweke sheria ambayo itamuongoza asije akaongozwa kwa hisia zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano hapa wa sheria inayoitwa *Electricity Act*, Sura 131; kuna sheria ndogo inasema *Electrical Installation Services* hii imetoa adhabu mbili; adhabu ya kwanza kwa mtu ambaye hana leseni ya kufanya *installation* ni faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichozidi miaka mitano au vyote viwili, lakini mtu mwingine anayo leseni, lakini atafanya jambo nje ya leseni yake, leseni imekwambia wewe kazi yako ni kuweka waya tu hautakiwi baada ya waya kuweka *meter* kwa mfano, kuweka *plug,* yeye kwa sababu ya ubinadamu wake akapitiwa akaweka vile vitu, kwa hiyo, yeye anatakiwa alipe shilingi 200,000; lakini amefanya kitu ambacho ni nje ya leseni yake maana yake ni kwamba tuna mli- *guard* kwamba huyu leseni pia hana jambo alilofanya hana leseni, lakini sheria imemfanya kwamba yeye alipe faini shilingi 200,000. Sasa lazima tuwe waangalifu tusiwe na *bias* kwamba huyu yupo hivi yupo hivi, lazima tufike mahali wananchi wetu wote ni wamoja tuwe na huruma kama alivyo Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale tunaomwakilisha lazima tuwe makini katika jambo hilo. Lakini sawa ulishaliona tatizo hili sheria ndogo ilishaona tatizo tumeitana na tunawasifu Mawaziri *Mashallah Alhamdulillah,* ni wasikivu sana wanalichukua tunakubaliana tunaenda kulirekebisha hasa hiyo kurekebisha hiyo huku sheria ipo mtaani inafanyakazi, lakini hapa muda

wa kurekebisha watu wanaumia *field,* hairekebishwi inatuchukua muda mrefu sana mpaka kurekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwa ametoa wazo kwamba Bunge hili liazimie kwamba sasa kazi inapotolewa hii ya kurekebisha iwe na muda maalum. Kwa hiyo, tunaliomba sana Bunge lifanye hivyo kwasababu hizi sheria ndiyo zinaumiza watu wetu kule *field*. Tuwafikirie watu wetu kwamba wao ndiyo wanaumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Tumaini Magessa, ajiandae Mheshimiwa Kunti, hayupo? Mheshimiwa Kunti, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Leonard Chamuriho, Mheshimiwa Judith Kapinga na Mheshimiwa Mtinga.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kuhusiana na suala zima la hizi sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa niaba ya Bunge ama kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo imetueleza vizuri kwamba lengo la madhumuni ya kuwepo kwa hizi sheria ndogo. Tunapokwenda kutunga sheria kwa mfano sisi Wabunge, sisi Wabunge humu ndani wote si wanasheria, lakini Ofisi ya Spika imeamua kuwa na utaratibu kunapokuwa na Muswada, kunapokuwa na jambo lolote linalohusu sheria Kamati inayohusika *either* ya sheria inayotungwa kwenye Wizara yoyote ile Kamati kupatiwa fursa ya kupewa uelewa wa pamoja ili Bunge linapokwenda kufanya maamuzi ya sheria husika Wabunge wote waweze kuwa na uelewa wa sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye halmashauri zetu Madiwani wetu ndiyo wanaopitisha ama ndiyo wanaotunga hizi sheria ndogo, lakini Madiwani wetu hawapati fursa ya kupitishwa ili waweze kupata uelewa wa hiyo sheria inayokwenda kutungwa ina madhara gani kwenye halmashauri hiyo, ama ina madhara gani kwa wananchi wa eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, cha kwanza niiombe Wizara inayohusika na suala zima la halmashauri iweze kuona ni namna gani inakuwa inawapa semina Madiwani wetu ama inawapa elimu elekezi ya kwanza kabla hawajaanza kutunga hiyo sheria ili Madiwani wetu waweze kupata uelewa wa pamoja na wanapokwenda kutunga hiyo sheria iweze kuwasaidia wananchi na si kuwakwaza na kuwakandamiza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna wanasheria pia wa halmashauri. Wanasheria wetu wa halmashauri pia kutokana na wingi na shughuli nyingi zilizopo ndani ya halmashauri na wao pia wamekuwa nyuma kwenye suala zima la utungaji wa sheria. Lakini pili, wamekuwa hawapati semina ambazo zinawasaidia kuendelea kuwaongezea uwezo ili waweze kulishauri Baraza vizuri na kwenda kutunga hizo sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pia niishauri Serikali kwamba waweze kuona sasa ni wakati umefika wa kuweza kuwapatia semina wanasheria wetu ndani ya halmashauri ili waweze kuendelea kuongeza uwezo na kuweza kuwasaidia Madiwani wetu kwenda kupitisha hizo sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na kanuni nyingi sana ambazo zinatungwa na halmashauri na kanuni hizi zinatofautiana kwa kila halmashauri na kwenye kila halmashauri inategemea Halmashauri za Mijini, Halmashauri za Majiji, Halmashauri za Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Halmashauri za vijijini; waliopo wengi vijijini ni wakulima na wafugaji. Kwenye halmashauri zetu kuna kanuni ambazo zinatungwa suala zima la ukusanyaji wa mapato ambalo na wewe umetoka kulizungumza asubuhi ya leo. Mkulima amelima hajapewa mbegu na Serikali, hajapewa jembe na Serikali, mvua ya kutegemea Mwenyezi Mungu, hana chochote ambacho amewezeshwa, amelima ndani ya halmashauri yake, anatoa mazao yake shambani mkulima anaenda kukutana na geti limewekwa barabarani eti alipe ushuru wa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujakataa kuchangia maendeleo ya Taifa letu, lakini je, tunachangia kwa utaratibu upi? Mkulima aliyelima kwa jasho lake anatozwa ushuru anayekuja kununua mazao kwa mkulima anachajiwa ushuru mdogo sana, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba. Mkulima shambani anatozwa gunia shilingi 1,500 huko mashambani, lakini huyu mnunuzi ambaye amekuja kununua mazao anaambiwa yeye anapewa kibali cha kununua mazao jumla analipa shilingi 750. Sasa hivi vitu sheria zinakuwa kwa namna gani yaani mkulima aliyelima yeye ndiye anayezalisha kwenye eneo husika kanuni zetu ambazo Madiwani wetu huku wanazozitunga zinakwenda kumkandamiza huyu mwananchi wa chini halafu zinam-*fever* huyu mtu wa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukija kwenye suala zima la mifugo kwenye halmashauri za vijijini tuna minada ya mifugo, hii minada ya mifugo inamtaka mfugaji anapotaka kwenda kuuza mfugo wake siyo maeneo kata zote zenye minada anapotoka kwenye Kata A kwenda Kata B kuuza mfugo wake ni lazima awe na kibali na kile kibali ni cha kumtambulisha yeye aweze

kutambulika kwamba ule mfugo ni wa kwake na anahitaji kwenda kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye halmashauri zetu wametunga sheria ya hizo kanuni za kum-*charge* mfugaji fedha ya kupeleka ng'ombe wake ama kuku wake ama mbuzi wake kwenda kuuza mnadani, halafu yule anayenunua kule hawam-*charge*, mfugaji yeye anakuwa *charged,* lakini mnunuzi akinunua yule ng'ombe anachukua ile risiti ya mfugaji ndiyo anatembea nayo barabarani na kwenye magari mpaka anafika anakowapeleka. Kwa hiyo, ukiangalia hizi sheria bado Madiwani wetu hawajawa na uelewa mzuri wa namna bora ya kuweza kutunga hizo sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kanuni pia za Mawaziri, naomba nizungumzie Wizara ya Afya ni kweli kwamba wakina mama wajawazito wanatakiwa waweze kufika kliniki lakini pia waweze kujifungulia kwenye kliniki zetu, lakini ni ukweli usiofichika kwamba kwenye maeneo yetu yaliyo mengi bado hatujawa na zahanati za kutosha kwenye maeneo yetu, hatuna vituo vya afya vya kutosha kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mama huyu akitoka zaidi ya kilometa 20 ama 30 kwenda kutafuta hicho kituo cha afya ama zahanati ni mbali, wakati mwingine uchungu unapokuja anakuwa bado hajajiandaa wala hajui ni saa ngapi uchungu utafika, akijifungua anapotoka nyumbani anaenda anampeleka mtoto wake kliniki anapigwa faini na mimi kwangu halmashauri ya Wilaya ya Chemba mwaka 2020 nilikutana na hicho kitu wakati wa kampeni, ilikuwa mtoto mwanamke akijifungua mtoto wa kiume anakuwa-*chaeged* faini akijifungulia nyumbani akienda kliniki anakuwa *charged* faini mtoto wa kiume shilingi 30,000, mtoto wa kike shilingi 50,000 wakiuliza hizi ni kanuni tumeletewa, hii ndiyo sheria tunayo tekeleza sisi tumeletewa ili tuweze kutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, muone kwamba wakati mwingine hivi vitu *either* inaweza hata haikupelekwa, lakini kwa kuwa wananchi wetu hawana uelewa wanakwenda kujificha watumishi wetu watekelezaji wa hizi kanuni na sheria wanaenda kuwaumiza wananchi wetu kwenye maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, TAMISEMI suala zima la watoto wetu kupata chakula shuleni; hatukatai ni jambo jema sana ili kumpunguzia mtoto umbali ule mrefu wa kwenda na kurudi apate chakula shuleni ili aweze kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mzazi ana watoto wanne wako shuleni, shule imeamua kujipangia utaratibu na mbaya zaidi hawashirikishi kabisa wazazi wanakaa Kamati ya Shule kule, inapanga, inaanza kupeleka migambo huko

chini kwamba mzazi ana watoto wanne anapangiwa kila mtoto apeleke gunia la mahindi kwa muhula, debe la maharage. Mzazi huyu anakuwa hana uwezo wa kuweza kuwahudumia hawa watoto wote apeleke magunia manne na debe nne za mahindi anaanza kulipa kwa awamu kidogo kidogo *let say* huyu wa kwanza kamlipia, wa pili hivyo ili aweze kupunguza huo mzigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha wazazi hawa wamekuwa wakifanyiwa vitu vya ajabu, mzazi anaenda anakamatwa na mgambo kwa nini hajalipa chakula cha mtoto, *okay* akikamatwa na mgambo hela ya mgambo anatakiwa alipe yeye 30,000 anaenda kwenye Baraza la Kata anaambiwa alipe fedha ya Baraza, akitoka hapo anatakiwa kupigwa faini na Kamati ya Shule eti ameshindwa kulipa chakula kwa ajili ya watoto kwenda kupata chakula shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hizi kanuni bado tuone ni kwa namna gani zinakwenda kufanyiwa utafiti ili tuweze kukidhi mahitaji ya wananchi wetu huko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine hizi kanuni zote na sheria zote zinatungwa ili ziweze kuwasaidia wananchi wetu wasiweze kupotoka kwenye maeneo mbalimbali, lakini zitungwe sheria ambazo ni rafiki na kabla ya kutungwa tuwashirikishe watu husika ambao wanatekeleza hiyo sheria tusitunge sheria halafu mwisho wa siku watekelezaji inakuja kukutana nalo barabarani halafu mwisho wa siku inakuja kutuletea shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusiana na suala zima pia ya hizi sheria zetu na Kamati pia wamelisema, sheria zinatungwa wakishatunga kabla hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali sheria zinaanza kutumika matokeo yake zinaleta hasara kubwa sana kwenye halmashauri zetu kwa sababu zikianza kutumika mtu anaamua kwenda kushtaki, akishtaki halmashauri ikipelekwa kule kesi tunaenda tunashindwa kwa sababu sheria kwanza haijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali haikuwa tayari kwa matumizi. Kwa hiyo, mwisho wa siku tunaingiza halmashauri kwenye madeni makubwa ya kulipa gharama mbalimbali ambazo hazikuwa na sababu. Kwa hiyo. Mimi niwashauri pia Serikali waweze kuona kuelekeza halmashauri zetu zinapotungwa sheria hizi ndogo ndogo zihakikishwe zinaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, ajiandae samahani kidogo Dkt.

Wageni waliopo Bungeni muda huu; wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo wageni 5 kutoka Jumuiya Ah-Madia Muslim Jamat

Tanzania wakiongozwa na Sheikh Tahir Mahmood Choudhry ambaye ni Amiri na Mshauri Mkuu. Karibuni Dodoma, karibuni Bungeni, ahsanteni kwa kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, ajiandae Mheshimiwa Judith Kapinga.

**MHE. ENG. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya ya kuliongoza Taifa letu vizuri na kuwa msikivu katika changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza katika taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati Dkt. Rweikiza kwa kazi nzuri aliyofanya ya kutuongoza sisi wanakamati katika kutekeleza jukumu hili adhimu ambalo la uchambuzi huu wa sheria ndogo kazi ambayo tumepewa na Bunge lako tukufu na ambayo tumeifanya kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraka ya kutunga sheria zote yanatolewa na Katiba yetu katika Ibara ya 4 na Ibara ya 64 ambayo Bunge lako tukufu limepewa lakini katika Ibara ya 97 ya Katiba hiyo hiyo imetoa fursa ya kukasimu madaraka hayo kwa Idara au mtu yoyote ambaye itaona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ningependa kuchukua fursa hii kuwapongeza hawa waliokasimiwa kufanya kazi hiyo ambayo wengi ni Mawaziri, Naibu Mawaziri pamoja na watumishi kwani wamefanyakazi hiyo kwa umakini. Wametuletea sheria nyingi sana sheria ndogo lakini ni sheria 11 tu ambazo zimeweza kuleta tashiwishi na kuweza kuleta uchambuzi huu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzingatia vigezo vya uchambuzi ambao tumefanya katika Kamati yetu mimi nitajikita zaidi katika usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali katika sheria ndogo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi sheria ndogo zinapotungwa lengo lake kuu ni kurahisisha utekelezaji wa sheria mama ili ziweze kueleweka vizuri zaidi na kuelezeka kwa urahisi zaidi. Hivyo ikiwa sheria hizo hazikuandikwa kwa usahihi na kwa umakini mkubwa, basi zinaweza zikaleta mkanganyiko katika utekelezaji wake au changamoto vilevile katika ulewela ulio sahihi.

Kwa hiyo, nitaangalia katika kurejea kanuni sahihi katika utungaji wake, lakini vilevile kuangalia kama kanuni hizo ambazo zimerejewa zipo au

hazipo, lakini vilevile kama maudhui yaliyotakiwa kuwepo katika kanuni hizo ni yale ambayo yalikuwa yamelengwa na sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, wajibu uliokasimiwa wa kutunga sheria ndogo unaweza kupoteza maana yake kama haya majedwali ambayo lengo lake lilikuwa ni kurahisisha badala yake linakwenda kuzua changamoto au ugumu wa uelewa katika kanuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano michache; katika sheria ndogo ya *The Electricity Electrical Installation Services Rules* ya mwaka 2022 ambayo imetungwa kupitia Sheria ya *Electricity Act,* Sura ya 131 kuna majedwali ambayo yamewekwa mle, katika jedwali la nne la kanuni hiyo linamruhusu mwenye leseni ya uunganishaji umeme akishaunganisha basi ampatie mteja wake cheti cha kuonesha nini amefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya kanuni hiyo yanataka huyo muunganishaji atoe cheti hicho na kuelezea kila kitu kilichopo na yanasema kwamba muonekano wa cheti hicho ni kama ambavyo umeonekana katika jedwali hilo. Ukiangalia jedwali hilo muonekano wa cheti hicho haupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unakuta sasa kanuni hii japokuwa imetoa mwelekeo kwamba nini kifanyike, lakini cheti ambacho kinatakiwa kitolewe au muonekano wake haupo katika kanuni hiyo. Kwa hiyo, badala ya kuwa imesaidia imeleta tena mkanganyiko mkubwa zaidi kwani imesema toa cheti kama kilivyooneshwa katika jedwali na kwenye jedwali cheti hicho hakipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ambao nautoa ni huu wa kanuni ya *The Copy Rights Enabling Rights, Licensing and Rights to Benefits Re-Sells Regulation* ya mwaka 2022; kanuni hii nayo imetokana na Sheria ya *The Copy Right and Enabling Rights Act,* Sura Namba 218.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali la sheria hii limetoa mfumo wa kutoa mgawanyo wa mapato, wao wameita *distribution rules for public performance and broadcasting,* lakini utakuta kwamba kanuni ambayo imetungwa hapo, maudhui yake yanatokana na kifungu cha 29 cha sheria hiyo. Lakini ukiangalia maudhui ya sheria na kanuni iliyotungwa ni vitu viwili tofauti. Kwa hiyo, unakuta sasa badala ya kanuni hiyo kwenda kurahisisha utekelezaji wa sheria hiyo, inakwenda kuleta changamoto kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, umakini mkubwa unatakiwa na tunashukuru sana uongozi wa Mwenyekiti wetu ambaye alituongoza vizuri katika kupitia kanuni hizi ili kuhakikisha kwamba hatuleti mchanganyiko mkubwa na wajibu uliokasimu kwa hawa kutunga sheria ndogo unatekelezwa kwa usahihi na kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine uko katika Sheria ya *The Tanzania Shipping Agencies Performance Benchmark Regulations* ya mwaka 2022; kanuni hii imetokana na *The Tanzania Shipping Agencies Act,* Sura Namba 415. Katika kanuni hii, kanuni ya 16 inayohusu utolewaji wa notisi, notisi ya ukubalifu yaani *compliance notice* ambayo ni kitu muhimu kwamba ameridhia au amefanya kitu ambacho kinatakiwa kufanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeelekeza kuwa wakala wa meli atatoa notisi kwa namna ilivyofafanuliwa katika jedwali la tatu. Kwa hiyo, unakuta kwamba jedwali limetamkwa vizuri kwamba notisi itatolewa kwa mfumo huu. Ukienda kwenye jedwali hilo, unakuta kwamba jedwali hilo la tatu halipo. Sasa unakuta huku umeelekezwa uende jedwali namba tatu ukapate mwelekeo wa hiyo notisi, lakini kwenye utekelezaji utakwama kwa sababu jedwali hilo halipo. Kwa hiyo, hiyo italeta usumbufu katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ambao naweza kuutoa ni kuhusu muingiliano au mchanganyiko unaoletwa na lugha katika sheria; hHii nitatolea mfano katika *The Mining Government Mineral Warehousing Regulations* ya mwaka 2022 ambayo inatokana na *The Mining Act,* Sura namba 123.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali hilo utakuta linakudai fomu namba tatu ambayo imetungwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili, lakini ukiangalia usahihi wa maneno katika fomu ile Kiswahili na Kiingereza unakuta kwamba maana hazilingani au hazishabihiani. Kwa hiyo, unakuta kwamba hii inaleta changamoto katika ule utekelezaji, nini kifatwe, tafsiri ya Kiingereza au tafsiri ya Kiswahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta kwamba katika jedwali hilo hilo, fomu nyingine zimetungwa kwa lugha moja tu ambayo ni Kiingereza, basi Kamati yetu imeona kwamba ni muhimu kabisa kwamba lugha inayotumika ieleweke vizuri na tafsiri zishabihiane ili kutoleta mchanganyiko katika utekelezaji wa hayo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Judith Kapinga, ajiandae Mheshimiwa Francis Mtinga na ajiandae Mheshimiwa Mpina.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Sheria ndogo kwa jina lake zinaweza kudogoshwa, zinaweza zikachukuliwa kama kanuni na taratibu ambazo labda hazina umuhimu sana, lakini kiuhalisia sheria ndogo ndizo zinazoendesha maisha ya kila siku ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze kwa kuishukuru Serikali na mamlaka zilizokasimiwa kwa kutunga sheria ndogo. Kwa kweli kama wangekuwa wanatumia vibaya mamlaka hayo, pangekuwa pana mtifuano mtaani. Tunaamani na utulivu kwa sababu mamlaka zilizokasimiwa kutunga sheria ndogo zinatendea haki mamlaka hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo zimebeba mstakabali wa haki za watu, ndizo sheria ambazo zina-*define* haki na usawa wa watu katika jamii, ndizo sheria zinazoleta muongozo katika haki za msingi ikiwemo haki ya kupata kipato, haki ya kupata ujira, haki ya usalama na faraha na haki ya kushirikiana na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, haki hizi hususan haki ya ajira na ya kupata kipato ambazo ni muhimu kwa maisha ya binadamu ya kila siku na ambazo ni haki za Kikatiba, ni za muhimu sana ziangaliwe pale ambapo sheria ndogo zinatungwa. Kwa sababu ndizo ambazo zinagusa uhalisia wa maisha ya watanzania ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo mchakato wake ni tofauti na sheria mama. Sheria ndogo zinapotungwa na mamlaka zilizokasimiwa mamlaka hayo na Bunge, zinaanza kutumika kabla hazijaletwa Bungeni kupitiwa na Bunge na ndiyo maana ni muhimu sana kwa mamlaka zilizokasimiwa madaraka hayo kuhakikisha sheria ndogo zinazotungwa zinalinda haki na ustawi wa Watanzania, lakini vilevile zinazingatia masharti ya maendeleo katika jamii zetu za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya changamoto ambazo zimesemwa na Kamati ni sheria ndogo kutokuzingatia masharti ya uhalisia katika jamii, yaani zinatungwa bila kuangalia uhalisia wa maisha ya Watanzania. Jambo hili limekuwa likileta changamoto za mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, na napenda nianze kwa kusema kuhusiana na Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025. Dira ya Maendeleo ya Tanzania inasema tutajenga uchumi imara, anuai, himilivu na shindani ambao utazingatia mabadiliko ya masoko na teknolojia. Kwa hiyo, lazima sheria ndogo zinazotungwa ziende kwa mlengo huu ili kuhakikisha ya kwamba Taifa letu linapata maendeleo kwa kadri ya tulivyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa napenda nielezee masuala ya sheria ndogo yanavyoshika masuala ya teknolojia ambavyo siyo sahihi. Napenda nielezee kanuni elekezi za *LATRA* ambazo zimesababisha kampuni za teknolojia kama Bolt na Uber kusitisha huduma zake hapa nchini kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni elekezi za *LATRA* hazikuwa sahihi. Nasema hazikuwa sahihi kwa sababu zinaenda kinyume na Dira ya

Maendeleo ya 2025, lakini pamoja na hilo, *LATRA* hawakuwa na mamlaka ya kutunga kanuni zile ambazo zinasababisha kampuni za ubunifu na teknolojia kusitisha biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *LATRA* inahusiana na ku-*regulate* usafiri siyo masuala ya teknolojia. Bolt na Uber siyo kampuni ya usafirishaji, ni kampuni ya ubunifu na teknolojia. Kwa hiyo, *LATRA* hawakuwa na mamlaka ya kutunga kanuni ambazo zinaenda kufungia ubunifu wa teknolojia ya Uber na Bolt. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika nchi yetu yametapakaa. Kisera yako Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, lakini kiutendaji kwa kiasi kikubwa yako Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Sasa *LATRA* walipata wapi mamlaka ya kugusa masuala yanayoendana na teknolojia hali wakijua mamlaka yao ni kwenye masuala ya usafirishaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa napenda niishauri Serikali yangu, na ushauri huu niliutoa mwaka jana; masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu yameparanganyika, ni wakati sasa tuwekee uratibu ili kuhakikisha wabunifu hawa hawawi *frustrated.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni za Uber na Bolt kama zilivyo kampuni zingine za ubunifu, ni kampuni za hiyari kujiunga, mtu halazimishwi kujiunga, na kampuni hizi zinagusa maslahi ya pande mbili; zinagusa maslahi ya wananchi na zinagusa maslahi ya madereva.

Mheshimiwa Naibu Spika, *LATRA* kwenye kanuni zao walisema wanafungia Uber na Bolt kwa sababu wana-*charge* madereva *commission* ya asilimia 20 mpaka 25. Wanataka Uber na Bolt wa-*charge commission* isiyozidi asilimia 15, sawa labda hoja ipo. Labda hoja ipo, lakini *LATRA* baada ya Uber na Bolt kusitisha huduma ndiyo wanasema tutakaa nao mezani. Jamani kila siku tunasema hapa, nyenzo namba moja ambayo inachagiza ajira duniani kote ni nyenzo zinazoendana na sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeweka *commitment* ya ajira milioni 10. Ajira hii kwa urahisi itapatikana kwa nyenzo za sayansi na teknolojia, siyo popote pale. Sasa *LATRA* walitakiwa kukaa mezani na kujadili kabla ya kufunga na siyo wamefunga ndiyo wanasema watajadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii zaidi ya vijana 100,000 ambao walisema walikuwa wanawatetea wako mtaani. Ile asilimia 15 wanapata? Hawapati, wameanza upya kwa *applications* nyingine. Sasa tunaenda mbele, tunarudi nyuma? Wale waliokuwa wanawatetea hawafanyi biashara, wananchi ambao walikuwa wanapata ahueni na wenyewe mambo yao ni magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie, ile shilingi 30,000 ambayo labda mwananchi alikuwa analipa akitoka Mwenge kwenda Posta, alikuwa analipa kwa shilingi 10,000. *LATRA* unaumia nini mwananchi akilipa shilingi 10,000? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nia yetu, nia ya teknolojia ni kurahisisha maisha kwa wananchi. Mwananchi maisha yake yamerahisika sasa sisi tunaumia nini? Kama kulikuwa kuna jambo si wanakaa mezani tunalitatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, uliangaliwa upande mmoja, upande wa wananchi ambao maslahi yao na haki zao ambao maisha yao yamerahisika hawakuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi napenda niishauri Serikali yangu wawashauri *LATRA,* kanuni hizi wazivute nyuma. Kwa kweli ni kanuni ambazo hazina maslahi kwa madereva wala kwa wananchi ambao walikuwa wananufaika kwa huduma ya Bolt na Uber. Lakini vilevile tuangalie na *document* zetu kama dira za maendeleo. Kwa sababu kama tukiwa tunatunga kanuni kama hizi kwakweli inakuwa hatuwatendei haki Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi Kampuni za Uber na Bolt hizi siyo teknolojia zao kwa hapa Tanzania, wananunua hakimiliki. Kwa hiyo, na wenyewe wanazilipia, walipaswa kusikilizwa kwenye *commission* wanayoipata asilimia ngapi ni faida yao wenyewe binafsi? *Investment* yao wanailipiaje? Lakini siyo kuwafungia tu, kwa sababu hizi siyo teknolojia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mfano wa nchi nyingine, kwa mfano ukilipa shilingi 70,000 kama nauli ya Bolt ama ya Uber kuna *charge* nyingine ambazo zinaenda kwa mwananchi ambazo zinakaribiana na nusu ya ile bei karibia shilingi 30,000. Lakini kwa wenzetu hizi Uber na Bolt zinaendeshwa na wale wamiliki wa gari wenyewe, yaani kama mimi nina IST yangu ndiyo najisajili naendesha mwenyewe. Kwa hiyo, ile faida ya moja kwa moja naipata mimi mwenyewe. Tofauti na sisi, watu wengi ambao wanaendesha Bolt siyo wamiliki, ni watu ambao wameenda kuomba ajira kwa wamiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hapo ndiyo changamoto inapoanzia, kwa sababu ule ujira inabidi waugawanye ambao siyo tatizo la Uber. Kwa hiyo, kama mtu hanufaiki siyo tatizo la Uber, ni tatizo la mfumo wenyewe uliopo. Kwa hiyo, kanuni hizi zilitungwa kwa kuangalia juu juu siyo kwa kufanya utafiti wa kina na kuhakikisha kwamba tunalinda makundi yote. Wale vijana ambao wamejiajiri, lakini vilevile na wananchi ambao wanatumia huduma zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, *LATRA* ilibidi wajielekeze kwenye masuala ya muhimu kabisa na kanuni ambazo zinashika mustakabali wa Taifa, kwa mfano, suala la ving'amuzi kwenye mabasi. Ving'amuzi vilivyofungwa kwenye mabasi havidhibiti mwendo, vinatoa tuu *alert* kwamba *speed* imezidi, yaani baada ya pale dereva anakanyaga mwendo kama kawaida. Vinaishia kupigia abiria tu kelele gw'igw'igw'i kwenye mabasi, havidhibiti *speed*. Yaani siku hizi dereva *speed* inazidi 80 anakanyaga mwendo king'amuzi kinalia tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ving'amuzi vilivyofungwa kwenye mabasi havidhibiti mwendo. Labda tufikirie upya kanuni ambazo tumezitunga. Je, tuna ulazima wa kuweka ving'amuzi ambavyo vinadhibiti mwendo ambavyo mtu akizidi 80 gari yenyewe ina-*stabilize* palepale havizidi. Haya ndiyo masuala ya msingi kabisa ambayo mamlaka tulizozipa mamlaka zinapaswa kuyaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku hizi teknolojia zimekuwa, kwa hiyo lazima tuyaangalie masuala haya kwa umuhimu sana, lakini vilevile *control systems* zinafanya nini? Kwa sababu dereva anaongeza *speed* lakini *no control systems*. kwa hiyo, tuangalie ving'amuzi, lakini vilevile *TBS* hawakuthibitisha hivi ving'amuzi, walisema havina ubora lakini vimefungwa kwenye mabasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli mimi napenda kuhimiza mamlaka ambazo Bunge imezikasimu mamlaka ya kutunga kanuni kwa niaba yake lazima zitunge sheria ndogo kwa ufanisi mkubwa na kwa kuzingatia haki, usawa na maslahi ya Watanzania wote kwa ujumla. Kwa kweli napenda kuishauri Serikali masuala haya, kanuni hizi elekezi za *LATRA* ziangaliwe kwa jicho la upekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Francis Mtinga, ajiandae Mheshimiwa Mpina na ajiandae Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo katika suala hili muhimu sana la sheria ndogo ambazo kiuhalisia ndiyo zinazowaongoza wananchi wetu katika kuishi katika maisha ya utawala bora na maendeleo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mawaziri, lakini zaidi nimpongeze sana Rais wangu Mama Samia kwa jinsi ambavyo muda wote amekuwa akiwaza maendeleo ya Watanzania na maisha bora kwa Watanzania. Rais wetu amekuwa halali, hapumziki, kuhakikisha kwamba wananchi wetu tunazidi kupata maisha bora na kwa kweli tuendelee kumuombea Mungu ili atimize lengo lake la kufanya Watanzania tuwe tuna maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo zimetungwa au zipo kwa ajili ya kufanya sheria mama ambazo zinatungwa na Bunge pamoja na kanuni zinazotungwa na Mawaziri ziweze kufanya kazi kiuhalisia katika jamii. Kwa hivyo, sheria hizi zinapokuwa hazina uhalisia zinafanya maisha ya wananchi wetu kuwa magumu na pengine kuingia kwenye hatia bila kukusudia au kuingizwa kwenye hatia au kurudishwa nyuma kimaendeleo. Kwa hiyo, Kamati inaposema kwamba sheria hizi ndogo marekebisho yake yafanyiwe mapema tena kwa *time line* ni jambo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano sheria kwenye *TS No. 105* ya tarehe 25 Februari, 2022 sheria inayotoa mamlaka *The Tax Administration Act* Sura Na. 438 ambayo inaipa sheria ndogo *The Tax Administration of Tax Ombudsman Service Regulation* ya 2022 kanuni ya sita inakataza mtu aliyeajiriwa kuwa mchunguzi wa kikodi wa masuala yote ya matatizo ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu kwamba wafanyabiashara wamekuwa na matatizo mengi kuhusiana na kodi, sasa yuko mtu hapa anaitwa *ombudsman* ambaye kazi yake ni kuchukua yale matatizo yote ya wafanyabiashara halafu anapochukua haya matatizo anayakabidhi kwa Waziri, ili Waziri aweze kuchukuwa hatua katika sehemu zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu huyu anaambiwa kwamba kwa kufanya kazi hii asifanye kazi nyingine yoyote inayompatia kipato cha mshahara anapofanya kazi hii. Kazi nyingine yoyote, lakini kanuni hii wala haijaeleza kwamba kazi zipi labda zinazoingiliana na kazi yake ile ya kupokea matatizo ya kikodi, imemzuia moja kwa moja. Kiuhalisia unaona kabisa kanuni hii haitekelezeki ina maana huyu mtu yaani anakuwa amekaa tu yani hata kuandika *write up* labda amuandikie mtu afanye biashara haruhusiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kanuni hapa ailezi zile kazi hasa ambazo zina muingiliano na kazi yake ya kupokea matatizo ya kikodi imeacha tu wazi. Kwa hiyo tunaposema kanuni kama hii irekebishwe maana yake inampa mtu huyu utata, aidha, atakuwa lofa zaidi au kiuhalisia atafanya kazi kinyume kwa sababu kanuni haijamueleza kwamba kazi zipi hasa zinazoingiliana na kazi yake ya kupokea matatizo ya kikodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapo hapo katika kifungu kinachohusu *Administration Tax Ombudsman Service Complain Procedure Regulations of 2022* ambazo zimetungwa chini ya kifungu cha 28(g) kwamba huyu mtu akisha *collect* matatizo anamkabidhi Waziri, Waziri aweze kutoa maelekezo kwenye mamlaka kwa mfano *TRA* kuchukua hatua juu ya matatizo ya kikodi ambayo ameyapokea kutoka kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kanuni haijambana Waziri ndani ya muda gani aweze kutoa hayo maelekezo, kwa hiyo, Waziri anaweza

akachukuwa akatia kwenye *draw* akaendelea na shughuli zake zingine, mwezi, miezi, mwaka wakati tatizo lile la kikodi kwa wale wafanyabiashara linawasumbua, pengine limefanya wengine wanafilisika kwa sababu tayari sheria zile zinaendelea kutumika wakati marekebisho, yanasubiliwa lakini sheria zinaendelea kutumika kwa sababu zimeshaanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kifungu hakijambana Waziri kwamba unapaswa sasa umeshapokea haya matatizo toa maelekezo ndani ya miezi mitatu, ndani ya mwaka. Kwa hiyo tunaposema kwamba marekebisho haya yafanyike haraka na ninashukuru kabisa kwamba Kamati imetoa mpaka muda maalum kwamba ndani ya muda fulani marekebisho yawe yamefanyika kwa sababu hivi vitu vinawaumiza watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mtu analalamika labda anatozwa kodi kubwa kutokana na biashara anayofanya Waziri ameshapelekewa, ametia kwenye *draw,* hakuna kifungu kinambana, mwaka unaisha, mwisho mtu anafilisika. Kwa hiyo, utaona kabisa kwamba ni kifungu kidogo sana, lakini kimesababisha maisha ya watu wengi kuharibika kama hakijafanyiwa marekebisho ndani ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo wamesema wenzangu hapa zipo sheria kama hizi kwenye halmashauri, kwa mfano halmashauri inakuambia sasa utafuata kalenda kipindi cha kulima mahindi kimefika utalima mahindi, sasa mtu unakuta ana shamba la umwagiliaji, ana maji anataka kulima nyanya kalenda ya halmashauri inamwambia sasa unatakiwa ulime mahindi. Sasa huyu mtu unamtia umaskini, pengine ndio kipindi ambacho nyanya zinahitajika kwa wingi kalenda haisemi inakuambia tu ni kipindi cha kulima kitu fulani, kwa hiyo unakuta ni sheria ndogo imetungwa kwa lengo zuri, lakini kwa sababu haina uhalisia inasababisha maishi magumu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaposema kwamba kanuni hizi zifanyiwe marekebisho haraka ni mambo ambayo yanawagusa wananchi, halmashauri inasema utafuga kwa idadi maalum, sasa unampangia mtu utajiri! Yaani mtu ana uwezo wa kufuga ng'ombe 1,000 wewe unataka unamwambie afuge ng'ombe wanne kwa hiyo sasa ina maana sheria sasa inaanza kubana watu wasitajirike wakati sisi tunataka watu watajirike, nchi ipate kodi na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo utaona hizi sheria ndogo zisipoangaliwa vizuri zinaweza zikasababisha umaskini ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, Maazio ya Kamati yanaposema sasa marekebisho yafanyike haraka na inaweka na muda tujue kabisa tunagusa mambo ya wananchi kuweze kuishi maisha bora waweze kupata utajiri na nchi iweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilitaka nisisitize hilo kwa kuunga mkono hoja kwamba hizi sheria ndogo ndio *engine* ya kufanya sheria mama zifanye kazi, ndio *engine* ya kufanya kanuni zile za Mawaziri zifanye kazi na niwaombe basi na hawa Mawaziri wanapotunga hizi kanuni wawe wanakumbuka kabisa wanaenda kugusa maisha ya watu na wasitoke nje ya sheria mama ambayo inakuwa imetungwa humu ndani ya Bunge na mara zote sheria zinazotungwa humu haziendi kuwakandamiza wananchi bali kuwaletea maendeleo katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba niunge mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mpina, ajiandae Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa nafasi hii ambayo umenipatia na mimi niweze kuchangia hii taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo na mwanzo kabisa nimeshindwa kujizuia kuwapongeza sana Kamati hii ya Sheria Ndogo kwa uchambuzi wao mzuri sana wa hizi sheria na kasoro zilizokuwepo pamoja na mapendekezo ambayo wameyapendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imeelezwa hapa na Kamati kwamba hili suala la sheria ndogo ni suala ambalo ni muhimu sana, ni suala ambalo kama lisiposimamiwa vizuri linaweza kwenda kupoteza hata maana ya sheria zenyewe ambazo zilitungwa na kupitishwa na Bunge hili tukufu. Sasa tusipoliwekea maanani na msimamo mzuri kuanzia kwenye mfumo wa utungaji wake na mpaka utekelezaji wake, tunaweza tukawa tunapiga *mark time* kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri sana kamati hapa imefanya uchambuzi na imefanya uchumbuzi wa sheria wa kanuni kama 14 lakini ukweli ni kwamba sheria ambazo zina changamoto nyingi, ni nyingi sana kwa hiyo hizo ni 14 ni sehemu ndogo sana ya kanuni ambazo zina kasoro na zinazohitaji marekebisho. Kwa hiyo, ina maana kwamba hii Kamati ya Sheria Ndogo pamoja na kazi nzuri sana ya kufanya uchambuzi wa kanuni 14 katika taarifa hii lakini bado wana kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba zile kanuni zote zenye changamoto ambazo zinaleta mkanganyiko mkubwa kwa wananchi katika utekelezaji wake zinashughulikiwa na zenyewe zinafanyiwa uchambuzi na kuletwa hapa Bungeni kwa ajili ya kufanyiwa uamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubaliana nao, kwa mfano wametolea mfano kukinzana na masharti ya sheria inayotoa mamlaka ya kutunga sheria ndogo na sheria nyingine za nchi. Hizi tunazo nyingi sana na bahati mbaya sana Kamati wao wamezungumzia suala la sheria ndogo tu

lakini kuna waraka nao ambao ukiandikwa na Katibu Mkuu, kuna waraka nao ukiandikwa na Waziri unaenda kutumika na wenyewe kama sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hizi sheria ndogo pamoja na waraka zinapoenda kule zinaenda kwenda ku-*distort* au kuharibu kabisa hata mifumo ya sheria ambayo ilishawekwa na zingine zimekuwa zikienda hata tofauti kabisa na sheria zenyewe zilizopo sasa kwa mfano kipindi cha UVIKO - 19 tunatekeleza miradi ya UVIKO-19 kuna baadhi ya taasisi hapa ziliandikia taasisi nunuzi barua za kuwataka wakafanye manunuzi kwenye viwanda fulani kwa kuvitaja kwa jina na hayo yalifanyika huku wakijua Sheria ya Manunuzi hairuhusu hilo hayo yalifanyika huku wakijua Sheria ya Ushindani Na. 8 ya mwaka 2003 hairuhusu hilo, lakini yalifanyika na sheria zipo, kuja huku kwenye waraka wakaandikiwa barua ya waraka wahusika wafanye manunuzi katika maeneo hayo, kuja huku ikatekelezwa hivyo hivyo ilivyotekelezwa kinyume cha sheria na kinyume cha utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pale Mvomero kuna kijiji kimoja katika Wilaya ya Mvomero wametunga sheria kwamba mifugo hairuhusiwi kuwepo kwenye kijiji hicho huku wakijua wananchi wanayo ruksa kwa mujibu wa Katiba ya nchi kufanya shughuli za kiuchumi zozote wanazozitaka. Sasa unatunga sheria inasema kwenye kijiji husika hakuna mfugaji kuingia, inatungwa, kanuni inafanya kazi ya muda mrefu na watu wamekuwa wakipigwa faini ya mamilioni ya fedha wakiingiza mifugo kwenye eneo hilo, jambo ambalo linakiuka Katiba, jambo ambalo ni uonevu na manyanyaso kwa wananchi wasiokuwa na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kanuni hizi ndogo ndio zimetufikisha kwenye kasoro nyingi, mrundikano wa tozo na kodi nyingi katika eneo moja zinatungwa kila taasisi inatunga, *TBS* anatunga, *TMDA* anatunga na taasisi zingine zenyewe zinatunga kwenda kusimamia jambo moja, kijiji kina kodi eneo husika, halmashauri ina kodi kwenye eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka zingine zinazosimamia *NEMC* mlolongo huu wote umetufikisha hapa katika mfumo mzima wa utungwaji wa hizi kanuni na sheria zetu ndogo.

Sasa nasema nini; mfumo wa utungaji wa hizi sheria ni bora tuanzie pale, mfumo wa utungaji wa kanuni za hizi sheria ndogo ukoje utaratibu wa sasa sheria hizi kanuni ndogo hizi zinatungwa na taasisi kwa mfano Serikali ya Kijiji, Halmashauri ya Kijiji, lakini na Waziri kutunga sheria ya utekelezaji wa baadhi wa sheria, na anapomaliza kutunga na ana-*gazette* kwenye Gazeti la Serikali na baada ya kuwa *gazetted* kwenye Gazeti ya Serikali ndio Kamati yetu ndogo inarudi kuzipitia na kubaini kasoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nauliza leo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Bunge hili na wewe mwenyewe Naibu Spika, kwani kuna

shida gani hizi kanuni ndogo zikafanyiwa mapitio na Kamati yetu ndogo ya Sheria Ndogo kabla hazijaenda kuwa *gazetted* kwenye Gazeti la Serikali ili changamoto leo tunazojiuliza leo ziwe zimeshapata *oversight* mapema kabla hazijaenda kwenye utekelezaji wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hapa imezungumza na sisi wote ni mashahidi kwamba hizi sheria ndogo zimeenda ku-*distort* hata sheria yenyewe iliyotungwa, zimeenda kufifisha sheria yenyewe, nguvu ya sheria imeenda kufifishwa kwa kutunga sheria ndogo, lakini pia zimeenda kutungwa hata sheria ndogo ambazo ni kinzani na hata ile sheria mama, na kwa kufanya hivyo wananchi wengi wamepata mateso makubwa kwa sababu wameenda kuadhibiwa kwa kosa ambalo hata linakinzana na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia inazuia hata utekelezaji wa sheria yenyewe lakini Serikali tumekuwa tukishindwa kesi nyingi sana Mahakamani kutokana na haya, ukienda kutafsiriwa sheria Mahakamani *vs* hatua iliyochukuliwa kwa kanuni kwa sheria ndogo Serikali inatangazwa kushindwa wakati mwingine tunafidia mabilioni ya fedha kwa hizo *technical* zilizofanyika katika utungaji na uchukuaji wa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali hiyo lakini pia tumeelezwa hapa hata inapotekea kasoro kurekebishwa hazirekebishwi kwa wakati, sheria ndogo ina kasoro, Kamati imeita mamlaka husika, wamekaa nayo, wamezungumza na wamekubaliana, lakini miezi minne tunaambiwa na Kamati hakuna marekebisho, hayafanyiki, inachukua muda mrefu kufanya marekebisho. Sasa kama haya yote yanafanyika na tunaenda kuwaadhibu wananchi wasiokuwa na hatia na tunaenda kuiingiza Serikali hasara kubwa kwa nini hizi sheria ndogo Bunge hili likakasimu madaraka, kwa hiyo Kamati ya Sheria Ndogo kushughulika na hizi sheria ndogo kabla hazijaenda kwenye utekelezaji ili kuweza kuepuka hizi hasara ambazo tunawezakuwa tunazipitia za kunyika haki watu, lakini pia za kuleta mkanganyiko hata tafsiri ya sheria Mahakamani na kusababisha wakati mwingine watu wengine kukosa haki na kusababisha hata Serikali yenyewe kushindwa baadhi ya kesi mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tusipofanya maamuzi ya namna hiyo ninajua kwamba sheria ndogo hizi hata wakati mwingine kwa mfano kuna mambo tunapitisha humu kama Bunge na mnayapitisha mpaka kwenye bajeti, mnayaweka mpaka kwenye bajeti, halafu baadaye inaamuriwa kwamba kuna maeneo ya sheria ambayo yanarusu Waziri ataenda kutunga sheria ndogo kule, mwisho wa siku Waziri huyo huyo anaenda kufuta baadhi ya hata ya tozo ambazo mlikubaliana humu Bungeni kwa mamlaka hayo aliyonayo kupitia hiyo sheria ndogo bila hata *consultation* ya Bunge mambo ambayo yanaenda hata kuathiri bajeti yenyewe iliyopitishwa na Bunge, mambo ambayo yanaenda kuleta hasara

kubwa kwenye Taifa na mkanganyiko mkubwa wa mhimili wa Bunge pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine ambalo ninaomba Kamati ya Sheria Ndogo ikaliangalie ni utekelezaji wa *force account*. Suala hili la utekelezaji wa *force account* sasa hivi lina changamoto kubwa, leo hii mradi unapelekwa kwenye shule husika wa madarasa, mwalimu mkuu wa shule hiyo na mwalimu mwingine kila leo mguu na njia kwenda kufanya manunuzi, hawafundishi watoto wapo safari na njia kwenda kufanya manunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kwa madaktari zahanati ni moja, mnajenga pale nyumba ya mtumishi, daktari wa eneo hilo kila siku anaenda kwenye manunuzi, akileta mbao leo anaambiwa rangi imeisha, akimaliza kuleta rangi anaambiwa *cement* imeisha, kila leo yuko safari. Madaktari wetu wagonjwa wetu awatibiwi kwa sababu madaktari wameshapewa kazi nyingine ya manunuzi, kazi nyingine ya kusimamia ujenzi badala ya kazi ambazo husika walizopewa kuzisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kanuni ya sheria ya manunuzi ambayo ndio ina utekelezaji wa *force account* ni muhimu sana iende ikatizamwe upya, lakini hili suala la *force account* linatuletea hasara nyingi. Leo hii mradi ukiwa unatekelezwa kwa sababu unasimamiwa na watumishi wa umma maana yake kama ni kwenye halmashauri Mkurugenzi mguu na njia anaenda kuukagua mradi huo, *engineer* mguu na njia anaenda kukagua mradi huo, Afisa Elimu kama ni wa elimu mguu na njia kila siku anaenda kukuagua mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo watumishi karibu halmashauri nzima yote wako barabarani na jana Waziri wa Fedha ametuthibitishia hapa kwamba sasa hivi kuna gharama kubwa sana ya matumizi ya *force account* kwa sababu ina *involve* usimamizi wa watu wengi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninyi mnasema mmepunguza gharama, lakini ukweli kwamba hakuna miradi yenye gharama kubwa kama ya *force account* na inakwepa vitu vingi kwenye *force account* tunajinyima sisi wenyewe kwa sababu hata *VAT* hatulipi, kama angekuwa *contractor* pale hata kama ni mdogo namna gani angelipa *VAT*. Lakini sisi tunajidanganya, mradi umetekelezwa kwa fedha ndogo kwa sababu tumekwepa kulipa kodi sisi tunajidanganya mradi umetekelezwa kwa fedha ndogo lakini ukichukulia fedha ya mafuta, ya madiwani kwenda kukagua mradi huo, Mkurugenzi Injinia, Afisa Elimu sijui nani gharama zake ni kubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na hasara nyingine pale inapotokea sasa mradi umejengwa chini ya viwango, nani anakamatwa sasa, nani analipia kama ni mkandarasi tungeweza kumwambia mkandarasi kwamba

mradi huu aurudie, abomoe na ajenge upya. Sasa leo umejengwa kwa *force account*, baada ya mwaka mmoja jengo limebomoka, tunaenda kumkamata nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukamkamate Mkurugenzi Mtendaji, tukamkamate Mganga, tukamkamate nani inahusisha mlolongo mkubwa wa watumishi wa Serikali inahusisha mlolongo mkubwa wa wananchi katika jamii husika. Tunaenda kumkamata nani?

Sasa mimi niombe sana hizi kanuni zilianzishwa kwanza Kamati yetu ya Sheria Ndogo ikajiridhishe na matakwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mpina muda wako umekwisha**.**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ajiandae Mheshimiwa Jenista na ajiandae na mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii, pia napenda sana kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Sheria Ndogo ikiongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza sana uchambuzi ambao umefanywa na Kamati pamoja na maazimio ambayo yametolewa. Sisi tunafarijika kwamba katika sheria mama nyingi tulizonazo takribani 446 na sheria ndogo zaidi ya 40,000; dosari ambazo zimeendelea kujitokeza zinaendelea kupungua kadri ya hatua mbalimbali zinavyozidi kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa ushahidi ambao Kamati inapochambua inakutana nayo, inatufanya sisi Serikali/Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuona bado tunao wajibu wa kuhakikisha kwamba sheria zetu zinazotungwa kwa mujibu wa Katiba yetu na sheria zetu zinakidhi yale matakwa na malengo ambayo pale zimetungwa. Kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba dosari ambazo zimetajwa, zinaendelea kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Chamuriho katika mchango wake amedhihirisha hii kwa kueleza kwamba wamepitia sheria ndogo nyingi lakini dosari zikawa chache. Kwa hiyo, kati ya mambo ambayo Serikali inayafanya kwa sasa mojawapo ya Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakamilisha mwongozo ambao utatumika kuongoza mamlaka zinazotunga sheria ndogo katika ngazi ya halmashauri, Mawizara na mamlaka zingine

kwa wote ambao walio na dhamana tunaamini mwongozo huu pamoja tunaamini mwongozo huu pamoja na mambo mengine utajaribu kutoa maelekezo kwa mambo yale ya msingi ambayo kwayo wote walioko na dhamana wanatakiwa kuyazingatia, hili nafikiri mwongozo ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili utaendana na jitihada za Serikali za kuona jinsi ambavyo tutaendelea kutoa elimu kwa wote ambao walio na dhamana ya kutunga sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kwamba sheria yoyote sheria mama nyingi mchakato wake unahusisha tafiti na mawasilisho katika hatua mbalimbali kitu ambacho ni tofauti kidogo na sheria ndogo, kwa hiyo tunaona upo umuhimu kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia kuona kwamba umuhimu wa kutoa elimu, lakini na hata kutafuta utafiti ni jambo ambalo litahitaji kuachwa nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi yangu kwa sasa na Waheshimiwa Wabunge inamalizia kufanya usajili wa wanasheria wote walio kwenye huduma ya umma na mpaka kufikia sasa tuna wanasheria 2,550 na hawa wamo pamoja na hizi waliomo kwenye halmashauri na mwezi huu tutazindua *Public Bar Association* (Chama cha Mawakili wa Umma Tanzania). Lengo lake moja wapo ni kuhakikisha kwamba wanasheria wote tulionao kwenye huduma umma wanakuwa na kiwango kwa maana ya kuwa na elimu na kuongeza stadi zao za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kupitia hatua tunazozichukua tunaamini tutaendelea kujitathimini jinsi ambavyo hatua tunazozichukua kwa kuhakikisha wanasheria walioko kwenye Halmashauri, walioko kwenye Mamlaka za Mikoa na walioko kwenye Mawizara pamoja na hata zile taasisi kubwa, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali *(Solicitor General)* na Ofisi yangu kwa pamoja tuhakikishe kwamba kila mmoja wetu anatimiza wajibu wa kuhakikisha kwamba sheria zinazotungwa na Bunge hili basi ziwe zile zile na zenye ubora lakini na sheria ndogo zinazotungwa ziwe zinaendana na masharti mama yaliyo kwenye sheria kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pia nitoe rai ofisini kwangu kuna mfumo wa kieletroniki ambao ukiingia kuna sehemu ya mrejesho, ningefikiri hili ni eneo mojawapo la kusaidiana kwa wale wote ambao wanahusika na kazi za kisheria na huduma za kisheria na changamoto za kisheria mambo mengine si ya kusubiri yakaenda na urasimu mrefu, haihitaji kuweka neno la siri yaani *password* kuingia kwenye ile fomu ya mrejesho na sehemu ya mwisho ya ile fomu ofisi yetu inapenda kujulishwa jambo lolote na maoni yoyote ambayo mtu anaweza akaandika na akapata mrejesho.

Kwa hiyo, hizi ni njia ambazo naamini nazo tutajaribu kuona, tunaamini sisi kwamba tukizitumia vizuri zitaongeza thamani ya huduma ambayo inatolewa na Serikali upande wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo lingine ambalo nifikiri halijazoeleka sana kwa hizi sheria ndogo; kwa sheria mama mara nyingi mnaona Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge tunakuja na sheria na miswada ya sheria mbalimbali. Kwa sheria ndogo marekebisho mengi au kufuta sheria ndogo zilizokwisha kutungwa ni zile nyingi tulizopokea hasa kwenye Mawizara, naona kutoka halmashauri ni mara chache sana, basi ningetoa rai tu kwamba tusisubiri na kuelezea sana maumivu yanayotokana na dosari zile za msingi ziko kwenye sheria ndogo taratibu zingine za kufahamisha ofisi yangu, Wizara ya Katiba na Sheria na mamlaka zingine nafikiri zichukuliwe haraka kama walivyo madaktari wowote wanaotibu binadamu tusisubiri ugonjwa mpaka unakuwa mkubwa au kuna kuwa na madhara haki za watu kupotea bila kuchukua hatua ambazo kumbe tungepata taarifa tungechukua hatua ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naishukuru na kuipongeza Kamati kwa mapendekezo yake na mimi kama sehemu muhimu katika utekelezaji wa maazimio haya upande wa Serikali nitashirikiana na wenzangu wote wa Serikalini kuhakikisha huo muda walioutoa tutafanya linalowezekana kupunguza dosari zilizojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa *AG*, ahsante sana kwa mchango wako na kwa njia uliyoitoa na kwa Kamati, AG ameshakubali marekebisho yote ya haraka mpelekeeni mkae naye yafanyiwe kazi, kwa sababu kipindi kirefu sana haya marekebisho hayafanyiki.

Ahsante sana kwa mwongozo huo kwa kweli umetusaidia sana kurekebisha mambo mengi ambayo yanaleta ukakasi kwa wananchi na hasa kwenye uwekezaji. Mheshimiwa Jenista, ajiandae mtoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na *Government Chief Whip* ninaomba nichukue fursa hii na mimi kusema maneno machache na hasa nikizungumza pia kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ni utamaduni ulio mzuri kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema na kutuwezesha kuwa hapa na tunaendelea na ajenda katika mkutano huu wa Bunge. Lakini naungana na Waheshimiwa Wabunge pia waliochangia awali bila kusahau kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

na Amiri Jeshi Mkuu kwa kazi nzuri anazozifanya na hasa katika kuhakikisha kwamba ameendelea kuwa mzalendo mwenye maono ya kuliongoza Taifa letu na kuendelea kutoa miongozo mbalimbali kwa viongozi na hata sisi Mawaziri ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na ustawi wa taifa letu na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati Dkt. Jasson Samson Rweikiza kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Kamati yake, lakini pia akisaidiana na ndugu yangu Kilumbe Shabani Ng'enda ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati, lakini vilevile wajumbe wa Kamati hii ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kazi inayofanywa na Kamati hii ukiangalia juu juu unaweza ukaona ni kazi ndogo, lakini ni kazi kubwa sana na inatija kubwa kweli kwa ustawi wa Taifa letu. Kwa hiyo, nawapongeza sana wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa mnayoifanya katika kuhakikisha kunakuwa na utawala bora, haki na usawa katika utendaji wa kazi ndani ya Serikali na katika kusimamia maslahi ya Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani ninawiwa pia kuwapongeza sana watumishi wa Serikali na hasa ambao ni wanafanya kazi kwenye Kitengo cha Sheria wale ambao wamekuwa wakihakikisha kwamba wanatekeleza wajibu wao sawa sawa kwa kufuata sheria, taratibu, Katiba na kanuni zilizowekwa ili kutunga sheria ndogo ambazo zinahakisi mwenendo mzima wa usimamizi wa majukumu ya kila siku katika maeneo yao. Kwa kweli tunawapongeza sana watumishi hao kwa sababu wanasheria wetu katika maeneo mbalimbali kama ilivyosemwa na Kamati hapa kwamba kuna sheria nyingi ambazo zimekuwa zikipelekwa kwenye kamati hii ya sheria ndogo lakini unakuta si sheria zote ambazo zimekuwa na matatizo makubwa.

Kwa hiyo, kama kuna sheria ambazo hazina matatizi ina maana kuna timu ya watumishi wa umma wanasheria ambao wanafanya kazi zao kwa ufasaha ni lazima tuwapongeze sana hao kwa kazi hizo na tuwaombe wale ambao wamekuwa wakiwa wakijirudia kuwa na makosa ya uandishi wa sheria na makosa mengine kujirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawasilisha nakala ya matoleo ya Magazeti ya Serikali hapa Bungeni na hiyo inapelekea kuwa na mjadala kupitia sheria ndogo na hasa kwa msingi wa Kikatiba wa kukaimu na kukasimisha madaraka haya ya utungaji wa sheria kwa taasisi mbalimbali kupitia ndani ya Serikali na ninaomba nichukue nafasi hii kuungana na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba tumepokea maelekezo ya Kamati kama yalivyowasilishwa kwenye taarifa hii ya Kamati na sisi kama Serikali tunakila sababu ya kuyafanyia kazi na kwa maana hiyo basi kwa niaba ya *Chief Whip* - Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu ninaomba nitoe

maelekezo yafuatayo kwa watendaji wote wa Serikali ambao wanahusika na maelekezo haya na maazimio haya ambayo yako ndani ya hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ni kuhakikisha wanatii na kutekeleza agizo la Kamati la muda uliowekwa kuhakikisha kwamba sheria ndogo zote zenye dosari zinarudishwa hapa Bungeni mapema ili ziweze kukaguliwa na kuondolewa dosari zilizokuwepo. Kwa hiyo, eneo hilo ni lazima mamlaka zote zilizokasimiwa utungaji wa sheria hizo ninaomba sana wafuatilie mjadala huu na wapokee maelekezo ya Serikali na wahakikishe wanatekeleza jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili ninaomba niendelee kuziagiza na kuzisisitiza mamlaka zote zilizokasimiwa kazi hii ya utungaji wa sheria ndogo kuhakikisha kwamba wanazingatia Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyopendekezwa na Kamati na kuendelea kuhakikisha kwamba wanapunguza dosari zinazoonekana katika sheria ndogo zikigongana na matakwa ya Kikatiba kwa hiyo jambo hili pia lizingatiwe sana na timu ya wanasheria wetu na mamlaka zilizokasimiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika mjadala tumeona hapa zimesemwa baadhi ya sheria ambazo kwa kweli zinakiuka misingi kwa namna moja ama nyingine ya haki ambazo zingeweza kuwa ni haki za msingi kwa Watanzania na wananchi wanazotumia sheria hizo ndogo. Kwa hiyo tunaendelea kuziagiza hizo mamlaka kuzihakikisha sheria ndogo zinazoenda kurekebishwa zikaandaliwe na kutengenezwa zikiwa na uhalisia wa maisha ya Watanzania katika kuwezesha maisha ya Watanzania kuakisi sheria mama ambazo zimetungwa na siyo kuleta migogoro na migongano ya utendaji wa kazi wa sheria katika maeneo mbalimbali na hapa leo tumeona sheria ndogo za *LATRA* zimesemwasana hapa ndani na ni kama vile zilienda kuibua sintofahamu katika utekelezaji wake katika jamii. Kwa hiyo, tunaomba marekebisho hayo yatakapofanyika yahakikishe kwamba hayaibui tena migogoro ya namna hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tunaendelea kuwakumbusha mamlaka zetu kuhakikisha wanapotunga hizo kanuni ama sheria ndogo ziwe na uhalisia wa mambo ambayo yanaendana na hali halisi ya uchumi wa nchi kwa Taifa letu na tumesikia hapa baadhi ya Wabunge wakitukumbusha kwamba sasa hivi tumeamua uchumi wa taifa hili uwe ni uchumi wa kidijitali tunaenda kwenye mitizamo ya ki-TEHAMA, kwa hiyo kila sheria ambayo tunaitunga ni lazima itakuwa na *component* hiyo ya ki-TEHAMA, kwa hiyo na sheria ndogo ziakisi mwelekeo wa uchumi wa Taifa letu ambao tunao kwa sasa.

Lakini tunaendelea kuagiza na kuwakumbusha kuhakikisha wanatunga sheria ndogo zenye usahihi na ufasaha wa uandishi wa majedwali ya sheria

ndogo na hasa kurejea kanuni husika na sheria husika katika kuyatengeneza majedwali hayo, jambo hilo pia watakapokuwa wanarekebisha sheria hizo ndogo wahakikishe wanazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine tunaendela kuwakumbusha kuzingatia misingi ya uandishi wa sheria ambayo imewekwa katika taratibu mbalimbali ambazo zinatumika katika uandishi wa sheria nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, na jambo lingine tunaendelea kuwakumbusha kuwasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kila eneo ambalo lina matatizo wawasiliane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupata miongozo na kuhakikisha kwamba matatizo haya ya uandishi wa sheria ndogo ambazo zimeshindwa kuakisi sheria mama na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jambo hili linaondoka kwa haraka na ikiwezekana tuendelee kupunguza sheria zenye makosa mengi zinapowasilishwa hapa ndani ya Bunge lako tukufu kwa kupitia Kamati ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimalizie kwa kusema kwamba Serikali itaendelea kujitahidi kusimamia taasisi zote zinazohusika na mamlaka hii ya uandishi wa sheria ndogo ili kuhakikisha kwamba utawala wa sheria unachukua nafasi yake ndani ya nchi yetu, lakini utawala bora pia unachukua nafasi yake ya kutosha ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaendelea kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali tupo tayari kushirikiana kwa karibu na Kamati ya Sheria Ndogo kuhakikisha kila jambo linakwenda sawasawa kwa ustawi wa nchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawapongeza tena Kamati ya Sheria Ndogo na tunawahakikishia kwamba tutaendelea kushirikiana nao. Ahsante sana naomba kuunga mkono hoja ya Kamati hii ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jenista kwa mchango mzuri na Serikali kuwa wapo tayari kurekebisha sheria zilizoibuliwa na Kamati ya Sheria Ndogo. Mtoa Hoja.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu na nipende kusema kwamba nawashukuru sana Wabunge kwa michango mbalimbali mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata wachangiaji wa kuzungumza kumi na kwasababu siyo wengi naomba niwataje; Mheshimiwa Edwin Swalle, Mheshimiwa Simai Sadiki, Mheshimiwa Amour Mbarouk, Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Dkt. Leonard Chamuriho, Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Francis Mtinga, Mheshimiwa Luhaga Mpina na Mheshimiwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimishimiwa Feleshi na Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana kwa michango yao mizuri waliyoitoa ambayo kwa kweli imekuwa kwanza wanaunga mkono hoja yetu, lakini wanaboresha pale ambapo panastahili na panawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kazi za kutunga sheria ni ya Bunge, sheria zote, sheria mama, sheria ndogo zote ni ya Bunge, lakini Bunge limekasimu kazi hii kwa mamlaka mbalimbali kwa sababu ni nyingi sana, inahusu sheria zenyewe, sheria ndogo, sheria kubwa zenyewe, sheria mama. Amesema Mheshimiwa Mpina zile zote zimo waraka, matangazo, amri, kanuni ile nyingine *proclamation* zimo kwenye sheria ndogo, zote zimo zinahusu humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Bunge haliwezi kutunga sheria zote hizi peke yake likamaliza, lazima likasimu kwenye mamlaka mbalimbali Halmashauri, Wizara mbalimbali, idara mbalimbali ili kazi hii iweze kutendeka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa lengo la sheria ndogo hizi zote nilizozitaja zikiwemo na waraka na nyingine hizo ni kusaidia kutekeleza sheria mama, kuzifafanua vizuri zaidi ili zieleweke vizuri, kurahisisha utekelezaji wa sheria mama, si kuzikwamisha au kuweka masharti ambayo yanaleta ukinzani kwenye sheria mama au yanakwamisha ufanisi na maslahi ya Watanzania na urahisi wa Maisha, ni kurahisisha sheria zenyewe ziweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunawaomba watungaji wale wa sheria ndogo wawe makini, kule kwenye mamlaka kwenye halmashauri kwenye wizara kuna wanasheria kule wanaweza kufanya kazi hii kwa umakini na waondoe hizi kero ambazo tumezibainisha hapa na Wabunge wamechangia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kama niliousema hapa sheria mama inasema kwenye kosa fulani adhabu ni shilingi isiyozidi shilingi 300,000 au kifungo kisichozidi miezi 15; sheria ndogo inakuja inasema kwenye kosa hilo hilo adhabu isiyopungua shilingi milioni tatu au kifungo kisichopungua miaka mitano. Sasa unashangaa hii sheria ndogo ya namna gani inakinzana na sheria mama na inaongeza adhabu kuliko ilivyosema sheria mama, hii siyo sawa sawa huu ni ukiukwaji ambao upo dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Kamati inachofanya sisi tunachambua hizi na kubainisha mapungufu haya na makosa haya ambayo yamo na kuyarekebisha na kwamba tunawaambia wale warekebishe. Tatizo ni kwamba kama nilivyosema hapo mwanzoni tunawapelekea maelekezo

hawaleti, ndiyo maana tumesema hapa angalau ikifika Novemba na Desemba tarehe 1 wawe wameleta. Sasa inavyoonesha kwamba itabidi tuanze kwenda kule kwenye hizo Wizara kuchunguza kwa nini hamjaleta, hili tuliwaelekeza hamjaleta mpaka leo watupe majibu; kama yanaridhisha kama hayaridhishi sisi tutawaambia maana yake inachafua taswira ya Bunge. Mwananchi akiumia kule analaumu Bunge halaumu ile mamlaka kule anasema Bunge hili namna gani imetunga sheria mbovu ambayo haitekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumemsikia Mheshimiwa Kapinga hapa anaongelea Bolt na Uber zimefunga kabisa biashara zao ambayo ilikuwa ni huduma nzuri, inagharama nafuu kwa mwananchi, unapiga simu dakika mbili umeshapata huduma, sasa hiyo imesimama; hii siyo kuboresha maslahi ya Watanzania au ufanisi wa maisha kuwa mazuri ni kukwamisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ndogo hazina lengo hilo, wale wanaotunga hizo sheria wajitahidi kuzingatia sheria mama, kuwa na utu, kupenda maendeleo na si kukwamisha maendeleo. Wajitahidi kufanya hiyo kazi kwa umakini mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa maelekezo waliyoyatoa hapa kwanza wamekubali kwamba kuna dosari ndogo ndogo, nawashukuru sana kwa kazi waliyoisema kwamba wataenda kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pia mwishoni kwa kumalizia kwamba dosari hizi si nyingi sana, zimepungua sana kadri tunavyokwenda mbele, mwanzoni zilikuwa nyingi sana sasa zimepungua na nitumie nafasi hii kuwapongeza wale ambao wanatunga sheria nzuri kwenye mamlaka mbalimbali huko kwenye halmashauri na sehemu nyingine wanajitahidi sana kufanyakazi nzuri ambayo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Sita na Mkutano wa Saba na Bunge pamoja na uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Tatu na Mkutano wa Nne wa Bunge.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda na Maazimio haya yamepita.

Waheshimiwa Wabunge, nimshukuru sana *Attorney General* kwa kutoa mwanga mzuri sasa Kamati sheria zote zile ambazo zina ukakasi zipelekeni moja kwa moja kwa *Attorney General* ili ziweze kufanyiwa kazi na zirekebishwe. Haya mambo yapo sana huko juzi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha ametangaza hapa kuwa kupata leseni si lazima uanze kulipa *provision,* lakini ukienda huko halmashauri lazima uanze kulipa *advance payment* mpaka leo bado ipo hiyo pamoja na kauli ya maelekezo uliyoyatoa huwezi kupata leseni mpaka ulipe *advance*. Kwa hiyo, bado inabidi mahusiano huko yarekebishwe zaidi.

Baada ya maneno hayo nishukuru Kamati kwa kazi nzuri, Mwenyekiti, michango ya wajumbe, naishukuru Serikali upande wa Mheshimiwa Jenista kuiweka vizuri sana na *Attorney General.*

Kwa hiyo, hakuna la ziada zaidi ya tangazo; Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeweka dawati katika viwanja vya Bunge kuanzia leo tarehe 21 Septemba ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kufanya uhakiki wa taarifa za anuani za makazi zilizotolewa mwezi Februari hadi mwezi Mei, 2022.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuhakiki taarifa zenu za anuani za makazi.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 6.43 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 22 Septemba, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*